UBORA WA MAUDHUI YA VYOMBO VYA HABARI TANZANIA

Upembuzi wa Mhimili wa Nne:
Uripoti wa Vyombo Vya Habari Katika Uchaguzi wa Mwaka 2025 Tanzania



1 Abdul Juma Mluya
Democratic Party (DP)

2 Coster Jimmy Kibonde
Chama cha Makini (MAKINI)

3 David Daud Mwaijojele
CCK

4 Doyo Hassan Doyo
NLD

5 Georges Gabriel Bussungu
ADA-TADEA

6 Gombo Samandito Gombo
CUF

7 Haji Ambar Khamis
NCCR-MAGEUZI

8 Hassan Kisabya Almas
NRA

9 Kunje Ngombale Mwiru (AAFP)

10 Majalio Paul Kyara
SAU

11 Mwajuma Noty Mirambo -- UMD

12 Salum Mwalimu
Chaumma

13 Saum Hussein Rashid
UDP

14 Twalib Ibrahim Kadege
UPDP

15 Wilson Elias Mulumbe - ADC

16 Yustas Mbatina Rwamugira -TLP

Upembuzi wa Mhimili wa Nne:
Uripoti wa Vyombo Vya Habari Katika
Uchaguzi wa Mwaka 2025 Tanzania

WAANDISHI

Dr Zacharia Malima
UDSM (SJMC)

Dr Darius Mukiza
UDSM (SJMC)

Njonjo Mfaume
UDSM (SJMC)

WAPITIAJI WA RIPOTI

Prof Michael Andindilile
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM)

Dr. George Gathigi
Chuo Kikuu cha Nairobi (UoN)

MSANIFU KURASA & UBUNIFU

Essy Ogunde
Mshauri Mtaalam

MCHAMBUZI WA DATA NA MSANIFU PICHA

Mustafa Hamza Njozi
Tathmini Consulting Limited

Nuzulack J. Dausen
Nukta Africa

ISBN 978 99 87 710 70 6
All rights reserved.

IMETOLEWA NA

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano ya Umma
S.L.P 4067 Mikocheni B Mtaa wa Makaburi,
Plot Block D, No.34 Simu: +255 (22) 2700756 Dar es Salaam, Tanzania
barua pepe: sjmc@udsm.ac.tz yearbookmediatz@gmail.com

Recommended citation:
Malima, Z., Katunzi, A., Mukiza, D., Mfaume, N. (2025). Watching the Fourth Estate: Media coverage of the 2025 elections in Tanzania. The Yearbook on Media Quality in Tanzania Research Project. University of Dar es Salaam

YALIYOMO

Shukrani		iii
Muhtasari Mahsusi		iv-vi
Kuhusu Mradi wa Yearbook		vii
1.0	UTANGULIZI	01
2.0	USULI	02
2.1.1	Hali ya Vyombo vya Habari na Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025	02
2.1.2	Ithibati ya Waandishi wa Habari na Miongozo ya Uripoti	06
2.1.3	Waandishi wa Habari Waliogombea Nafasi za Kisiasa	08
2.1.4	Mazingira ya Biashara ya Vyombo vya Habari	08
2.1.5	Dhima ya Vyombo vya Habari Wakati wa Uchaguzi	09
2.2	Mfumo wa Kisiasa na Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025: Mwenendo wa Kihistoria	10
2.1.1	Mwenendo wa Ushiriki wa Wanawake kwenye Siasa za Uchaguzi	10
3.0	METHODOLOJIA	12
3.1	Vigezo vya Ubora	12
3.2	Tathmini ya Wagombea	12
3.3	Sampuli ya Vyombo vya Habari	13
3.4	Sampuli ya Maudhui ya Vyombo vya Habari	13
3.5	Uteuzi na Mafunzo kwa Waandishi, Wasimbaji na Wanaorekodi	13
3.6	Udhibiti Ubora wa Kazi Zilizorekodiwa na Usimbaji Wake	13
3.7	Uchunguzi na Uchambuzi wa Data	13
4.0	MATOKEO YA UTAFITI	14
4.1	Muhtasari	14
4.2	Uripoti wa Chaguzi Mbalimbali	14
4.3	Muktadha wa Uripoti	14
4.4	Vyanzo vya Habari	16
4.5	Uripoti wa Vyombo vya habari kuhusu Wagombea	18
4.5.1	Wagombea Urais wa Muungano	18
4.5.2	Uchaguzi wa Rais wa Zanzibar: Uripoti wa Wagombea Wawili Wenye Ushawishi mkubwa	29
4.5.3	Uchunguzi wa Wagombea Ubunge na Vyama Vyao	33
4.5.4	Uchaguzi wa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar	34
4.5.5	Uchunguzi wa Wagombea Udiwani	35
4.6	Uripoti kwa Mada	36
4.6.1	Mada za Uchaguzi	36
5.0	MITAZAMO YA WADAU KUHUSU UCHAGUZI MKUU WA MWAKA 2025	36
5.1	Uhuru wa Vyombo vya Habari na Uhuru wa Kihariri	37
5.2	Hofu, Vitisho na Kujidhibiti Binafsi	37
5.3	Kukosekana kwa Usawa wa Kisiasa na Mwonekano wa Vyama	38
5.4	Kuzimwa kwa Intaneti na Kuvurugwa kwa Mtiririko wa Upashanaji Taarifa	39
5.5	Ukosefu wa Uwajibikaji na Utendaji wa Uripoti	40
5.6	Usalama wa Waandishi wa Habari na Changamoto za Kiulinzi	40
5.7	Ujumuishaji, Mienendo ya Kijinsia na Ufuatiliaji	41
5.8	Udhaifu wa Kiuchumi na Shinikizo la Kibiashara	42
5.9	Mageuzi ya Kiudhibiti na Uhalali wa Kitaasisi	42
6.0	URIPOTI WA VYOMBO VYA HABARI VYA KIMATAIFA KUHUSU MATUKIO YA BAADA YA UCHAGUZI	43
7.0	WANANCHI KAMA WASHIRIKI HAI: TATHMINI YA USHIRIKI WA WANANCHI MITANDAONI	44
8.0	TATHMINI NA MAPENDEKEZO	45
	Kiambatisho	46-47

SHUKRANI

Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano kwa Umma ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM-SJMC) inatoa shukrani zake za dhati kwa Ubalozi wa Uswisi na Ubalozi wa Uingereza nchini Tanzania kwa msaada wao wa kifedha uliofanikisha utafiti huu na kwa dhamira yao ya dhati ya kuboresha ubora wa vyombo vya habari na uandishi wa habari nchini. Ripoti hii ni ya pili baada ya ripoti iliyochapishwa mwaka 2020 ambayo ilijikita kwenye uripoti wa vyombo vya habari kwenye Uchaguzi Mkuu nchini Tanzania. Kimsingi ripoti ya kwanza ilifadhiliwa na Ubalozi wa Uswisi kama sehemu ya mradi wa utafiti wa Yearbook kuhusu Ubora wa Uripoti wa Vyombo vya Habari Nchini Tanzania (2021-2024).

Tunazielekeza shukrani zetu kwa wanahabari kutoka vyombo mbalimbali vya habari kwa mchango wao ambao umechangia pakubwa kwenye masuala ya weledi kitaaluma kwa vyombo vya habari hapa nchini. Tunawashukuru kwa dhati wale ambao walitenga muda wao kushiriki kwenye mahojiano na kushiriki kwenye majadiliano ya wazi. Shukrani za dhati pia ziwaendee wataalamu wetu walioipitia kazi hii: Prof. Michael Andindilile kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na Dkt. George Gathigi kutoka Chuo Kikuu cha Nairobi (UoN), Idara ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano kwa Umma, kwa maoni na mchango wao wenye thamani kubwa.

Vile vile tunawiwa kuwashukuru watafiti wasaidizi kwa kujitoa kwao wakati wote wa utafiti huu: Swaum Manengelo, Faidha Ngaga, Safina Yasini, Theodora Munisi, Caroline Malewo, Esther Kasanga, Teddy Mparanyanga, Emmanuel Ngabo, Hafidhu Linguya, Jacksoni Gilberth and Ramadhani Fupi. Wengine ni pamoja na Aisha Makame, Theodora Theodory, Pascael George, Shadida Salum, Salma Tanzilu, and Lineth Renatus.

MATOKEO YA UTAFITI KWA MUHTASARI

Utafiti huu ulichunguza uripoti wa vyombo vya habari katika Uchaguzi Mkuu wa 2025 kwa kutumia sampuli ya vipengele vya habari 2,017 (habari, makala, taarifa za habari, na vipindi) vilivyotolewa kutoka vyombo vya habari 46, vikiwemo vyombo vya utangazaji (1,107), magazeti (461), na vyombo vya habari vya mtandaoni (449) kwa Tanzania Bara na Zanzibar. Aidha, utafiti ulifanya uchambuzi wa maoni ya wananchi mtandaoni kwa kutumia jumla ya maoni 17,202 kutoka machapisho 200 ya vyombo vya habari mtandaoni. Utafiti ulitumia mbinu ya uchambuzi wa maudhui ya kiasi (quantitative content analysis) kwa kuzingatia viashiria maalum vya ubora wa uandishi wa habari, vilivyojaribiwa mwaka 2019 wakati wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na kutumika kwa mara ya kwanza katika Uchaguzi Mkuu wa 2020.

Matokeo Makuu

Yafuatayo ni matokeo muhimu yaliyopatikana katika utafiti huu

1. *Uripoti mdogo wa utekelezekaji wa ahadi za wagombea urais.* Vyombo vya habari vilivyofanyiwa utafiti vilijadili kwa nadra uwezekano huo wakati wa uchaguzi, ambapo ni asilimia 14 tu ya uripoti kuhusu uchaguzi wa urais wa Muungano uliogusia utekelezekaji wa ahadi za wagombea. Kwa kuzingatia nafasi muhimu ya vyombo vya habari wakati wa uchaguzi, ukosefu huu wa uchambuzi wa suala hili muhimu kwa wapiga kura, unapaswa kuangaliwa kwa kina, kwani unawanyima wapiga kura fursa ya kufanya maamuzi sahihi. Vyombo vya habari vinapaswa kuchambua kwa kina ahadi za wagombea ili kuwasaidia wapiga kura kufanya maamuzi sahihi wakati wa uchaguzi.

2. *Ukosefu wa uwakilishi wa sauti za wananchi:* Uripoti wa uchaguzi mkuu ulionyesha upungufu mkubwa katika kuwakilisha sauti za wananchi, ambazo mara nyingi zilitengwa. Uripoti wa vyombo vya habari ulipendelea sauti za wagombea, hali iliyosababisha pengo katika uwakilishi wa wapiga kura. Ni asilimia 11 tu ya vyombo vya habari vilivyowajumuisha wananchi kama vyanzo vya habari, huku vyombo vya habari vinavyomilikiwa na serikali vikionesha uwakilishi mdogo zaidi wa asilimia 12.1 ikilinganishwa na asilimia 87.9 kwa vyombo vya habari vya binafsi. Katika makundi ya vyombo vya habari, vyombo vya utangazaji vilionyesha kiwango cha juu zaidi cha kujumuisha sauti za wananchi (asilimia 70.85) katika uchaguzi ikilinganishwa na vyombo vya habari vya mtandaoni na magazeti, vilivyorekodi asilimia 17.5 na 11.7 mtawalia. Redio ya CG FM ilijitokeza kuwa kinara katika kujumuisha sauti za wananchi, ikifuatiwa na ITV, Star TV, na Pemba Today.

3.*Ujumuishaji wa sauti za wanawake bado ni changamoto:* Utendaji wa jumla kuhusu matumizi ya vyanzo vya wanawake katika vyombo vya habari umeimarika kidogo ikilinganishwa na Uchaguzi Mkuu wa 2020. Mwaka 2020, vyanzo vya wanawake vilichangia asilimia 20 ya maudhui ya vyombo vya habari yaliyofanyiwa tathmini, huku katika uchaguzi wa 2025 idadi hii ikiongezeka hadi asilimia 38. Hata hivyo, asilimia 61.8 ya vyombo vya habari bado havijumuishi sauti zozote za wanawake. Kwa ujumla, vyombo vya habari na waandishi wa habari huonyesha mwenendo unaofanana katika kushughulikia vyanzo vya wanawake, huku tofauti kati ya vyombo vya habari vya magazeti, utangazaji na mtandaoni zikiwa karibu kutokuwepo kabisa.

4. *Umakini mkubwa zaidi kwa mgombea aliyeko madarakani:* Rais aliyeko madarakani na mgombea wa CCM, Samia Suluhu Hassan, alipata uangalizi mkubwa zaidi wa vyombo vya habari miongoni mwa wagombea wote wa nafasi ya urais wa Muungano, akipata asilimia 56.2 za uripoti wote, huku wagombea wengine 16 wa urais wakigawana kwa pamoja asilimia 43.17 iliyobaki. Kwa mtazamo wa kijinsia, mbali na Samia Suluhu Hassan, wagombea wengine wa kike wa urais—Saum Hussein Rashid (UDP) na Mwajuma Noty Mirambo (UMD)—hawakupewa uzito mkubwa na vyombo vya habari, kwani waliripotiwa kwa asilimia 4 tu kwenye uchaguzi mkuu huo.

5. *Uripoti wenye uwiano Zanzibar:* Kwa upande mwingine, Zanzibar ilishuhudia ushindani hai na wenye ushindani halisi kati ya vyama viwili vikuu na wagombea wao. Uripoti wa vyombo vya habari kwa mgombea urais kupitia CCM, Dkt. Hussein Ali Mwinyi, na mgombea wa ACT-Wazalendo, Othman Masoud Othman, ulikuwa kwa kiasi kikubwa na uwiano. Othman alipata asilimia 39.2 ya uripoti, ilhali Mwinyi—Rais wa Zanzibar aliyeko madarakani—akipata asilimia 38.8, ikiwa ni tofauti ndogo. Wagombea wengine waliosalia, kwa Pamoja, wakipata asilimia 23.5 ya uripoti wa vyombo vya habari. Kwa upande wa mgawanyo wa majukwaa, Mwinyi alipata uripoti mkubwa zaidi katika vyombo vya habari vya uchapishaji (asilimia 40.6) ikilinganishwa na Othman Masoud Othman aliyepata asilimia 28.1. Kinyume chake, Othman Masoud Othman alipata asilimia 32.7 ya uripoti katika vyombo vya habari vya mtandaoni, huku Mwinyi akipata asilimia 22.64 tu.

6. *Chama tawala kilipata uripoti mkubwa zaidi*: Mwelekeo kama huo, ambapo vyombo vya habari vilitoa kipaumbele kikubwa kwa chama tawala cha CCM, ulijitokeza pia katika chaguzi nyingine, zikiwemo uchaguzi wa wabunge wa Muungano (Bunge), Baraza la Wawakilishi la Zanzibar (ZHoR), na Serikali za Mitaa (udiwani). Katika uchaguzi wa Bunge, uripoti wa CCM ulikuwa asilimia 56; ZHoR asilimia 70.4; na udiwani asilimia 71. Kama ilivyokuwa katika chaguzi zilizopita, vyombo vya habari vya serikali viliripoti zaidi wagombea wa CCM kuliko wale wa vyama vya upinzani. Vyombo vilivyoripoti zaidi kuhusu Samia Suluhu Hassan ni Habari Leo na TBC Taifa, kila kimoja kikiwa na asilimia 5.8% ya marejeleo yote, vikifuatiwa kwa karibu na Fullshangwe Blog (asilimia 5.5), *Green Waves Media* (asilimia 4.7), *Global TV Online* (asilimia 4.2), na *Daily News* (asilimia 4). Katika uchaguzi wa urais Zanzibar, *Zanzibar Leo na ZBC Redio* ziliongoza katika uripoti wa kampeni za Mwinyi kwa asilimia 9.4 na 7.6 mtawalia

7. *Ilani za vyama zilipata uripoti mkubwa*: Hali ya kurejelea ilani za vyama ilionekana katika idadi kubwa ya taarifa zilizowahusu wagombea. Kwa ujumla, katika wagombea watano wa nafasi urais, uripoti wa vyombo vya habari ulihusisha kwa kiwango kikubwa ilani za vyama vyao husika. Uripoti uliomhusu Samia ulijumuisha urejelezi wa ilani ya uchaguzi ya chama chake kwa asilimia 67.9, ilihali, Salum Mwalimu, Gombo, Kunje, na Doyo wakipata asilimia za juu kidogo kwa asilimia71 hadi 79.3. Kunje alichomoza juu zaidi kwa kupata asilimia79.3 ikiwa ndiyo kiwango cha juu zaidi kwa wagombea wa upinzani.

8. *Haiba dhidi ya sera*. Kuhusu uripoti wa uchaguzi unaolinganisha sera na haiba, matokeo yanaonesha kuwa haiba za wagombea zilikuwa na mchango mdogo katika Uchaguzi Mkuu wa 2025. Vyombo vya habari kwa kiasi kikubwa vilijikita katika sera za wagombea, jambo ambalo ni alama ya uripoti bora wa uchaguzi kwani linawawezesha wapiga kura kuzielewa na hivyo kufanya maamuzi sahihi ya kupiga kura.

Sababu zinazoathiri ubora wa uandishi wa habari za uchaguzi

Kuna sababu tatu zinazofafanua ubora wa uandishi wa habari ulioelezwa hapo juu.

1.Kwanza, mazingira ya vyombo vya habari kabla ya uchaguzi na wakati wa kampeni yaliminya uhuru wa vyombo vya habari nchini. Kufungiwa kwa baadhi ya vyombo vya habari kufanya shughuli zake kulichochea kujidhibiti (self-censorship) miongoni mwa waandishi wa habari na wahariri.

2.Sababu ya pili, inahusu mazingira ya kiuchumi ya vyombo vya habari. Kwa ujumla, vyombo vya habari nchini vinakabiliwa na changamoto za kifedha, vingi vikiwa katika hali ya kusuasua, hasa kutokana na kushuka kwa kiasi kikubwa kwa mapato yanayotokana na matangazo, madeni yasiyolipwa, na kuvurugika kwa mifumo iliyozoeleka ya kibiashara. Kutokana na hali hiyo, vyombo vingi vya habari vilikosa rasilimali za kutosha kufanikisha uripoti wa uchaguzi kwa ufanisi. Kadri vyombo vya habari vingi vilivyokuwa vikihangaika kuendelea kuwepo na kufanya kazi, ndivyo ilivyokuwa vigumu zaidi kuwa na uripoti huru wa uchaguzi bila kutegemea msaada usio wazi kutoka kwa vyama vya siasa au wagombea.

3.Changamoto ya tatu inahusu taaluma na upungufu wa waandishi wa habari wenye uzoefu na wenye rekodi nzuri katika uandishi wa habari za uchaguzi. Vyombo vya habari vinakosa waandishi wenye uzoefu wa kina katika kuripoti uchaguzi. Ni nadra sana leo hii kumkuta mwandishi wa habari aliyeripoti chaguzi nne zilizopita akiwa kwenye vyombo vya habari. Ukosefu huu wa waandishi wenye uzoefu mkubwa katika kuripoti uchaguzi, pamoja na upungufu wa umahiri muhimu katika aina hii maalum ya uandishi wa habari, unatatiza uwezo wa vyombo vya habari kuripoti na kuchambua masuala muhimu na kuyafikisha kwa hadhira kwa ufanisi.m to the audience's attention.

Mapendekezo

1) Utafiti huu unatoa mapendekezo yafuatayo.

Uwezekano wa utekelezekaji wa ahadi za wagombea: Andaa mafunzo ya uandishi wa habari ili kushughulikia mapungufu yaliyobainishwa kwenye utafiti huu, hususan hitaji la kutathmini uwezekano wa utekelezekaji wa ahadi za wagombea. Jukumu hili limeonekana kuwa changamoto kubwa kwa waandishi wa habari. Mashirika ya vyombo vya habari na wadau wengine wanapaswa kushirikiana na wataalamu wa uhakiki wa taarifa (fact-checkers) ili kuthibitisha kwa uhuru madai na ahadi za wagombea. Ushirikiano huu unaweza kuimarisha mbinu ya kina na makini katika uandishi wa habari.

2) Kuboresha uwakilishi wa sauti za wananchi: Vyombo vya habari, hususan redio zenye leseni za wilaya na zile za jamii, kwa kushirikiana na mashirika yenye mtazamo unaofanana, vinapaswa kuanzisha mipango ya uandishi wa habari za kijamii pamoja na vipindi maalum vinavyohamasisha uandishi wa habari wa wananchi (citizen journalism), ili kuwawezesha wanajamii kuripoti masuala ya maeneo yao na kushiriki katika mchakato wa uchaguzi. Hii inaweza kusaidia kuwa na sauti za aina tofauti tofauti kwenye uripoti wa vyombo vya habari. Aidha, wanapaswa kuandaa majukwaa yatakayowawezesha wananchi kushirikiana moja kwa moja na wagombea na kueleza changamoto zao, huku mijadala hiyo ikihakikishwa kuripotiwa na vyombo vya habari.

3) Kutoa nafasi zaidi kwa wagombea wasiopewa kipaumbele cha kutosha:Vyombo vya habari vinaweza kuanzisha majukwaa maalum yatayowaangazia wagombea wasiojulikana sana, ambao wengi wao ni vijana na wanawake, ili kuwapa fursa ya kukutana na wapiga kura wao na kunadi sera zao. Vilevile, vinapaswa kujitahidi kuhakikisha uwakilishi wa haki na usawa, hususan kwa vijana, wanawake, na wagombea wa makundi maalumu.

4) Uwezo wa kifedha wa vyombo vya habari: Kutokana na changamoto zinazovikabili vyombo vya habari katika uendeshaji wake, vinapaswa kuendelea kutafuta vyanzo mbadala vya mapato ili kupanua na kuimarisha mapato yao. Katika juhudi hizi, ushirikiano kati ya vyombo vya habari, pamoja na ushirikiano kati ya vyombo hivyo na mashirika yenye mtazamo unaofanana, ni wa muhimu sana. Kwa hiyo, Serikali na washirika wa maendeleo wanapaswa kuzingatia kutoa ruzuku kwa redio za jamii ili kuimarisha uandishi wa habari wakati wa uchaguzi.

5) Kuimarisha uhuru wa vyombo vya habari: Vyombo vya habari na waandishi wa habari wanapaswa kushirikiana na asasi za kiraia katika kutetea sera na miongozo ya kisheria inayolinda uhuru wa vyombo vya habari. Hatua hii inaweza kujumuisha kushinikiza uwepo wa sheria zinazozuia udhibiti wa maudhui (censorship) na kuhamasisha uwazi katika uendeshaji wa vyombo vya habari.

6) Kuimarisha utendaji wa vyombo vya habari vya serikali: mamlaka za usimamizi wa vyombo vya habari zinapaswa kuvisimamia vyombo hivi kama zinavyosimamia vyombo vingine. Usimamizi wa aina hii ni wa muhimu ili kuhakikisha kwamba vyombo vya habari vya serikali vinatimiza wajibu wao wa kisheria na kitaaluma wakati wa uchaguzi wa uchaguzi kwa kuwa na uripoti wenye haki na usawa kwa wagombea na vyama vyote vinavyoshiriki uchaguzi.

Kuhusu Mradi wa Ubora wa Maudhui ya Vyombo vya Habari Tanzania

Mradi huu wa Ubora wa Maudhui ya Vyombo vya Habari Tanzania ni mpango wa kina wa kila mwaka unaotafiti hali ya vyombo vya habari na uandishi wa habari nchini Tanzania kwa lengo la kuhamasisha uandishi wa habari wenye ubora. Mradi huu unaangazia masuala muhimu kama hali ya uripoti wa habari, uhuru wa vyombo vya habari, na mazingira ya kibiashara ya sekta ya habari. Tafiti zinazofanyika chini ya mradi huu zinatumia mbinu za uchambuzi wa maudhui (quantitative content analysis) wa vyombo vya habari vya uchapishaji, utangazaji, na vyombo vya habari vya mtandaoni. Pamoja na uchambuzi wa maudhui, ukusanyaji wa maoni na mitazamo ya wadau hufanyika ili kusaidia kutafsiri matokeo ya takwimu zilizokusanywa. Mradi huu unajengwa juu ya nguzo tatu kuu: Mafunzo, Utafiti, na Usambazaji wa Matokeo kwa wadau mbalimbali.

Tangu kuzinduliwa kwa ripoti yake ya kwanza mwaka 2018, kufuatia tafiti ya majaribio ya mwaka 2017, mradi huu umechapisha ripoti tano kamili za utafiti mwaka 2018, 2019, 2020, 2022 na 2024, huku ripoti hii ikiwa ya sita. Ripoti hizi za kitafiti zimetumika na kunukuliwa kwa kiasi kikubwa katika machapisho ya kimataifa.

Kutokana na mradi huu, makala mbili za kitaaluma: *"The quality of radio journalism in Tanzania: Empowering citizens or at a crossroads?"* na *"Exploring a Practice-Oriented Methodology for Measuring News Media Quality in Tanzania"* zimechapishwa kwenye majarida ya SAGE na Routledge. Aidha, mradi huu ulishinda tuzo ya utafiti bora ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) katika wiki ya utafiti kwenye kundi la miradi inayoshirikisha jamii mwaka 2023.

Mradi huu umefaidika na msaada mkubwa wa kifedha kutoka Ubalozi wa Uswisi nchini Tanzania, pamoja na msaada wa ziada kutoka Ubalozi wa Uingereza na Uholanzi.

UBORA WA MAUDHUI YA VYOMBO VYA HABARI TANZANIA















1.0 UTANGULIZI

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (JMT) ilifanya uchaguzi wake mkuu wa saba uliohusisha vyama vingi vya siasa mwezi Oktoba 2025. Baada ya uliberali wa kisiasa na kurejeshwa kwa mfumo wa vyama vingi mwaka 1992, uchaguzi mkuu wa kwanza wenye ushindani ulifanyika mwaka 1995, ukifuatiwa na chaguzi za mwaka 2000, 2005, 2010, 2015, 2020, na 2025. Katika chaguzi zote hizi, vyombo vya habari vimekuwa vikitekeleza jukumu muhimu katika kuziripoti, ingawa kwa viwango tofauti vya uripoti.

Utafiti huu unachunguza utendaji wa vyombo vya habari kwenye uchaguzi wa mwaka 2025 pamoja na kutathmini namna vilivyofanikiwa kugusa maslahi ya umma. Hii ni ripoti ya pili katika mfuatano baada ya ile ya kwanza iliyotoka mwaka 2020 ikiwa ni sehemu ya mradi wa utafiti wa 'YearBook' kuhusu ubora wa uripoti wa vyombo vya habari nchini Tanzania.[1] Utafiti huu ulilenga kubaini ni kwa namna gani vyombo vya habari vilizingatia utamaduni wa uripoti wa uchaguzi, kuzifanya sauti za wananchi kusikika zaidi na hatimaye kuchangia kwenye uripoti wa kidemokrasia na kiuwajibikaji.

Uchambuzi ulijumuisha uripoti uliofanyika kwenye vyombo vya habari 47 vikiwamo magazeti 10, vyombo 23 wa utangazaji, na vyombo 14 vya mtandaoni. Utafiti ulijielekeza zaidi kuchunguza maeneo matano ya uchaguzi: uchaguzi wa rais wa Muungano, uchaguzi wa rais wa Zanzibar, uchaguzi wa wabunge, uchaguzi wa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na uchaguzi wa madiwani. Zaidi ya hapo, utafiti ulichunguza uripoti wa vyombo vya habari vya kimataifa baada ya uchaguzi wa Oktoba 29 na maoni ya wananchi mitandaoni wakati wa kipindi chote cha uchaguzi.

Utafiti umetumia kiunzi cha uchambuzi wa maudhui kitakwimu (quantitative content analysis) kutathmini uripoti wa vyombo vya habari kwenye uchaguzi wa mwaka 2025 ukitumia viashiria mbalimbali vya ubora wa kiuandishi wa habari. Viashiria hivi vinajumuisha urejeleaji wa ilani za uchaguzi za vyama, uripoti kuhusu uhalisia wa ahadi za wagombea na utekelezekaji wake, ulinganifu katika uripoti wa masuala ya kisera dhidi ya masuala binafsi ya wagombea, uwekaji kipaumbele na mahali zinapowekwa habari zinazohusu uchaguzi, muktadha wa uripoti, vyanzo vya habari vilivyotumika na uripoti wa wagombea wanawake. Ili kuboresha uchambuzi, tulifanya mahojiano na watoa taarifa wakuu wakiwakilisha wadau wa aina mbalimbali. Hawa walijumuisha wataalamu wabobezi wa masuala ya habari kama vile wahariri na mameneja wa stesheni mbalimbali, wawakilishi kutoka taasisi za habari na wadhibiti wa kisekta, wanachama wa vyama vya siasa, watu wenye ulemavu, waandishi wa habari waandamizi na wastaafu, na wawakilishi kutoka kwenye taasisi za kiraia za kitaifa zilizokuwa zimeteuliwa. Mahojiano haya yalilenga kupata ufahamu wa kina wa namna vyombo vya habari vinavyofanya mchakato wake wa uchujaji taarifa, vinavyotengeneza agenda na dhima zake kwenye uchaguzi mkuu.

Utafiti umegawanyika katika sehemu nane: Utangulizi, Usuli, Methodolojia, Matokeo ya Utafiti (kitakwimu na kimaelezo), Mtazamo wa Wadau, Uripoti wa Vyombo vya Habari vya Kimataifa, Maoni ya Mitandaoni, Hitimisho na Mapendekezo. Ripoti hii inapatikana kwenye tovuti ya UDSM-SJMC (https://www.udsm.ac.tz/web/index.php/schools/sjmc), kupitia menyu ya the Yearbook on Media Quality in Tanzania.

[1] Monitoring the Watchdog: How the media covered the 2020 elections, https://sjmc.udsm.ac.tz/yearbook/wp content/uploads/2022/01/MEDIA-COVERAGE-OF-ELECTION-IN-TANZANIA-20201.pdf

2.0 USULI

2.1.1 Hali ya Vyombo vya Habari na Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025

Sekta ya vyombo vya habari nchini imekuwa ikiimarika tangu chapisho la mwisho kuhusu uripoti wa vyombo vya habari kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 lilipotoka. Mwezi Desemba mwaka 2020, kulikuwa na stesheni 243 za redio na televisheni (TCRA, 2020)[2] Hadi kufikia mwezi Desemba mwaka 2025,[3] idadi hiyo imeongezeka kwa kasi zaidi hadi kuwa na watoa huduma ya utangazaji 331 kama inavyoonekana kwenye jedwali lifuatalo hapa chini:

Leseni za watoa huduma za utangazaji kama ilivyokuwa mwezi Desemba 2025

Na	Aina	Desemba 2025
1	Leseni za maudhui ya Televisheni kitaifa	21
2	Leseni za maudhui ya Televisheni kiwilaya (FTA)	21
3	Leseni za maudhui ya Redio kitaifa	14
4	Leseni za maudhui ya Redio kimkoa	37
5	Leseni za maudhui ya Redio kiwilaya	188
6	Redio za Kijamii	19
7	Maudhui ya Kitaifa ya Televisheni kwa kulipia	30
8	Maudhui ya Kiwilaya ya Televisheni kwa kulipia	1
9	Maudhui ya Kitaifa (huduma saidizi)	3
10	Wakusanya Maudhui ya Mtandaoni	6
11	Blogu	77
12	Redio za Mtandaoni	13
13	Televisheni za Mtandaoni	222
14	Televisheni za kebo (Cable Televisions)	55
	Jumla ya leseni za utangazaji	**707**

Chanzo: Ripoti za Takwimu za Sekta ya Mawasiliano (Desemba 2025)

Desemba 2020
243
Vituo vya redio na televisheni

Desemba 2025
331
Vituo vya redio na televisheni

Wakati uchaguzi ulipoanza kule Zanzibar, kulikuwa na stesheni za redio 32 zilizokuwa na leseni, stesheni 10 za televisheni na watoa huduma za maudhui mtandaoni walikuwa 60,[4] huku ikishuhudiwa vyombo vya habari vya mtandaoni vikikua kama ilivyo Tanzania Bara.
Kwa vyombo vya habari vya uchapishaji[5] (magazeti), data kutoka Idara ya Habari-Maelezo[6] zinaonyesha kwamba, kabla ya kuanza kwa kampeni za uchaguzi

[2] TCRA (2020). Quarterly Communications Statistics October - December 2020
[3] Statistics, https://www.tcra.go.tz/services/statistics
[4] Official data from the Zanzibar Broadcasting Commission (ZBC), 2025
[5] Official data from Maelezo, 2025
[6] This includes newspapers and magazines

mkuu mwezi Agosti 2025, kulikuwa na magazeti 183 yaliyokuwa yamesajiliwa. Jumla ya magazeti 16 yalikuwa ya kila siku na 36 ya kila wiki ambapo magazeti 19 miongoni mwayo yalikuwa yamesajiliwa mwaka mmoja tu kabla kampeni hazijaanza. Kwa Zanzibar, sekta ya vyombo vya habari vya uchapishaji haijaendelea sana huku magazeti mengi yakimilikiwa na kampuni ya magazeti ya serikali. Jedwali lifuatalo linaonyesha mchanganuo wa magazeti yenye leseni/yaliyosajiliwa Tanzania Bara na Zanzibar pamoja na idadi ya waandishi wa habari waliopo kazini:

Idadi ya aina za vyombo vya habari vyenye leseni na waandishi wa habari kama ilivyokuwa mwezi Desemba, 2025

	Stesheni za Redio	Stesheni za TV	Vyombo vya habari vya mtandaoni	Magazeti	Waandishi wa habari
Tanzania Bara	258	73	301	183	3,379
Zanzibar	32	10	60	DNA	DNA

Chanzo: TCRA, Maelezo (Tanzania Bara), JAB, na ZBC (Zanzibar), DNA = data hazikupatikana.

Licha ya ukuaji usiokuwa na kifani wa vyombo vya habari asilia – magazeti, redio, televisheni na vile vya mtandaoni – nchi pia ilishuhudia maendeleo makubwa katika matumizi ya intaneti. Kwa miaka mitano iliyopita, idadi ya watumiaji wa intaneti imeongezeka kwa zaidi ya mara mbili kutoka watumiaji milioni 28.4 mwezi Desemba mwaka 2020 hadi kufikia watumiaji milioni 58.1 mwezi Desemba mwaka 2025, huku matumizi ya intaneti jongefu isiyotumia waya yakiongezeka zaidi na kufikia asilimia 99 ya watumiaji wote.[7] Kutanda kwa matumizi ya intaneti hakupo maeneo ya mijini tu; bali pia yamefika maeneo ya vijijini. Maendeleo haya yamewezesha wananchi kupata habari sambamba na kushiriki mijadala ya umma mitandaoni ikiwamo ile ya wakati wa uchaguzi mkuu wa mwaka 2025 kama ambavyo itafafanuliwa zaidi kwenye sehemu ya sita ya ripoti hii (maoni ya wananchi mitandaoni).

2015–2020: Udhibiti wa vyombo vya habari nchini Tanzania

Uhuru wa vyombo vya habari ni nguzo muhimu ya demokrasia na uchaguzi. Wakati uhuru wa vyombo vya habari unatishiwa, demokrasia na mchakato wa uchaguzi huathirika vibaya. Ili kuelewa mazingira ya vyombo vya habari katika Uchaguzi Mkuu wa 2025, ni muhimu kuchunguza maendeleo ya muongo uliopita ili kutoa ufahamu muhimu kuhusu hali ya sasa ya vyombo vya habari nchini. Utawala wa Rais John Magufuli (2015–2021) ulitawaliwa na marufuku za vyombo vya habari, kusimamishwa kwa shughuli zake, na kufutwa kwa leseni, pamoja na kuporomoka kwa kiwango cha uhuru wa vyombo vya habari. Mwaka 2016, gazeti la *Mseto* lilipigwa marufuku kwa miaka mitatu; mwaka 2017, *Tanzania Daima* kwa siku 90, *Raia Mwema* kwa miezi mitatu, *Mawio* kwa miaka miwili, Mwanahalisi kwa miaka miwili, na *The Citizen* kwa siku saba (7). Mwaka 2020, Serikali ilifuta leseni ya uchapishaji ya Tanzania Daima, gazeti lililoonekana kuwa na mrengo wa upinzani, ambalo hapo awali lilikuwa limepigwa marufuku kwa siku 90 mwaka 2017, ikitaja ukiukwaji wa mara kwa mara wa sheria za nchi na maadili ya uandishi wa habari kama sababu za kufutwa kwa leseni hiyo.[8]

Katika mwaka huo huo, 2020, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), ambayo ni mdhibiti wa vyombo vya utangazaji nchini, ilisimamisha utangazaji wa *Clouds Television* na *Clouds Entertainment FM Radio* kwa muda wa wiki moja kuanzia tarehe 28 Agosti hadi 3 Septemba 2020. Katika taarifa yake, TCRA ilibainisha kuwa vyombo hivyo viwili vya habari vya kielektroniki vilikiuka Kifungu cha 16 (1) na (2) cha Kanuni za Huduma za Utangazaji (Maudhui) (Matangazo ya Uchaguzi ya Vyama vya Siasa), 2015, ambacho kwa sehemu kinawataka watoa huduma za maudhui kusambaza/kurusha matokeo ya uchaguzi kama yanavyotolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).

[7] TCRA (2025). Communications statistics report quarter ending December 2025

[8] Katunzi, A., Spurk, C. (2021). Monitoring the Watchdog: How the media covered the 2020 elections in Tanzania, Dar es Salaam: University of Dar es Salaam' School of Journalism and Mass Communication (UDSM-SJMC).

Hivyo basi, *Clouds Media* ilizuiwa kurusha mapema matokeo ya uchaguzi ambayo NEC haikuwa imetangaza rasmi. Cha kushangaza, baadaye NEC ilitangaza matokeo hayo hayo.

Mazingira haya ya uhuru wa vyombo vya habari yalipata ukosoaji. Ripoti ya The Reporters Without Borders Press Freedom Index ilionyesha kushuka kwa uhuru wa vyombo vya habari kati ya mwaka 2016 na 2020. Kwa mwaka 2016, Tanzania ilishika nafasi ya 71 (kati ya nchi 180), mwaka 2017 ilishika nafasi ya 83, 2018 nafasi ya 93, 2019 nafasi ya 118; na mwaka 2020 ilishika nafasi ya 124 ikiwa ni anguko la nafasi 53 ndani ya miaka mitano. Hili lilikuwa ni anguko kubwa kuwahi kushuhudiwa nchini. Katika kipindi hicho, mazingira ya vyombo vya habari yalizungukwa na udhibiti binafsi (self-censorship). Matokeo ya utafiti wa Yearbook wa mwaka 2019 yanabainisha kwamba umma, waandishi wa habari, na wataalamu wabobezi, walikuwa wakihofia kutoa maoni yao kwa uwazi hasa maoni yaliyokuwa yakiikosoa serikali. Mwaka mmoja nyuma, ripoti ya utafiti wa Yearbook wa mwaka 2018 ilionyesha kwamba kulikuwa na uripoti mchache kutoka kwenye vyombo vya habari asilia (legacy media) uliowasilisha maoni yaliyokuwa yakiikosoa serikali. Ripoti ya mwaka 2019 ilibainisha hali ile ile, ikionyesha kwamba vyombo vya habari vya uchapishaji vilichapisha asilimia 4 tu ya habari zilizokuwa zikiikosoa serikali.

2021-2025: Tumaini dogo?

Baada ya kifo cha Rais Magufuli tarehe 17 Machi 2021 na kusimikwa madarakani kwa Makamu wake wa Rais, Samia Suluhu Hassan, 19 Machi 2021, tasnia ya habari nchini ilishuhudia mwanga wa matumaini na maendeleo chanya. Palishuhudiwa mapitio ya Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016, kuondolewa kwa amri iliyovizuia vyombo vya habari vya mtandaoni, kuondolewa kwa amri ya lazima ya kuwa na leseni ili kurusha maudhui yale yale kwa wakati mmoja kwenye jukwaa zaidi ya moja (simulcasting); kupunguza ada ya leseni ya mwaka kwa vyombo vya habari vya mtandaoni vinavyotengeneza maudhui ya habari na matukio (kutoka dola za Marekani [9]432 mpaka dola za Marekani 216) mwaka 2022 mapitio ya kanuni za Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta za mwaka 2018 (utangazaji wa maudhui ya Redio na Televisheni), kuondolewa kwa zuio la uchapishaji wa magazeti manne – *Mwanahalisi*, *Mawio*, *Tanzania Daima na Mseto*. Miongoni kwa magazeti hayo manne ambayo yaliondolewa zuio la uchapishaji, ni gazeti la *Mwanahalisi* pekee ndilo lililofanikiwa kurudi sokoni likizalisha nakala ngumu (print) na zile za mtandaoni kwenye tovuti yake.

Taasisi mbalimbali za kimataifa, ikiwamo Shirika la Haki za Binadamu (Amnesty International), CIVICUS, na Taasisi ya Habari Kusini mwa Afrika – tawi la Tanzania (MISA-TAN), na vyombo vya habari nchini viliipongeza hatua hiyo vikiiita ni “hatua chanya” [10] na “hatua nzuri kwenye muelekeo sahihi”.[11]

Licha ya kuwepo kwa maendeleo ya aina fulani, marufuku na kusimamishwa kwa vyombo vya habari kuliendelea bila kupungua. Mwezi Agosti, mwaka 2021, gazeti la Uhuru linalomilikiwa na chama tawala, Chama Cha Mapinduzi (CCM), lilichapisha habari kwenye ukurasa wake wa mbele iliyotokana na mahojiano ya BBC na Rais Samia, ikiwa na kichwa cha habari kilichosomeka “Sina wazo kuwania urais 2025 - Samia.”

Siku hiyo hiyo, serikali ililikemea vikali gazeti hilo, ikiita habari hiyo kuwa ya uongo, na kulisimamisha kwa siku 14. Gerson Msigwa, Mkurugenzi wa Idara ya Habari na Msemaji Mkuu wa Serikali, alifafanua kuwa Samia Suluhu Hassan hakutoa kauli iliyohusishwa naye kuhusu kutokuwa na nia ya kugombea urais mwaka 2025. Aidha, mmiliki wa gazeti hilo, Chama Cha Mapinduzi (CCM), alisimamisha uchapishaji wake kwa siku saba. Timu ya juu ya uhariri ya gazeti hilo pia ilisimamishwa kazi na baadaye kuondolewa katika nafasi zao. Chama kilikuwa kimeunda kamati ya kuchunguza suala hilo, ingawa matokeo ya kamati hiyo hayakuwekwa wazi kwa umma.

[9] In February 2026, the government announced a licence fee of USD 20 for content creators.

[10] Tanzania: Victory for media freedom as ban on four newspapers lifted, https://www.amnesty.org/en/latest/news/2022/02/tanzania-victory-for-media-freedom/

[11] Tanzania: Reversal of Ban on Four Newspapers a step in the right direction, https://www.civicus.org/index.php/media-resources/news/5604-tanzania-reversal-of-ban-on-four-newspapers-a-step-in-the-right-direction


UHURU

Usikose kusoma gazeti la Uhuru Vijijini kila ijumaa

Ukweli Daima

Shaka awaumbua CHADEMA, ACT

>Ni kuhusu upotoshaji dhidi ya kauli ya Rais Samia kwa Mbowe

>Ataka ziheshimu Mahakama, zisitafute umaarufu kwa njia za hila

>Aionya ACT kupotosha ukweli kujiuzulu mbunge mteule Konde

Sina wazo kuwania urais 2025-Samia

>Abainisha uhuru wa kisiasa upo, kinachofanyika ni vurugu za kisiasa

> Asema wananchi hawajakataa tozo za miamala ya simu

SEKRETARIETI YA CHAMA

Makamu wa Pili wa Rais akemea upandishaji holela bei za bidhaa

Mwalimu amuua mkewe kwa kumwekea vidonge katika bia ya Bingwa

Chongolo awataka wananchi kutunza miundombinu


CHAMA CHA MAPINDUZI

Simu +255 26 23 22965
Nukushi : +255 -26- 2322965
Barua pepe: katibumkuu@ccm.or.tz

Ofisi ya makao makuu mtaa wa Kuu S.L.P 50, Dodoma.

TAARIFA KWA UMMA.

Chama cha Mapinduzi kimesikitishwa na upotoshwaji mkubwa uliyofanywa na gazeti la Uhuru toleo Namba 24084 la leo Jumatano tarehe 11 Agosti, 2021.

Gazeti hilo limepotosha sehemu ya mahojiano aliyofanya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na Shirika la Utangazaji la Uingereza BBC ,Ikulu Jijini Dar es Salaam.

Katika habari yake kuu limeandika kichwa cha habari "Sina wazo kuwania urais 2025- Samia" Huu ni upotoshwaji mkubwa na kumlisha maneno Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan hakusema kabisa maneno hayo. Hili ni kosa kubwa linalokwenda kinyume na sera inayoongoza vyombo hivyo, jambo ambalo halitavumiliwa hata kidogo hivyo HATUA KALI za kinidhamu zitachukuliwa dhidi ya wote waliohusika katika uandaaji wake.

Gazeti la Uhuru ndiyo **"Adam na Hawa"** wa magazeti yote hapa nchini, linawajibika kuonesha weledi wa hali ya juu na sio vinginevyo.

Tunawaomba wanachama wa Chama Cha Mapinduzi na watanzania kwa ujumla kupuuza habari hiyo kwani imeandikwa na watu wenye maslahi yao binafsi.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan fikra na nguvu zake kwa sasa zimejikita katika kuwatumikia watanzania na si vinginevyo.

Kidumu Chama Cha Mapinduzi.

Shaka Hamdu Shaka
Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa
Itikadi na Uenezi
11 AGOSTI, 2021

chama cha mapinduzi ccmtanzania @ccm_tanzania www.ccm.or.tz

Mnamo tarehe 5 Septemba 2021, serikali ililisimamisha gazeti la Raia Mwema kwa muda wa mwezi mmoja kwa madai ya kukiuka mara kwa mara sheria za vyombo vya habari na viwango vya taaluma ya uandishi wa habari. Ukiukaji huo ulidaiwa kujumuisha utoaji wa taarifa potofu na uchochezi. Inafahamika kwamba gazeti hili pia liliwahi kufungiwa kwa miezi mitatu mwaka 2017 (tazama hapo juu). Akitoa maoni yake kuhusu kusimamishwa huko, Muthoki Mumo, Mwakilishi wa Kanda ya Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara wa kamati ya kuwalinda waandishi wa habari (Committee to Protect Journalists-CPJ), alibainisha kuwa "ahadi za serikali ya Tanzania za kuboresha hali ya uhuru wa vyombo vya habari nchini zitaendelea kuwa batili ikiwa mamlaka zitaendelea na utaratibu wa kuyaondoa magazeti kwenye mzunguko kwa misingi dhaifu." [12]

Mnamo Oktoba 2024, mwaka mmoja kabla ya Uchaguzi Mkuu wa 2025, mdhibiti wa vyombo vya habari vya utangazaji, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), ilisimamisha leseni za huduma za vyombo vya habari mtandaoni zilizokuwa zimetolewa kwa Mwananchi Communications Limited (MCL), The Citizen, Mwananchi Digital, Mwananchi, na Mwanaspoti kwa muda wa siku 30, baada ya toleo la mtandaoni la The Citizen kuchapisha katuni iliyotafsiriwa kuwa ilikuwa ikimkosoa Rais. Kikatuni hicho kilikuwa kikielezea hali ya kuongezeka kwa matukio ya utekaji nyara na kutoweka kwa watu nchini. Taarifa ya kusimamishwa ilitolewa tarehe 02 Oktoba, 2024 wakati kikatuni husika kilichapishwa tarehe 01 Oktoba 2024. Taarifa hiyo ya kusimamishwa ilirejelea vifungu vya kisheria vilivyokiukwa kuwa ni pamoja na Kanuni ya 16 ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Mtandaoni) za mwaka 2020, ambayo inakataza kuchapisha maudhui yanayohatarisha utulivu wa umma, kudhalilisha au kuharibu sifa, hadhi na heshima ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.[13]

Kufungiwa kwa majukwaa ya mtandaoni ya Mwananchi Communications Limited (MCL) kwa siku 30 kuliibua maswali matatu ya msingi: Kwa nini mdhibiti alifungia leseni za vyombo vyote vinne vya MCL, wakati ni chombo kimoja tu (The Citizen online) ndicho kinachodaiwa kufanya

[12] Tanzanian authorities suspend Raia Mwema newspaper for 1 month, https://cpj.org/2021/09/tanzanian-authorities-suspend-raia-mwema-newspaper-for-1-month/
[13] TCRA (2024). Suspension of the online media services licenses issued to Mwananchi Communications Limited T/A The Citizen, Mwananchi Digital, Mwananchi and Mwanaspoti

ukiukwaji huo wa kikanuni? Kwa nini mdhibiti aliweza kulishughulikia suala hilo kwa haraka kiasi hicho (ndani ya siku moja tu), na kutoa taarifa ya kuvisimamisha? Je, hili halikuwa ni onyo kwa watoa huduma wengine wenye leseni? Kati ya mwaka 2021 na 2025, watoa huduma za habari mitandaoni walielezea hali wanayokumbana nayo wakisema kuwa, wakati fulani mdhibiti alikuwa akiwashinikiza kuondoa baadhi maudhui yao ambayo tayari yalikuwa yameshachapishwa mtandaoni. Mengi ya maudhui hayo, ni yale ambayo mdhibiti aliyaona kama yalikuwa yanaenda kinyume na serikali. Ndani ya miaka hii minne yote, kulikuwa na mahitaji makubwa ya ukimya kuhusu masuala haya yenye athari kisheria.

Siku chache tu baada ya kampeni za uchaguzi wa mwaka 2025 kuanza, tarehe 06 Septemba 2025, TCRA iliifungia leseni ya JamiiForums (Jukwaa la mtandaoni linalowezesha mijadala ya kitaifa nchini) kwa siku 90 kwa kile mdhibiti alichodai, “kuchapisha maudhui yanayopotosha umma, yanayoidhalilisha na kuitweza serikali na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kinyume na Kanuni za Maudhui Mtandaoni za mwaka 2020 pamoja na mabadiliko yake ya mwaka 2022 na 2025”[14]

Likitoa maoni yake kuhusiana na zuio hilo, Shirikisho la Haki za Kupata Taarifa (Coalition on Rights to Information, CoRI) linalojumuisha taasisi 15 ikiwamo JamiiForums, lilitoa tamko kuelezea masikitiko yake na kulaani zuio hilo. Sehemu ya tamko hilo linasomeka hivi: “Uamuzi huu unajumuisha ukiukwaji mkubwa wa haki ya msingi ya kikatiba ya uhuru wa kujieleza na upatikanaji wa taarifa kama ilivyohakikishwa chini ya Ibara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, ambayo inatoa kwamba kila mtu ana haki ya kutafuta, kupokea na kusambaza taarifa.” Kusimamishwa kwa JamiiForums hakuzuii tu haki hizi, bali pia kunadhoofisha misingi ya uwazi, uwajibikaji na majadiliano ya wazi ambayo ni muhimu katika jamii ya kidemokrasia... JamiiForums imekuwa na mchango mkubwa katika kuhamasisha ushiriki wa wananchi, uwazi na uwajibikaji nchini Tanzania. Kusimamishwa kwa shughuli zake kwa siku 90 kunaweka mfano hatarishi na kudhoofisha utawala wa kidemokrasia. CoRI inaamini kwamba haki ya uhuru wa kujieleza na upatikanaji wa taarifa si fursa tu, bali ni nguzo ya msingi ya demokrasia, uwajibikaji na utawala bora” (CoRI, 2025).

Shirikisho liliitaka serikali kuondoa zuio hilo na “kuacha kutumia mamlaka yake ya kisheria kuyanyamazisha au kuyadhibiti majukwaa yanayotekeleza majukumu yake muhimu kwa kutoa nafasi zinazokuza ushiriki wa kiraia, kufichua uovu na kuwezesha upatikanaji wa taarifa zilizothibitishwa”. Wito wa kuitaka serikali kuondoa zuio hilo pia ulitolewa na Kamati ya Kuwalinda Waandishi wa Habari[15] na Kikosi Kazi cha Usimamizi wa Intaneti Tanzania (The Internet Governance Tanzania Working Group IGTWG)[16]

2.1.2 Ithibati kwa waandishi wa habari na miongozo ya uripoti

Mwaka 2016, serikali ilitunga Sheria ya Huduma za Habari ili kuifanya tasnia ya uandishi wa habari kufanyika kitaaluma na kiweledi nchini. Ili kulikamilisha hili, Sheria hii pamoja na Kanuni zake za mwaka 2017, iliweka stashahada ya uandishi wa habari kuwa ndio kiwango cha chini cha mtu anayetaka kufanya kazi ya uandishi wa habari nchini. Aidha, sheria iliunda Bodi ya Ithibati ya Waandishi wa Habari mahsusi kwa ajili ya kutoa ithibati kwa wale wanaokidhi vigezo vya kitaaluma. Mwezi Machi mwaka 2025, Bodi hiyo ilizinduliwa rasmi na Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Prof. Palamagamba Kabudi, ambaye aliielekeza Bodi hiyo kuwasajili waandishi wa habari wote wanaokidhi vigezo na kuhakikisha kwamba waandishi wa habari wenye ithibati wanazingatia weledi na maadili ya taaluma hii. Mpaka kufikia mwezi Novemba mwaka 2025, jumla ya waandishi wa habari 3,379 walikuwa wameshapata ithibati, miongoni mwao wanaume walikuwa 1,871 huku wanawake wakiwa 1,508[17]

[14] TCRA (2025). Kusitishwa kwa muda leseni ya huduma za maudhui mtandaoni iliyotolewa kwa Vapper Tech Limited (JamiiForums)
[15] https://cpj.org/2025/09/tanzanian-authorities-suspend-online-forum-for-90-days-weeks-ahead-of-election/
[16] https://tmc.co.tz/igtwg-statement-on-the-suspension-of-jamii-forums-by-tcra-calls-for-dialogue-and-protection-of-press-freedom/
[17] Official data requested from JAB



Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Prof. Palamagamba Kabudi (kulia) akikabidhi nyaraka muhimu kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Ithibati ya Waandishi wa Habari Ndugu Tido Mhando wakati wa uzinduzi wa Bodi hiyo mwezi Machi mwaka 2025 jijini Dar es Salaam (picha kwa hisani ya Bodi ya Ithibati ya Waandishi wa Habari).

Mwezi Agosti mwaka 2025, Idara ya Habari-Maelezo ilichapisha muongozo maalumu kwa ajili ya uripoti wa masuala ya uchaguzi wenye kichwa cha habari *"Mwongozo kwa vyombo vya habari na waandishi wa habari katika kuripoti Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani wa Mwaka 2025"*.[18] Muongozo unabainisha wajibu wa wadau mbalimbali kama vile Idara ya Habari-Maelezo, Bodi ya Ithibati ya Waandishi wa Habari, vyumba za habari, waandishi wa habari, TCRA, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, na vyama vya siasa. Kwa ujumla, muongozo unahimiza uripoti wa kiuwajibikaji, kuhakikisha kunakuwa na usawa katika uripoti, kuepuka kuchapisha maudhui hasi na hatarishi sambamba na kulinda amani na mshikamano wa taifa. Tofauti na ilivyokuwa kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka 2020, ambapo Tume ya Taifa ya Uchaguzi iliandaa Miongozo ya Matumizi ya Vyombo vya Habari vya Umma na Vyama vya Siasa Wakati wa Kampeni za Uchaguzi wa Mwaka 2020 (Guidelines for the use of public media by political parties during election campaigns, 2020), hakukuwa ma muongozo mwingine wowote wakati huo. Muongozo uliotolewa na Maelezo ulihusu vyombo vyote vya habari, yaani vya umma na vya binafsi.

Muongozo uliunda kamati maalumu kufuatilia uripoti wa uchaguzi mkuu wa mwaka 2025 ikijumuisha wajumbe kutoka Idara ya Habari-Maelezo, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC), Bodi ya Ithibati ya Waandishi wa Habari (JAB); wawakilishi wawili kutoka vyombo vya habari vya umma, wawakilishi wawili kutoka vyombo vya habari vya binafsi, wawakilishi wawili kutoka vyuo vya elimu ya juu vinavyotoa mafunzo ya uandishi wa habari, Wizara ya Mambo ya Ndani, TCRA, Jumuiya ya Wanahabari wa Mitandao ya Kijamii Tanzania (JUMIKITA), Jukwaa la Wahariri (TEF), Shirikisho la Vilabu vya Waandishi wa Habari Tanzania (UTPC) na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA). Mpaka kufikia tarehe 01 Machi, 2026,

[18] http://maelezo.go.tz/storage/app/uploads/public/68a/623/b3a/68a623b3a91fd718446033.pdf

kamati hiyo ilikuwa bado haijatoa ripoti yake.

2.1.3 Waandishi wa habari wanaogombea nafasi za kisiasa

Kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka 2025, kulikuwa na idadi isiyokuwa ya kawaida ya waandishi wa habari waliojitokeza kuomba kuteuliwa na vyama vyao vya siasa ili kugombea nafasi za ubunge na udiwani, hasa kupitia chama tawala, CCM. Kwa mujibu wa Kifungu cha 7(l) cha muongozo uliotolewa na Maelezo, ikiwa mwandishi wa habari kutoka chombo chochote cha habari atajitokeza kugombea nafasi yoyote ya kisiasa na akashindwa, basi hataruhusiwa kurudi tena kwenye nafasi yake kwenye chombo cha habari mpaka uchaguzi utakapokamilika. Hata hivyo, kwa kuwa Maelezo bado hawajatoa ripoti ya ufuatiliaji wake kwenye eneo hili, haifahamiki jambo hili lilisimamiwa kwa uzito kiasi gani.

2.1.4 Mazingira ya kibiashara ya vyombo vya habari

Mazingira ya kibiashara ya vyombo vya habari yametetereka, huku wadau wa vyombo vya habari wakiumiza vichwa kuhusu kuporomoka kwa mapato yatokanayo na matangazo ya biashara. Kushuka kwa mapato yatokanayo na matangazo ya biashara kunahusishwa na mambo mbalimbali mtambuka: mabadiliko ya mfumo wa kibiashara yaliyosababishwa na mabadiliko ya kiteknolojia ambapo inashuhudiwa ongezeko kubwa la bajeti za matangazo zikielekezwa kwenye majukwaa ya mtandaoni; uamuzi wa serikali kupunguza bajeti yake ya matangazo kama namna ya kupunguza matumizi kipindi cha kati ya mwaka 2015 na 2020; kupungua kwa bajeti ya sekta binafsi ya matangazo na kujitangaza; uwekezaji mdogo kwenye sekta ya vyombo vya habari; ukosefu wa mkakati sahihi wa biashara na usimamizi; ukosefu wa wafanyakazi wabunifu; ongezeko la deni linalowakabili watoa matangazo; huku serikali ikiwa ndio mdaiwa mkuu; mifumo ya kodi, vikwazo kwenye sera ya uwekezaji inayoweka ukomo wa umiliki kwa mgeni ambapo kiasi cha juu kabisa ni asilimia 49, uwepo wa vyombo vingi vya habari ambao hauendani na soko (kufeli kwa soko); na ukosefu wa sekta binafsi yenye nguvu.[19]

Haya yote yamesababisha changamoto kwa waandishi wa habari. Kwa kutambua ukubwa wa changamoto za kiuchumi zinazoikabili sekta ya vyombo vya habari nchini, mwaka 2023, serikali iliunda kamati kuchunguza hali ya kiuchumi ya vyombo vya habari na changamoto zilizopo, ambapo ripoti ya kamati hiyo ilizinduliwa na Rais Samia Suluhu Hassan mwaka 2024. Ripoti ilibainisha kwamba asilimia 60 ya waandishi wa habari waliohusishwa kwenye utafiti walikuwa wakilipwa chini ya Sh. 300,000/= kwa mwezi. Kwa ujumla, wengi wa waandishi wa habari ambao ni wawakilishi wanalipwa kwa habari inayokwenda hewani ambapo kwa habari moja wanalipwa kiwango kidogo cha hadi shilinghi 2000/= , yaani chini ya dola moja ya Marekani. Wengi wa waandishi wa habari hawajaajiriwa na wanalipwa kiasi kidogo sana ambacho nacho mara nyingi ukipata kwa kuchelewa. Isipokuwa kwa vyombo vya habari vinavyomilikiwa na serikali na vichache vya watu binafsi, waandishi wengi huishia kutegemea vyanzo vya habari uwandani ili kujipatia chochote cha kujikimu.[20] Nukuu ifuatayo kutoka kwenye ripoti na kutafsiriwa hapa chini inaelezea hali halisi kwa muhtasari:

> “Hali ya kiuchumi ni mbaya zaidi kwa waandishi wa habari wawakilishi ambao wanalipwa kwa habari inayoenda hewani. Mpaka kufikia mwaka 2023, vyombo vya habari vilikuwa vikiwalipa waandishi wawakilishi sh. 2,000/= kwa habari, na bado malipo yalikuwa yakichelewa. Ni jambo la kawaida kwamba, kwa aina hiyo ya malipo, waandishi wengi wa habari hawawezi kujikimu wao wenyewe, na matokeo yake, huwa wanategemea zaidi vyanzo vyao vya habari ili kujipatia chochote cha kujikimu. Hali hii imesababisha baadhi ya waandishi wa habari kutumia maikrofoni zao kujitafutia fedha (kwa kuripoti tukio ili alipwe). Wengine wamekuwa ‘ombaomba’ na wanategemea huruma ya vyanzo vyao vya taarifa kujipatia chochote hali inayokinzana na uhuru wa uhariri na hatimaye kuweza kuingia kwenye mtego wa kuvitumikia vyanzo vya habari vyenye nguvu kifedha” (URT, 2024:11).

Hali huzidi kuwa mbaya zaidi nyakati za uchaguzi ambapo vyama vya siasa huwa ‘vinaajili’ waandishi wa habari ili kutoa habari za upande mmoja na kuwapendelea wao huku wakifanya hivyo kwa kuwapatia malipo fulani. Kwa hali hiyo, waandishi hao hupuuza haki ya wananchi kupata habari sahihi na zisizoegemea upande wowote[21]

Aidha, hali hii ya mazingira yenye changamoto imevilazimisha baadhi ya vyombo vya habari kujipanga upya kwa kupunguza wafanyakazi, kupunguza mishahara, na kufunga ofisi zao za

[19] http://maelezo.go.tz/storage/app/uploads/public/68a/623/b3a/68a623b3a91fd718446033.pdf
[20] URT (2024). Tathmini ya hali ya utendaji na uchumi kwenye vyombo vya habari Tanzania Bara, Ripoti ya Kamati ya Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari
[21] COMPLIANCE ORDER DECISIONS, https://www.tcra.go.tz/pages/public-registe

mikoa. Pia mazingira magumu ya kifedha na yasiyovumilika, yamesababisha baadhi ya vyombo za habari kufunga kabisa biashara hiyo. Mwaka 2019, redio moja ya kijamii yenye makazi yake jijini Mwanza, Lake FM, ilifungiwa na TCRA kufanya kazi zake baada ya kushindwa kulipa malimbikizo ya gharama za kulipia masafa na ada za udhibiti. Mara kwa mara Msimamizi wa huduma za utangazaji amekuwa akitoa amri kadhaa zinazopaswa kutekelezwa[22]kuhusiana na kutokulipa ada ya udhibiti kwa taasisi yoyote yenye leseni ya utangazaji, hali inayoashiria changamoto za kiuchumi zinazoikabili sekta hii ndogo. Mwaka 2020, kampuni ya New Habari 2006 Ltd, wachapishaji wa magazeti ya Mtanzania, Rai, Bingwa, na Dimba ilisitisha shughuli zake ikiyataja mazingira duni ya kibiashara kuwa ndio sababu ya kufanya hivyo.[23]

Ili kuzishughulikia baadhi ya changamoto hizi, vyombo vingi vya habari vimeanza kubuni njia mpya za kujipatia kipato, huku njia maarufu ikiwa ni kuandaa matukio, ubia, shughuli za viwanjani na uandishi wa habari wa ucheshi (comedy journalism). Akifafanua kuhusu mkakati huu mpya wa kujipatia kipato, Katunzi na Ssenabulya (2022) wanabainisha: “Ingawa ubunifu katika kuandaa matukio haya ya kifedha hutofautiana kati ya chombo kimoja cha habari na kingine kulingana na rasilimali za kifedha zilizopo, imeonekana ndio njia mbadala inayopendwa zaidi na vyombo vya habari. Changamoto pekee kuhusu matukio haya ni kwamba, yanatumia muda na rasilimali kujipatia umaarufu. Kwa hiyo, vyombo vya habari vinapaswa kuwa na subira vinapojaribu kuitumia njia hii ili kujipatia fedha”

Hali endelevu ya kifedha ni ya muhimu kwenye sekta ya habari ikiangaliwa kama biashara na kama mhimili wa nne wa serikali. Ikiwa vyombo vya habari vitashindwa kujiendesha katika hali ya uendelevu, matokeo ya hali hiyo huenda mbali zaidi ya vyombo husika vya habari na waandishi wa habari hadi huiathiri jamii kwa ujumla. Bila kuwa na vyombo vya habari endelevu, umma unaweza usipate habari za kuaminika na zinazokidhi viwango vya ubora. Ukata huvidhoofisha vyombo vya habari huku ukivifanya viwe tegemezi na hatimaye kutumiwa na kuendeshwa na wanasiasa na watu wenye ushawishi ambapo baadae huamua namna vyombo hivyo vinavyoripoti habari zake. Ikifika hapo, vyombo vya habari huharibu ubora wa uripoti, hasa katika maeneo muhimu kama vile uripoti wa uchaguzi pamoja na masuala yanayohusu uongozi mbaya na rushwa.

2.1.5 Dhima ya vyombo vya habari kwenye uchaguzi

Kuna seti kuu mbili za dhima za vyombo vya habari kwenye uchaguzi. Seti ya kwanza inaegemea kwenye viwango vya kitaaluma (kiweledi) na uwajibikaji kwa jamii, wakati seti ya pili inaegemea kwenye wajibu wake kisheria. Kwa ujumla, vyombo vya habari vina dhima kubwa ya kuhabarisha, kuelimisha, na kuwawezesha wananchi. Haya yatafikiwa kwa kuwapatia wananchi habari sahihi, inayokuja kwa wakati, iliyojengwa kwenye muktadha wake, ikiwahusu wao, na ikiwa na taarifa zilizofanyiwa utafiti kuhusu mchakato mzima wa uchaguzi.

Hii inahusisha kuhamasisha wananchi kuchukua hatua kwa pamoja na kushiriki kwenye uchaguzi. Hivyo, ili kuwa na uchaguzi huru na wa haki, vyombo vya habari ni nyenzo muhimu na isiyoweza kuepukika. Kwa umahsusi zaidi, vyombo vya habari vina wajibu na dhima ifuatayo kijamii na kitaaluma (kiweledi). Kwa mtazamo wa kitaaluma, vyombo vya habari vina dhima muhimu tatu.

- Vyombo vya habari kama mwalimu wa jamii: vyombo vya habari vina dhima kubwa ya kuelimisha jamii kuhusu mchakato mzima wa uchaguzi. Vinatoa taarifa muhimu ambazo zinawajengea uelewa wapigakura unaowafanya kuwa na maamuzi sahihi na hatimaye kupiga kura kwa busara.
- Vyombo vya habari kama jukwaa la kampeni na majadiliano: chombo cha habari kinafanya kazi kama jukwaa la kampeni na majadiliano, kikitoa nafasi kwa wagombea na wananchi kwa ujumla kuelezea mawazo yao na maoni yao yanayokinzana.
- Vyombo vya habari kama muangalizi wa uwazi: vyombo vya habari vinafanya kazi kama mwangalizi, vikifuatilia kuwafichua wale wote wanaoweza kuharibu mchakato wa uchaguzi, kwa hali hiyo husaidia kuhakikisha kunakuwa na uchaguzi huru na wa haki.
  Usimamizi wa uchaguzi kwenye nchi yetu unaongozwa na miongozo kadhaa ya kisheria ambayo inafanyakazi na washirika wote vikiwamo vyombo vya habari. Mifumo hii ya kisheria inavitaka vyombo

[22] COMPLIANCE ORDER DECISIONS, https://www.tcra.go.tz/pages/public-registe
[23] Kampuni ya New Habari yasitisha uzalishaji, retrieved on 24/9/2021,https://www.mwananchi.co.tz/mw/habari/kitaifa/kampuni-ya-new-habari-yasitisha-uzalishaji--3218412

vya habari kutoa taarifa zisizoegemea upande wowote, sahihi sambamba na zilizoripotiwa kwa usawa kwa vyama vyote vya siasa na wagombea. Matokeo yake, wajibu huu wa kisheria unawakilisha seti ya pili ya wajibu ambao vyombo vya habari vinapaswa kuutimiza nyakati za uchaguzi hapa nchini.

2.2 Mfumo wa kisiasa na Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025: mwenendo wa kihistoria

Uchaguzi mkuu wa mwaka 2025 nchini Tanzania ulihusisha mchakato uliokuwa kwenye ngazi mbalimbali zilizosimamiwa na Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC). Kwa mujibu wa data kutoka INEC, jumla ya wapiga kura 37,647,235 waliokuwa wamejiandikisha walikuwa na uhalali wa kupiga kura kwenye vituo 99,895 vya kupigia kura nchini kote – 97,348 kati ya hivyo vikiwa Tanzania Bara na 2,547 vikiwa Zanzibar[24]

Tangu ulipoanzishwa upya mfumo wa demokrasia ya vyama vingi mwaka 1992, nchi imeendesha chaguzi kuu saba. Kihistoria chaguzi hizi zimeonyesha mwendelezo wa utawala wa CCM sambamba na ujitokezaji wa wapiga kura kwa idadi tofauti tofauti pamoja na ushindani kwenye chaguzi hizo, ambao mwisho wa siku ulimalizika kwa ushindi usio wa kawaida wa CCM kwenye uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025.

Takwimu za uchaguzi wa rais kutoka mwaka 1995 mpaka 2025 zinaonyesha kuwa CCM imekuwa ikitawala matokeo ya chaguzi hizo. Ushindi wa CCM unaviacha mbali vyama vingine tukianzia kwa Benjamin Mkapa mwaka 1995 aliyepata asilimia 61.82, ikaongezeka hadi zaidi ya asilimia71 mwaka 2000 na asilimia 80 mwaka 2005, kabla ya kushuka kwa kiasi kikubwa kwenye utofauti wa asilimia mwaka 2010 (asilimia 62.84) na 2015 (asilimia 58.46), ikionyesha kipindi cha ushindani mkubwa. Mwelekeo huu ukageuka ghafla mwaka 2020 (asilimia 84.40) na kufikia matokeo ya juu kabisa mwaka 2025 (asilimia 97.66). Hali imekuwa ya kipekee huko Zanzibar, ambako vyama viwili vimetawala kwa muda mrefu. Isipokuwa uchaguzi wa urais wa Zanzibar wa 2025, ambapo mgombea wa chama tawala, Dkt. Hussein Ali Mwinyi, alipata asilimia 74.8 ya kura, chaguzi nyingine zilikuwa na ushindani mkali. ACT-Wazalendo, chama kikuu cha upinzani, kilipinga matokeo ya uchaguzi.[25]

2.2.1 Ushiriki wa wanawake kwenye siasa za uchaguzi (1995–2025)

Ushiriki wa wanawake kwenye siasa za uchaguzi nchini Tanzania unaonesha kuongezeka kidogo dhidi ya vizingiti ambavyo vimekuwepo kwa muda mrefu. Tangu uchaguzi wa kwanza wa vyama vingi mwaka 1995, ambapo wanawake walikuwa ni asilimia 4.43% tu za wagombea wa nafasi ya ubunge, jitihada za dhati kuongeza uwakilishi wao zimekuwa ni kupitia mfumo wa viti maalum.[26]
Hatua hii ya ufidiaji kwenye eneo la uwakilishi wa wanawake iliongeza idadi lakini haikuondoa vizingiti kuruhusu uchaguzi wa moja kwa moja. Uchaguzi mkuu wa mwaka 2025 ulikuwa ndio mwanzo mpya ikishuhudiwa idadi isiyotarajiwa ya wanawake waliogombea nafasi ya urais na umakamu wa rais wa muungano. Mabadiliko haya yalisababishwa na ujio wa kihistoria wa Samia Suluhu Hassan kwenye nafasi ya urais mwaka 2021. Uongozi wake ulishawishi wanawake wengi kuingia kwenye siasa, ukitengeneza lugha moja ya kitaifa kuhusu ujumuishi kijinsia.[27] Jambo hili lilitengeneza jukwaa kwenye uchaguzi wa mwaka 2025, ambapo ilishuhudiwa rekodi mpya ya wanawake wengi kugombea nafasi ya urais – rais aliyeko madarakani Samia Suluhu Hassan pamoja na wanawake wengine wawili. Mwanamke wa kwanza kugombea nafasi ya Urais wa muungano ni Anna Senkoro kupitia chama cha PPT-Maendeleo mwaka 2005, akafuatiwa na Anna Mghwira (ACT-Wazalendo) mwaka 2015, na Queen Curthbert Sendiga na Cecilia Augustine Mmanga mwaka 2020.

Vikwazo kwa wanawake wanaogombea nafasi kwenye majimbo ni vikubwa na vyenye sura tofauti tofauti kama ilivyofafanuliwa zaidi kwenye uchambuzi wa Chama cha Wanasheria Wanawake Zanzibar (Zanzibar Female Lawyers Association-ZAFELA).[28] na kwenye ripoti za uangalizi kutoka TAMWA Zanzibar. Kizuizi kikuu ni hali ngumu ya kifedha kuweza kuhimili matumizi ya uchaguzi ikiwamo mipaka ya matumizi ya juu ya fedha za kampeni chini ya Sheria ya Matumizi ya Uchaguzi na kutokuwepo kwa uhusiano wa kifedha na ugombea kwenye Sera ya Uwezeshaji wa Kiuchumi ya Zanzibar.[29]
Wanawake wanaripoti matatizo makubwa katika kupata mikopo ya kifedha na ufadhili, jambo ambalo linawaweka katika mazingira ya kukosa nafasi ikilinganishwa na washindani wao wanaume ambao kwao ni rafiki tangu awali.

24 Independent National Electoral Commission (INEC), "Kuhusu Takwimu za Wapiga Kura na Vituo vya Kupigia Kura Vitakavyotumika Katika Uchaguzi Mkuu wa 2025," October 7, 2025, Instagram post, https://www.instagram.com/p/DPf7UkICCD-/

25 October 7, 2025, Instagram post, https://www.instagram.com/p/DPf7UkICCD-/. ACT Wazalendo rejects 2025 election results, calls for constitutional reforms, https://www.therespondents.co.tz/2026/01/act-wazalendo-rejects-2025-election.html

26 Victoria Lihiru (2023). Why Tanzania celebrates 30 years of multiparty democracy with only 9.8 percent of elected women parliamentarians? A legal explanation. In J. C. Mashamba, A. Henga, V. Lihiru, & J. Ulimwengu (Eds.), Thirty years of multiparty democracy in Tanzania (pp. 129–148). Dar es Salaam, Tanzania: Legal and Human Rights Centre (LHRC).

27 The Citizen, "30 Years After Beijing: Samia focuses on gender equality for Tanzania's youth," March 8, 2025, https://www.thecitizen.co.tz/tanzania/news/national/30-years-after-beijing-samia-focuses-on-gender-equality-for-tanzania-s-youth-4956588

28 Zanzibar Female Lawyers Association (ZAFELA). (2025). Strengthening Women in Leadership: Policy and Legal Gaps.

29 TAMWA Zanzibar et al. (2025). Election Participation Monitoring Report 2025: Women, Youth, and People with Disabilities in Zanzibar.

(2005)



Anna Claudia Senkoro

(2015)



Anna Mghwira

(2020)



Queen Curthbert Sendiga



Cecilia Augustine Mmanga

(2025)



Samia Suluhu Hassan

Vikwazo hivi vya kifedha vinaongezwa na mfumo uliopo wa kisheria na kikanuni ambao kimsingi ni mzuri lakini una mapungufu katika utekelezaji wake. Wakati sheria ya Masuala ya Vyama vya Siasa ya mwaka 2024 (na maboresho yake) ikivilazimisha vyama vya siasa kuwa na Sera za Jinsia na Ujumuishaji wa Kijamii, haiweki adhabu yoyote kwa wanaoikiuka. Hali kadhalika, Sheria ya Kupambana na Rushwa na Uharifu wa Kiuchumi Zanzibar (2023) imeufanya unyanyasaji wa kingono kuwa ni kosa la jinai lakini inakosa taratibu za utekelezaji wake kwa haraka, hasa kwa malalamiko nyeti ya aina hii yanayojitokeza nyakati za uchaguzi. Zaidi ya hayo, kanuni za vyombo vya habari zinazipa mamlaka nguvu za kisheria za kutoa leseni, hali ambayo inaweza kuwa kikwazo kwa majukwaa ya sauti za wanawake katika siasa.

Mwelekeo kutoka mwaka 1995 mpaka mwaka 2025 unaonesha kuwepo kwa mafanikio katika ongezeko la idadi ya wabunge wanawake, hata hivyo bado haijaondoa mifumo inayozuia wanawake wengi kuyafikia mamlaka ya kweli. Kuufikia usawa wa kweli kijinsia kunahitaji kwenda mbali zaidi ya mfumo wa viti maalumu ili kuifanyia mageuzi mifumo yote inayosababisha kutokuwepo kwa usawa: kutekeleza kanuni za uteuzi za vyama, kuweka utaratibu maalumu wa ufadhili wa umma kwa kampeni za wanawake, kuimarisha ulinzi wa kisheria dhidi ya ghasia za kisiasa, na kuanzisha kampeni endelevu za kitamaduni ili kubadilisha mtazamo wa uongozi wa wanawake.

3.0 METHODOLOJIA

Tangu awali, methodolojia iliyotumika kuchunguza uripoti wa vyombo vya habari kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 ilikuwa imeandaliwa mwaka 2019, kisha kufanyiwa majaribio kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka huo huo. Baadaye, methodolojia hiyo ilitekelezwa kikamilifu kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020. Methodolojia hiyo hiyo ikatumika kutathmini uripoti wa vyombo vya habari kwenye uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025. Methodolojia iliyotumika inagusa maeneo mbalimbali ya vigezo vya ubora kuanzia kwenye nadharia ya uandishi wa habari hadi kwenye utendaji wake.

3.1 Vigezo vya ubora

Ripoti za Yearbook hutumia "ubora" kama dhana inayoelezea kwa muhtasari vitu mbalimbali ambavyo kwa ujumla wake ndio huielezea dhana ya vigezo vya ubora. Kimsingi, 'ubora' ukichukuliwa kama kitu kimoja inakuwa haiwezekani kupimika. Badala yake, ubora unaweza ukaangaliwa kama jumla ya mambo kwenye utendaji wa vyombo vya habari kwa msingi wa vigezo halisi vya ubora. Vigezo vya ubora vilivyotumika vimeandaliwa kutokana na nadharia ya uandishi wa habari, utendaji wa vyombo vya Habari, na tafiti za uripoti wa vyombo vya habari nyakati za uchaguzi. Baadhi ya vigezo vya ubora hasa vile vya kitaaluma na kiweledi, vilichukuliwa kutoka kwenye ripoti za Yearbook zilizopita, ambapo vilikubalika miongoni mwa wanatasnia ya vyombo vya habari nchini. Vigezo hivyo ambavyo pia ni faafu kwenye uripoti wa uchaguzi ni:

- Muktadha wa uripoti: kigezo hiki kinaangalia matukio au matamko yaliyosababisha uripoti wa uchaguzi. Pia kinachunguza ikiwa waandishi wa habari wanaenda mbali zaidi ya kuripoti matukio na kukusanya habari zao wenyewe zinazohusu uchaguzi. Kigezo hiki kinasaidia kuweka wazi mambo makuu mawili: mosi, nafasi ambayo kila chama cha siasa kimepata kwenye uripoti wa vyombo vya habari na pili, ulinganifu kwenye uripoti unaozingatia matukio dhidi ya habari ambazo chombo cha habari kimejiandalia chenyewe.
- Vyanzo vya habari: kuwa na angalau vyanzo vya habari viwili kwenye kila kazi ya kiuandishi (kwenye habari) ni jambo muhimu mno kwenye uripoti wa uchaguzi. Jambo hilo linawawezesha waandishi wa habari kutoa nafasi kwa uwepo wa mitazamo tofauti au taarifa ya kina ili kuwasaidia wapiga kura kufanya maamuzi huku wakiwa na taarifa sahihi. Zaidi ya hayo, inasaidia kubainisha sauti (vyanzo) kwa wadau mbalimbali, wakiwamo wananchi wa kawaida ambao mara kadhaa wamekuwa wakipuuzwa.
- Uripoti wa wagombea kwa namna mbalimbali: kwenye uchaguzi wa urais (wa muungano na ule wa Zanzibar), tangu awali tuliwachagua wagombea watano na watatu mtawalia na kuchambua uwiano wao kwa namna walivyoripotiwa na vyombo vya habari. Hii ndio hatua ya kwanza katika kubaini uripoti wenye usawa au usiokuwa na usawa (wenye mwelekeo wa upande fulani) kwenye chaguzi za wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na madiwani, hatukuangalia wagombea mahsusi (kwa sababu ni wengi), badala yake tulichambua uripoti wa vyama vya siasa vilivyo wateua kugombea. Hili pia lilifanyika ili kubaini uwezekano wa kuwepo upendeleo wa upande fulani.
- Utofauti wa mada: kigezo hiki kinaangalia mada zinazohusiana na uchaguzi na masuala ya mada zinazoibuka kwenye kazi za kiuandishi (habari tofauti). Hii inatoa picha ya vyombo vya habari kwa namna ya mada wanazopenda kuziripoti, mathalani muelekeo wao kisiasa, maendeleo, uchumi au masuala mengine.

3.2 Tathmini ya wagombea

Kwa upande mwingine, tathmini ya ubora wa uripoti wa wagombea wa nafasi ya urais ulitumia vigezo vifuatavyo vya ubora:

- Uripoti wa maudhui ya sera: vyombo vya habari vinatakiwa kuwajuza wapiga kura kuhusu sera za wagombea na mustakabali wao wa baadae. Ubora mzuri humaanisha maudhui ya sera yana nafasi muhimu kwenye uripoti.
- Urejeleaji wa ilani za uchaguzi za vyama: kurejelea ilani za uchaguzi za vyama ni jambo muhimu kwenye uripoti wa uchaguzi kwani huwafahamisha wapiga kura kuhusu programu ambazo wagombea wanakuja nazo. Waandishi wa habari wanapaswa kuling'amua hili.
- Kutekelezeka kwa sera hapo baadae: nyakati za uchaguzi, hutoa ahadi nyingi kwa wapiga kura. Kwa hiyo, ni wajibu wa vyombo vya habari kuhoji na kuuliza kama sera hizo zinatekelezeka sambamba na uwezeshaji kifedha. Ni namna ya kupima uhalisia wa ahadi hizo. Kigezo hiki kinapima ikiwa chombo cha habari kimeripoti kuhusu kipengele hiki au la, kwani wagombea huwa hawajihoji wenyewe.
- Uwepo wa mitazamo tofauti: kwa kuvishirikisha vyanzo vya habari vyenye mtazamo tofauti, vyombo vya habari vinapaswa kuweka usawa kwa maoni yenye mtazamo tofauti, iwe kwa kuwapendelea au hata kukinzana na wagombea.
- Haiba dhidi ya sera – Haiba ya mgombea na sera zake vina mchango katika uchaguzi, japokuwa kwa uzito tofauti. Uchanganuzi ulichunguza jinsi mitazamo hii miwili ya mgombea—sera na haiba—ilivyojitokeza katika uripoti.

Uripoti wa chaguzi kwa kutumia vigezo vya ubora vilivyobainishwa mapema hapo juu ni wa muhimu, ikizingatiwa ukuaji wa uandishi wa habari wa kiraia unaoendelea hapa nchini. Vyombo vya habari na waandishi wa habari ni lazima waimarishe uripoti wao ili kuwa na jamii yenye ufahamu na kuwawezesha wapiga kura kufanya maamuzi sahihi kulingana na taarifa walizonazo. Aina hii ya uripoti wenye ubora wa hali ya juu inapaswa kutofautisha uripoti wa waandishi wa kiraia na uandishi halisi wa habari, ambao hulenga kuibua kweli zilizofichika kuhusu masuala na matukio ambayo yanaathiri jamii nyakati za michakato ya uchaguzi, ama kwa kutumia njia ya kufichua au kufafanua.

3.3 Sampuli ya vyombo vya habari vilivyofanyiwa uchunguzi

Awali tulikuwa na sampuli ya vyombo 47, lakini tuliweza kuvitafiti 46. Dar24 kiliondolewa kutokana na kutokuwepo hewani kipindi cha uchaguzi. Ukiachilia mbali vyombo vya habari vya mtandaoni, vingi vya vyombo hivi vya habari vilijumuishwa kwenye ripoti ya Yearbook ya mwaka 2020. Vyombo vya habari vya uchapishaji vilikuwa 10, ambavyo ni *The Citizen*, *Daily News*, *The Guardian*, *Mwananchi*, *Habari Leo*, *Nipashe*, *Raia Mwema*, *Jamhuri*, *Zanzibar Leo na Zanzibar Mail*. Vyombo vya habari vya utangazaji (redio na TV) vilikuwa 23 ambapo vituo vya redio ni *TBC Taifa*, *Radio Free Africa*, *Radio One*, *Clouds FM*, *Dodoma FM*, *Highlands FM*, *Arusha 1 FM*, *Uvinza Community FM*, *CG FM*, *Sengerema FM*, *Jamii FM Radio*, *Tumbatu FM*, *UFM*, *ZBC Radio*, *Micheweni FM*, *Mjini FM*, *Mkoani FM*, *na vituo vya televisheni ni TBC1*, *ITV*, *UTV (Azam)*, *Star TV*, *na ZBC TV*.

Vyombo vya habari vya mtandaoni vilivyojumuishwa kwa mara ya kwanza kwenye utafiti huu unaohusu uripoti wa uchaguzi vilikuwa 14 ambavyo ni, *Mwanahalisi Online*, *Ayo TV*, *The Chanzo*, *Global TV Online*, *Fullshangwe Blog*, *TBC Online*, *Jambo TV*, *Mwananchi Digital*, *Pambazuko*, *Michuzi Blog*, *GREEN WAVES MEDIA*, *Pemba Today*, *ASAM Online TV*, *na TM TimesMajira*. Sampuli inawakilisha aina mbalimbali za vyombo hivyo vya habari kuanzia vyombo vinavyomilikiwa na serikali mpaka vile vinavyomilikiwa na watu binafsi, vya uchapishaji, vya utangazaji na vya mtandaoni.

3.4 Sampuli ya kazi za kihabari zilizofanyiwa uchunguzi

Tulinunua sampuli za magazeti yote yaliyohusishwa kwenye utafiti huu, tulirekodi taarifa za habari za jioni za kila siku na kuvifuatilia angalau vipindi vitatu kwa wiki kutoka kwenye vyombo vya habari vya utangazaji vilivyokuwa vimeteuliwa. Kipindi kilichofanyiwa utafiti ni kuanzia 28 Agosti 2025 mpaka 03 Novemba, 2025. Sampuli zilizojumuishwa kwenye utafiti zilipatikana kutoka kwenye magazeti, redio na televiusheni. Kwa magazeti, tulichagua habari nane kwenye siku iliyojumuishwa kwenye sampuli, ikijumuisha pia habari tatu zilizokuwa kwenye ukurasa wa mbele kwa siku hiyo, habari ongozi kwenye kurasa za ndani, makala, maoni na maoni ya wahariri. Kwa televisheni na redio, tulichagua habari nne za mwanzo kutoka kwenye taarifa kuu za habari za jioni sambamba na vipindi viwili au vitatu vilivyoenda hewani kwenye siku hiyo, au kwa kipindi cha wiki hiyo, hasa pale ilipokuwa ngumu kuvipata vipindi vyote vitatu kwa siku moja. Baadhi ya vyombo vya habari vilikuwa na kazi chache zilizohusiana na uchaguzi kuliko vyombo vingine. Kwa ujumla, tulichunguza kazi 2,017 za kihabari: 461 kutoka kwenye vyombo vya habari vya uchapishaji, 1,107 kutoka vyombo vya habari vya utangazaji na 449 kutoka kwenye vyombo vya habari vya mtandaoni, kazi zote kwa ujumla wake ndio zilitumika kama kiunzi cha uchambuzi.

3.5 Mafunzo kwa watafiti wasaidizi

Utafiti huu uliandaa mafunzo ya aina tatu kwa watafiti wasaidizi ambao ni waandishi (transcribers), wasimbaji na warekodi (recorders). Warekodi walikuwa na wajibu wa kurekodi vipindi vya redio na televisheni walivyopangiwa. Kisha vipindi hivi vikabadilishwa na wafasiri (transcribers) kutoka kwenye sauti kwenda kwenye maandishi na kisha kukabidhiwa kwa wasimbaji ili waweze kusimba kulingana na mwongozo wa usimbaji (code book) ulivyokuwa umeandaliwa. Usimbaji wa vipindi vilivyobadilishwa na kuwa kwenye hali ya maandishi uliwawezesha wasimbaji kuvifanyia kazi vipindi hivyo kwa urahisi zaidi kuliko vilivyokuwa awali baada ya kurekodiwa kama vipindi halisi vya vya redio na televisheni. Makundi yote haya yalipatiwa mafunzo kwa mujibu wa protokali za mradi wa Yearbook. Jumla ya warekodi (11), wafasiri (7) na wasimbaji 12 walishiriki kwenye mafunzo.

3.6 Udhibiti wa ubora kwa kazi zilizorekodiwa na kusimbwa

Udhibiti wa ubora ni eneo nyeti kwenye mradi wa Yearbook. Unajumuisha mchakato wa kina ili kuhakikisha kwamba vipindi vyote vilivyorekodiwa vinaandaliwa kwa ukamilifu tayari kwa kuingizwa kwenye maandishi. Zaidi ya hayo, tulihifadhi makala za magazeti na nakala za redio na televisheni zilizowekwa kwenye hali ya maandishi kwa matumizi ya rejea hapo baadaye. Utaratibu huu unafaa kwenye kutoa ufafanuzi wa usimbaji ikitokea kuna masuala yataibuka wakati wa kufanya uchambuzi wa data.

3.7 Uchunguzi na uchambuzi wa data

Data zilizofanyiwa usimbaji zilipitia mchakato wa kina wa ukaguzi ili kujihakikishia usahihi na uhakika wa data kabla hazijawekwa kwenye faili moja la SPSS. Utafiti ulitumia zana za kawaida za kitakwimu zikijumuisha uhesabu idadi, na ulinganishaji wa data halisi na zilizofanyiwa upya usimbaji ili kukidhi mahitaji ya vigezo ubora.

4.0 MATOKEO YA UTAFITI

4.1 Muhtasari

Utafiti ulichunguza maeneo manne: uripoti wa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025; maoni ya wananchi kuhusu habari za uchaguzi zilizokuwa zinawekwa kwenye vyombo vya habari vya mitandaoni; uripoti wa vyombo vya habari vya kimataifa kuhusu matukio yaliyojitokeza baada ya uchaguzi; na kuzimwa kwa intaneti na amri ya kutokutoka nje na athari zake kwenye uripoti wa matukio ya baada ya uchaguzi. Jumla ya kazi za kihabari 2,017 kutoka kwenye magazeti (461), vyombo vya habari vya utangazaji (1,107) na vyombo vya habari vya mtaandaoni (449) zilichunguzwa. Kuhusu maoni ya wananchi, utafiti huu ulichambua maoni 17,202 kutoka kwenye taarifa 200 zilizopakiwa kwenye vyombo vya habari vya mtandaoni (tazama sehemu ya hapa chini inayohusu maoni ya wananchi mtandaoni).

4.2 Uripoti wa chaguzi mbalimbali

Uripoti wa vyombo vya habari kuhusu Uchaguzi Mkuu wa 2025 ulijikita kwa wagombea wa urais wa Muungano, urais wa Zanzibar, wabunge wa Muungano (Bunge), wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, na madiwani. Uchaguzi wa rais wa muungano ulivutia sehemu kubwa ya uripoti ukiwa na kazi 676 (asilimia33.5) za kihabari, ukifuatiwa na uchaguzi wa wabunge ukiwa na kazi 359 (asilimia 17.8), urais wa Zanzibar kazi 273 (asilimia 13.5) uchaguzi wa madiwani kwa Tanzania bara uliokuwa na kazi za kihabari 63 (asilimia 3.1). Kwa upande wa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar kulikuwa na kazi 72 (3.6), na uchaguzi wa madiwani wa Zanzibar kazi 16 (asilimia 0.8). Kuna utofauti mkubwa ikilinganishwa na uripoti wa vyombo vya habari kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 ambapo uchaguzi wa rais wa muungano ulikuwa na asilimia 43 wa habari zote zilizohusiana na uchaguzi, ukifuatiwa na uchaguzi wa wabunge uliokuwa na asilimia 28, uchaguzi wa rais wa Zanzibar asilimia 20, uchaguzi wa madiwani (Tanzania bara) asilimia 10, uchaguzi wa wawakilishi kwenye Baraza la Wawakilishi Zanzibar asilimia 5 na uchaguzi wa udiwani Zanzibar asilimia 1.

Kwa upande wa Tanzania Bara, uripoti wa vyombo vya habari kuhusu urais wa muungano ulikuwa asilimia 33.5 ikilinganishwa na asilimia 13.5 kwa uchaguzi wa rais wa Zanzibar. Vyombo vya habari vya Zanzibar viliripoti uchaguzi wa rais wa Zanzibar kwenye kazi 130 (asilimia 47.6) ikilinganishwa na kazi 57 (asilimia 8.4) za rais wa muungano. Hii ni kama ilivyokuwa kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020, hii inaonyesha kwamba vyombo vya habari vina mtazamo wa ndani katika uripoti wake. Vyombo vya habari viliripoti kwa namna tofauti uchaguzi kwa Tanzania Bara na Zanzibar.

Kwenye kazi za kihabari 676, vyombo 6 vya habari vilionekana kuwa na uripoti wa juu (≥4asilimia) kwa uchaguzi wa urais wa muungano, sawa na asilimia 32.8 ya uripoti wote. *TBC Taifa* iliongoza ikiwa na kazi 51 (asilimia7.5), ikifuatiwa na Daily News liyoripoti kazi 36 (asilimia 5.3), na Habari Leo kazi 35 (asilimia 5.2). Vyombo vya habari vya utangazaji pia vilijitokeza, huku UTV (Azam) ikichangia kazi 32 (asilimia 4.73) na Dodoma FM kazi 30 (asilimia 4.4), wakati Jamhuri ilichangia kazi 31 (asilimia 4.6).

Kwenye kazi 273 za kihabari zilizohusu uchaguzi wa Zanzibar, vyombo vya habari 6 vilionekana kuwa na uripoti wa juu (≥4%) kwa pamoja vikichangia asilimia 39.9 ya uripoti wote. *Redio ZBC* iliongoza kwa kuwa na kazi 28 (asilimia 10.3) ikifuatiwa na *Asam Online* kazi 25 (asilimia 9.2), na *Zanzibar Leo* (asilimia 21; 7.7). *Nipashe na ZBC TV* kila kimoja kilichangia kazi 12 (asilimia 4.4), wakati *Pemba Today* ilikuwa na kazi 11 (asilimia 4.0).

4.3 Muktadha wa uripoti

Matukio au kauli zinazohusishwa na chama tawala (CCM) zilijitokeza kuwa kichocheo muhimu zaidi cha uripoti, zikichangia asilimia 28.2 (ikishuka kutoka asilimia 33 mwaka 2020), sawa na punguzo la asilimia 4.8. Kwa upande mwingine, matukio yanayohusishwa na vyama vya upinzani yalichangia asilimia 24.1 ya uripoti wa uchaguzi katika vyombo vya habari, yakiongezeka kutoka asilimia 23 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 1.1. Jitihada za vyombo vyenyewe vya habari zilichangia asilimia 27.8, ikilinganishwa na asilimia 19 mwaka 2020, huku kauli au mikutano na waandishi wa habari ikichangia asilimia 4.0, ikilinganishwa na asilimia 11 mwaka 2020, sawa na upungufu wa asilimia 7. Vichocheo vingine vya uripoti vilivyobaki, kama vile vyombo vya usalama, mashirika ya kiraia (CSOs), viongozi wa dini na wengineo, vilichangia asilimia 16.



Visababishi vya uripoti wa habari uchaguzi mkuu 2025



Visababishi vya uripoti kwa CCM na vyama shindani

	Kampeni za CCM/PC/matamko	Kampeni za upinzani/PC/matamko
Vya binafsi n (%)	403 (26%)	367 (24%)
Vya serikali n (%)	165 (34%)	120 (25%)
Vya uchapishaji n (%)	147 (32%)	108 (23%)
Vya utangazaji n (%)	215 (19%)	265 (24%)
Vya mtandaoni n (%)	206 (46%)	114 (25%)

Wakati wa kipindi cha uchaguzi, habari zilizoandikwa kwa jitihada za chombo husika cha habari ziliongezeka kwa asilimia 8.8, ikiwa ni jumla ya kazi 560. Matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba vyombo binafsi vya habari vilifanya vizuri kwenye eneo hili vikichangia jumla ya kazi 458(asilimia 81.8), wakati vyombo vinavyomilikiwa na serikali vikichangia kazi 102 (asilimia 118.2). Kwa upande wa aina za vyombo vya habari, vyombo vya habari vya utangazaji vilichangia karibu theluthi mbili ya habari zote zilizoandikwa kwa jitihada za chombo husika cha habari ikiwa ni jumla ya kazi 348 (asilimia 62.1). Hivi vilifuatiwa na vyombo vya habari vya uchapishaji ambavyo vilikuwa na kazi 129 (asilimia 23.0) na vyombo vya habari vya mtandaoni ambavyo vilikuwa na kazi chache zaidi, yaani kazi 83 tu ambazo ni sawa na asilimia 14.8. kulikuwa na utofauti katika mtawanyiko wa habari zilizoandikwa kwa jitihada za chombo husika cha habari. Vyombo vya habari ambavyo vilichangia kwa asilimia 5 au zaidi ya habari zote zilizoandikwa kwa jitihada za chombo husika cha habari ni pamoja na *CG FM* ikiwa na kazi 32 (asilimia 5.7), *Sengerema FM* kazi 31 (asilimia 5.5), na Pambazuko yenye kazi 29 (asilimia 5.2). Kinyume chake, vyombo vya habari vyenye idadi ndogo ya habari zilizoandikwa kwa jitihada za chombo husika cha habari ni *Fullshangwe Blog na Timesmajira(TM)* ambavyo kila kimoja kilikuwa na kazi moja tu ambayo ni sawa na asilimia 0.18.

Hakukuwa na mlingano katika namna vyombo binafsi vya habari vilivyoripoti masuala ya uchaguzi ikilinganishwa na vyombo vya habari vya serikali, vivyo hivyo kwa vyombo vya habari vya uchapishaji, vya utangazaji na vya mtandaoni. Kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025, vyombo vya habari vya serikali viliripoti kuhusu matukio ya chama tawala (CCM) na ya vyama vya upinzani kwa kiwango cha asilimia 34 na 27.7 mtawalia ikilinganishwa na asilimia 41 na 17 kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020. Ongezeko kwenye uripoti wa vyama vya upinzani kwa namna fulani unaweza ukahusishwa na wingi wa wagombea walioshiriki kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025: kulikuwa na wagombea 13 wa nafasi ya urais mwaka 2020 ikilinganishwa na wagombea 17 mwaka 2025. Vyombo vya habari vya uchapishaji viliripoti matukio ya CCM kwa asilimia 31.9, wakati vyama vya upinzani vikipata uripoti wa asilimia 23.4. Kinyume chake, vyombo vya habari vya utangazaji vikiwamo redio na televisheni, viliripoti matukio ya CCM kwa asilimia 19.4 ikilinganishwa na asilimia 23.9 ya uripoti kwa vyama vya upinzani. Uripoti wa vyombo vya habari vya mtandaoni ulikuwa na asilimia 45.9 kwa CCM na upinzani ulipata asilimia 25.4.

Vyombo vitatu vya habari vilivyoshika nafasi tatu za juu kwa kuiripoti CCM ni: *Habari Leo* – ikiwa na kazi 38 (asilimia 6.69), *Michuzi Blog* – kazi 32 (asilimia5.6) na *Fullshangwe Blog* – kazi 27 (asilimia 4.8). Tukiviangalia vyombo vya habari vinavyomilikiwa na serikali, *TBC1 na Zanzibar Leo* viliongoza kwenye uripoti wa CCM, ambapo vilikuwa na uripoti wa asilimia 3.7, vikifuatiwa na *Daily News* (asilimia3.5), *ZBC TV* (asilimia 3.2), na *TBC1* (asilimia 2.6). Kwa upande wa chombo kimoja kimoja cha habari, uripoti wa vyama vya upinzani

haukuwa na utofauti sana kiasi cha kuwa na chombo kimoja cha habari kuchomoza zaidi ya vingine. Vyombo vya habari vilivyokuwa na uripoti wa angalau asilimia 5 na zaidi kwa vyama vya upinzani ni *TBC Taifa* – iliyokuwa na kazi 29 (asilimia 6), *UTV (Azam)* – kazi 29 (asilimia 6), na *Jamii FM Radio* – kazi 26 (asilimia 5.3).

Ukiyangalia matokeo haya ya utafiti kwa ukaribu zaidi, yanabainisha kwamba vyombo vya habari viliripoti matukio mbalimbali ya vyama vya upinzani (CHAUMMA, CUF, NCCR-Mageuzi na NLD) yaliyohusu uchaguzi badala ya kumakinikia kwenye chama kimoja tu cha siasa. Hata hivyo, kati ya vyama 16 vya siasa ambavyo vilishiriki kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025, CHAUMMA kiliripotiwa zaidi kikiwa na kazi 72 (asilimia 3.6), kikifuatiwa na NLD kilichokuwa na kazi 57 (asilimia2.8). Habaripicha ifuatayo inaonyesha tukio lililoleteleza uripoti wa kazi zote zilizofanyiwa uchambuzi na mtawanyiko wake kwa aina ya umiliki wa chombo cha habari au jinsi kinavyojinasibisha (cha serikali, cha binafsi, cha uchapishaji, cha utangazaji au cha mtandaoni).

4.4 Vyanzo vya habari

Uripoti wa kiuandishi wa habari huwa unaweka kipaumbele kwenye vyanzo vingi vya habari. Habari yenye chanzo kimoja cha habari ni habari ambayo haijakamilika na haiisaidii chochote hadhira lengwa katika kulielewa tukio au hali inayoripotiwa. Kwa ujumla, asilimia 55, sawa na kazi 1,110 za kihabari, zilikuwa na vyanzo viwili au zaidi vya habari, na asilimia 45 (kazi 907) zilikuwa na vyanzo 0-1 vya habari. Tukilinganisha Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 na 2025, hakuna utofauti wowote kwenye eneo hili la vyanzo vya habari. Kwa mwaka 2020, habari zilizokuwa na vyanzo vya habari 0-1 vilikuwa ni asilimia 45 ya habari zote zilizofanyiwa uchambuzi, wakati habari zilizokuwa na vyanzo viwili au zaidi vya habari zilikuwa ni asilimia 55. Tafiti za mradi wa Yearbook zilizopita (2018, 2019, 2020, 2022) zimeonesha kuwa uripoti wa kutegemea chanzo kimoja ni pengo la kitaaluma katika uandishi wa habari nchini, hali ambayo imepewa jina la “ugonjwa wa chanzo kimoja” (single-source syndrome).

La kutia wasiwasi zaidi, na linalotoa ishara ya tahadhari ya kitaaluma katika matokeo haya, ni uwepo wa maudhui ya vyombo vya habari yasiyo na vyanzo kabisa. Aina hii ya uripoti ilijitokeza zaidi katika makala za maoni, hususan safu za maoni (n=29; asilimia 1.4) pamoja na tahariri (n=25; asilimia 1.2). Ingawa ni sawa kwa waandishi wa maoni kuwasilisha mitazamo yao, wanapaswa kujadili maoni yao kwa kuzingatia pia mitazamo ya wengine. Matumizi ya chanzo kimoja yanazidishwa na matumizi yanayoonekana ya uripoti wa kimatukio (episodic reporting), ambapo waandishi wa habari za uchaguzi huripoti matukio pekee bila kwenda mbali zaidi, kwa mfano kuthibitisha kauli au tuhuma, au kuhakiki ukweli wa taarifa kwa vyanzo mbalimbali.

Kwenye matumizi ya vyanzo vingi vya habari, hakuna utofauti mkubwa kati ya vyombo vya habari binafsi (asilimia 54.2) na vile vinavyomilikiwa na serikali (asilimia 57.6). Vyombo vya habari vya uchapishaji vinaongoza katika kutumia vyanzo vingi vya habari (asilimia 62.7), vikifuatiwa na vyombo vya habari vya utangazaji (asilimia 54.55) na vya mtandaoni (asilimia 48.6).

Kati ya vyombo vya habari vilivyotumika kwenye sampuli, vyombo vya habari vilivyoonesha kutumia vyanzo vya habari viwili au zaidi, na kwa hiyo, kuwa na usawa katika uripoti wa uchaguzi ni ITV (asilimia 56; 5), Daily News 47 (asilimia 4), Zanzibar Leo (asilimia 44;4), ZBC Radio (asilimia 42; 3), vile vile *Habari Leo*, *Star TV*, *CG FM*, *ZBC TV*, *UTV* (Azam), na Mwananchi, kila kimoja kikiwa na asilimia 3. Kinyume chake, vyombo vya habari vilivyokuwa na habari chache zilizokuwa na vyanzo vya habari viwili au zaidi na hivyo kuonesha udhaifu katika matumizi ya vyanzo vingi vya habari nyakati za uchaguzi ni pamoja na *Ayo TV*, *Green Waves Media*, *Zanzibar Mail*, *Mwanahalisi Online na Arusha 1 FM*.

Mchanganuo wa vyanzo vya habari kwa makundi ya vyombo vya habari



Mwanamke kama chanzo cha habari

Kwa ujumla, utendaji wa vyombo vya habari kwenye eneo hili umeimarika kidogo ikilinganishwa na matumizi ya mwanamke kama chanzo cha habari wakati wa Uchaguzi Mkuu wa 2020. Wakati matumizi ya mwanamke kama chanzo cha habari yakiwa ni asilimia 20 ya kazi za kiuandishi wa habari zilizofanyiwa uchambuzi kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020, uwiano wa kazi za kiuandishi wa habari kwenye eneo hilo kwa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 umeongezeka hadi kufikia asilimia 38,kukiwa na kazi za kihabari 766 zilizojumuisha sauti ya angalau mwanamke mmoja kama chanzo cha habari wakati wa kipindi cha uchaguzi. Kwenye eneo hili, hakuna utofauti mkubwa kati ya vyombo vya habari vya umma (asilimia36.6) na vile vya binafsi (asilimia 38.8). Hali iko hivyo pia kwenye utendji wa magazeti (asilimia32.7), vyombo vya habari vya utangazaji (asilimia 39.5) na vyombo vya habari vya mtandaoni (asilimia 40.8). Kwa ujumla, vyombo vya habari na waandishi wa habari wanaenenda kwa namna moja linapokuja suala la kumtumia mwanamke kama chanzo cha habari. Utofauti wao ni kama haupo kabisa.

Idadi ya wanawake kama chanzo cha habari



Vyombo vya habari vilivyokuwa na habari 28 au zaidi ambazo ziliwajumuisha wanawake kama vyanzo vya habari ndivyo vilivyofanya kazi nzuri zaidi katika kuzifanya sauti za wanawake zisikike zaidi kwenye uripoti wa uchaguzi. Vyombo hivyo ni pamoja na *Jamii FM Radio* (kazi 30, asilimia 3.92), *ITV* (kazi asilimia 29, 3.79), *Dodoma FM* (kazi asilimia 28, 3.66), na *CG FM* (kazi asilimia 28, 3.66). Vyombo vya habari vilivyojipambanua kwa kutokuwa na mwanamke kama chanzo cha habari kwenye kazi 40 au zaidi ni pamoja na TBC Taifa (58), H*abari Leo* (55), *Dodoma FM* (46), *Jamhuri* (45), *ZBC Radio* (42), *UTV (Azam)* (41), na *Daily News* (40).

Matumizi vya nyanzo vya habari



Je sauti za wananchi zina nafasi?

Kuwatumia wananchi wa kawaida (wapiga kura) kama vyanzo vya habari nyakati za uchaguzi ni muhimu kama ilivyo muhimu kwa wagombea na vyama vya siasa. Kuwapa wananchi nafasi na muda wa hewani kunawaongezea uwezo wa kufikisha mitazamo na malalamiko yao kuhusu uchaguzi, na kutengeneza jukwaa la ushirikishwaji wa wananchi jambo ambalo ni muhimu sana kwenye uchaguzi wa kidemokrasia. Kimsingi, wagombea wanapaswa kufahamu wapiga kura wao wanataka nini, kama ilivyo kwa wapiga kura wanavyohitaji kusikia wagombea wanasema nini. Kama ilivyokuwa kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka 2020, wananchi hawakupewa kipaumbele. Matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba ni kazi 223 tu ya kazi zilizofanyiwa uchambuzi (asilimia 11) ndizo zilitumia wananchi kama vyanzo vyao vya habari. Mwaka 2020 ilikuwa ni asilimia 10 tu. Vyombo vya habari vinavyomilikiwa na serikali vilibeba kwa uchache sauti za wananchi wa kawaida (asilimia12.1) kuliko ilivyokuwa kwa vyombo binafsi vya habari (asilimia 87.9). Vyombo vya serikali vilijielekeza zaidi kwa wagombea huku wananchi wa kawaida wakipewa uzito mdogo. Kwa msingi wa aina za vyombo vya habari, vyombo vya habari vya utangazaji vilirusha zaidi hewani sauti za wananchi wa kawaida (asilimia70.85) ikilinganishwa na vile vya uchapishaji na vile vya mtandaoni (asilimia17.5 na 11.7).

Tunapokichambua chombo cha habari kimoja kimoja, CG FM kiliongoza kikiwa na asilimia 12.1 ya uripoti uliojielekeza kwenye kujumuisha sauti za wananchi. *ITV* ilifuatia ikiwa na asilimia 8.5, *Star TV* ilikuwa na asilimia l6.3, na *Pemba Today* ikiwa na asilimia 5.4. *Sengerema FM* ilikuwa na asilimia 4.9, wakati RFA, *Dodoma FM*, na Mkoani FM kila kimoja kikiwa na asilimia 4.5. Kwa upande mwingine, vipo vyombo vingi vya habari vilivyokuwa na asilimia chini ya 1 ya uripoti uliolenga kupaza sauti za wananchi wa kawaida. Vyombo hivi ni pamoja na *Daily News*, *Habari Leo*, *Zanzibar Mail*, *Radio One*, *Arusha 1 FM*, *Jamii FM Radio*, *Global TV Online*, *Fullshangwe Blog*, *Pambazuko*, *The Citizen*, *Jamhuri*, *na Mwananchi Digital*. Miongoni mwa vyombo nane bora vya habari vilivyoonyesha kujali sauti za wananchi, nusu ya vyombo hivyo, ni vyombo vya habari vya kijamii *CG FM*, *Sengerema FM*, *Dodoma FM*, *na Mkoani FM*. Zikiwa kama redio za kijamii, redio hizi zimelenga kuinua jamii zao na kwa kufanya hivyo wakati wa uchaguzi ni ushahidi mzuri kwamba wanaziishi ndoto zao.

4.5 Uripoti wa vyombo vya habari kuhusu wagombea

4.5.1 Wagombea wa Urais wa Muungano

Kuna vyama vya siasa 19 vilivyosajiliwa na miongoni mwa hivyo ni vyama 17 tu ndiyo wagombea wake waliidhinishwa na Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC) kugombea nafasi ya urais wa muungano. CHADEMA kama chama kikuu cha upinzani walikosa sifa za kushiriki kwenye Uchaguzi Mkuu, ikiwamo kuweka mgombea wa urais, baada ya kushindwa kusaini Kanuni za Maadili za mwaka 2025 wakihitaji kwanza pafanyike mageuzi ya kisiasa. Chama kingine cha siasa, ACT-Wazalendo , chama kikuu cha pili cha upinzani, kilishuhudia mgombea wake wa urais Ndugu Luhaga Mpina akienguliwa na INEC[Uamuzi wa Pingamizi za Uteuzi wa Wagombea wa Kiti cha Rais kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,https://www.inec.go.tz/news/uamuzi-wa-pingamizi-za-uteuzi-wa-wagombea-wa-kiti-cha-rais-kwa-jamhuri-ya-muungano-wa-tanzania] baada ya kuwekewa pingamizi na Mwana Sheria Mkuu wa Serikali Ndugu Hamza Saidi Johari, taarifa ambayo haikuwekwa wazi na INEC.

Uripoti wa mgombea urais wa CCM

Rais aliyeko madarakani na mpeperusha bendera ya CCM, Samia Suluhu Hassan ndiye aliyeripotiwa zaidi na vyombo vingi vya habari miongoni mwa wagombea wote wa urais wa muungano. Aliripotiwa kwa asilimia 56.2 (380) ya kazi zote za kihabari zilizohusiana na wagombea urais wa muungano, wakati habari 676 sawa na asilimia 43.5 hazikumtaja. Uripoti wa mgombea wa CCM ulifanywa zaidi na vyombo binafsi vya habari (asilimia 74.0) ikilinganishwa na asilimia 26.1 aliyoipata kwenye vyombo vya habari vinavyomilikiwa na serikali. Kwa misingi ya aina za vyombo vya habari, uripoti wake kwa namna fulani ulikuwa sawa huku vyombo vya habari vya utangazaji vikimripoti kwa asilimia 39.0, vyombo vya habari vya mtandaoni kwa asilimia 31.8, na vya uchapishaji asilimia 29.2. Kijiografia, sehemu kubwa ya uripoti wake ulitoka kwenye vyombo vya habari vya Tanzania Bara (asilimia 89.5) huku asilimia 10.5 ya uripoti wake ukitoka kwenye vyombo vya habari vya Zanzibar.

Upana wa uripoti kwa makundi ya vyombo vya habari

Wagombea wa urais muungano	Samia Suluhu Hassan	Salum Mwalimu	Gombo Samandito Gombo	Kunje Ngombale Mwiru	Doyo Hassan Doyo	Wagombea wengine
						
Wagombea waliotajwa?						
Hapana	294 (44%)	602 (89%)	645 (95%)	644 (95%)	616 (91%)	508 (75%)
Ndiyo	380 (56%)	72 (11%)	31 (5%)	29 (4%)	57 (8%)	164 (24%)
Jumla	676 (100%)	676 (100%)	676 (100%)	676 (100%)	676 (100%)	676 (100%)
Umiliki wa chombo cha habari						
Binafsi	281 (74%)	59 (82%)	22 (71%)	24 (83%)	41 (72%)	115 (70%)
Serikali	99 (26%)	13 (18%)	9 (29%)	5 (17%)	16 (28%)	49 (30%)
Jumla	380 (100%)	72 (100%)	31 (100%)	29 (100%)	57 (100%)	164 (100%)
Aina ya chombo cha habari						
Cha uchapishaji	111 (29%)	31 (43%)	16 (52%)	7 (24%)	18 (32%)	47 (29%)
Vya utangazaji	148 (39%)	33 (46%)	11 (35%)	18 (62%)	29 (51%)	99 (60%)
Vya mtandaoni	121 (32%)	8 (11%)	4 (13%)	4 (14%)	10 (18%)	18 (11%)
Jumla	380 (100)	72 (100%)	31 (100%)	29 (100%)	57 (100%)	164 (100%)
Kijiografia						
Vya bara	340 (89%)	72 (100%)	31 (100%)	29 (100%)	51 (89%)	150 (91%)
Vya Zanzibar	40 (11%)	-	-	-	6 (11%)	14 (9%)
Total	380 (100%)	72 (100%)	31 (100%)	29 (100%)	57 (100%)	164 (100%)

Uripoti wa mgombea urais wa CCM ulikuwa umejikita kwa kiasi kikubwa katika vyombo vichache vya habari. Wachangiaji wakubwa walikuwa Habari Leo na TBC Taifa, kila kimoja kikichangia asilimia 5.8 ya marejeo yote, vikifuatiwa kwa karibu na Blogu ya Fullshangwe (asilimia 5.5), *Green Waves Media* (asilimia 4.7), *Global TV Online* (asilimia 4.2) na *Daily News* (asilimia 4.0). Kinyume chake, baadhi ya vyombo vya habari vilichangia chini ya asilimia 1 kila kimoja katika uripoti wake, ikiwemo *Sengerema FM*, *Tumbatu FM*, *Pemba Today*, *Asam Online* (asilimia 0.5 kila kimoja), pamoja na *Zanzibar Mail na Mjini FM*. Hivi vilikuwa hasa vyombo vya habari vya ndani au vya kijamii, jambo linaloonesha ushiriki mdogo katika uripoti wa uchaguzi katika ngazi ya kitaifa.

Uripoti wa mgombea urais wa CHAUMMA

Mgombea urais wa CHAUMMA, Ndugu Salum Mwalimu alipata uripoti mdogo wa vyombo vya habari akitajwa kwenye kazi 72 tu sawa na asilimia10.7 ya kazi zote zilizofanyiwa uchambuzi, huku asilimia 89.1 (602) ya kazi hizo hazikumtaja kabisa. Uripoti wake ulifanywa zaidi na vyombo binafsi vya habari (asilimia 81.9), wakati vyombo vya habari vya serikali vikichangia kwa asilimia 18.1 pekee. Vyombo vya habari vya utangazaji ndivyo vilivyotawala uripoti wake kwa asilimia 45.8 vikifuatiwa kwa karibu na vyombo vya habari vya uchapishaji (asilimia 43.1), huku vyombo vya habari vya mtandaoni vikifanya hivyo kwa asilimia11.1tu. Uripoti wake wote ulifanywa na vyombo vya habari vya Tanzania bara pekee. Kuonekana kwake kwenye vyombo vya habari kulikuwa zaidi kwenye stesheni za redio hasa *Clouds FM* na *Dodoma FM*, ambapo kila kimoja kilikuwa na mitajo ya asilimia 11.1. Uripoti wa wastani ulifanywa na mchanganyiko wa vyombo vya habari vya uchapishaji, vya kidijitali, na vile vinavyomilikiwa na serikali ikijumuisha *Nipashe*, *TBC Taifa*, *na Mwananchi Digital* (kila kimoja kikiwa na asilimia 8.3). Vyombo vingine vyote vilimtaja kwa nadra sana huku vyombo vingi kati ya hivyo vikichangia mtajo mmoja tu (asilimia1.4) pekee.

Uripoti wa mgombea urais kwa chama cha CUF

Mgombea urais kwa chama cha CUF Ndugu Gombo Samandito Gombo, alipata uripoti wa hali ya chini wa vyombo vya habari akijitokeza kwenye kazi 31 (asilimia4.6) tu ya kazi zote zilizohusiana na uripoti wa wagombea urais wa muungano. Uripoti aliopata, kwa sehemu kubwa ulitoka kwenye vyombo vya habari vya binafsi (asilimia 71.0), ilihali kwenye vyombo vya habari vya serikali alipata asilimia 29 ambao ni uripoti mkubwa kuliko uripoti waliopata wagombea wengine wa upinzani. Kwa misingi ya aina ya chombo cha habari, vyombo vya habari vya uchapishaji viliripoti zaidi kampeni zake kwa asilimia 51.6 vikifuatiwa na vyombo vya habari vya utangazaji kwa asilimia 35.48 na vile vya mtandaoni kwa asilimia 12.9. Jambo la kukumbuka na kuzingatia ni kwamba, uripoti wote aliopata Ndugu Gombo, ulitoka kwenye vyombo vya habari vya Tanzania Bara, huku kukiwa hakuna chombo chochote kutoka Zanzibar kilichofanya hivyo. Kwa pamoja, *Daily News* na *TBC Taifa* waliripoti kampeni za Gombo kwa asilimia 29 tu.

Uripoti wa mgombea urais wa AAFP

Bwana Kunje Ngombale Mwiru, mgombea urais wa AAFP, alipata nafasi ndogo sana kwenye uripoti wa vyombo vya habari wakati wa kipindi cha uchaguzi, akijitokeza kwenye kazi 29 (4.3%). Sehemu kubwa ya vyombo vilivyomripoti mgombea huyu, ni vyombo binafsi vya habari (82.8%), wakati kwenye vile vya serikali alipata asilimia 17.2. Vyombo vya habari vya utangazaji vilikuwa na asilimia 62.1 ya uripoti kwenye kampeni zake, vikifuatiwa na vyombo vya habari vya uchapishaji kwa asilimia 24.1, na vile vya mtandaoni kwa asilimia 13.8. Kama ilivyokuwa kwa wapinzani wake CHAUMMA na CUF, Bwana Kunje alipata uripoti wote kutoka vyombo vya habari vya Tanzania Bara. Tukiangalia chombo cha habari kimoja kimoja, Bwana Kunje aliripotiwa zaidi na *TBC Taifa*, *Dodoma FM na UTV (Azam)*, kila kimoja kikiwa na asilimia 13.8, vikifuatiwa na *Jamhuri na ITV*, kila kimoja kikiwa na asilimia 10.3.

Uripoti wa mgombea urais wa NLD

Ndugu Doyo Hassan Doyo, aliyekuwa kwenye kinyang'anyiro cha urais kwa tiketi ya NLD, alitajwa kwenye kazi 57 sawa na asilimia 8.4 ya kazi zote zilizofanyiwa uchambuzi, ikionesha uripoti wa wastani, japo ni wa kiwango cha chini ikilinganishwa na mgombea anayeongoza kwa kuripotiwa zaidi. Kwa kiasi kikubwa uripoti wake uliongozwa na vyombo binafsi vya habari (asilimia 71.9), huku vile vya serikali vikichangia kwa asilimia 28.1. Vyombo vya habari vya utangazaji ndio vilikuwa na sehemu kubwa ya uripoti wake kwa asilimia 50.9 vikifuatiwa na vile vya uchapishaji kwa asilimia 31.6, na vile vya mtandaoni kwa asilimia 17.5. Tofauti na wagombea wengine wa vyama vya upinzani kwenye nafasi ya urais, Bwana Doyo alipata uripoti kiasi kutoka kwenye vyombo vya habari vya Zanzibar (asilimia 10.5), japo sehemu kubwa ya uripoti wake ulifanywa na vyombo vya habari vya Tanzania Bara. Kwa pamoja, *TBC Taifa*, *UTV (Azam)*, *Raia Mwema*, *na Clouds FM* vilimuonesha Ndugu Doyo kwenye kampeni zake kwa asilimia 33.

Wagombea wengine wa nafasi ya urais

Wagombea wengine kumi na wawili, Bwana Hassan Kisabya Almas (NRA), Bwana Coster Jimmy Kibonde (MAKINI), Bwana Abdul Juma Mluya (DP), Bi. Saum Hussein Rashid (UDP), Bi. Mwajuma Noty Mirambo (UMD), Bwana Georges Gabriel (ADA-TADEA), Bwana Twalib Ibrahim Kadege (UPDP), Bwana Majalio Paul Kyara (SAU), Bwana Wilson Elias Mulumbe (ADC), Bwana Haji Ambar Khamis (NCCR-MAGEUZI), Bwana David Daud Mwaijojele (CCK), na Bwana Yustas Mbatina Rwamugira (TLP), kwa pamoja walipata asilimia 24.3 (164) ya uripoti wa vyombo vya habari, ikiwa ni chini ya nusu ya uripoti aliopata mgombea urais kwa tiketi ya CCM aliyepata asilimia 56.2.

Sawa na ilivyokuwa kwa wagombea wengine, sehemu kubwa ya uripoti wao ilitoka kwenye vyombo binafsi vya habari (asilimia 70.1), wakati vyombo vya habari vya serikali vikiripoti kwa asilimia 29.9. Vyombo vya habari vya utangazaji vilifanya vizuri kwenye eneo hili vikiwa na asilimia 60.4 ya uripoti, vikifuatiwa na vyombo vya habari vya uchapishaji ambavyo vilifanya hivyo kwa asilimia 28.7. Vyombo vya habari vya mtandaoni vilijipambanua kwa asilimia asilimia 11.0 tu. Kijiografia, sehemu kubwa ya uripoti (asilimia 91.5) ulifanywa na vyombo vya habari vya Tanzania bara, wakati vyombo vya habari vya zanzibar viliofanya hivyo kwa asilimia 8.5 tu.

Kwa kuviangalia vyombo vya habari vinavyomilikiwa na serikali, hasa hasa *TBC1*, *TBC Taifa*, *Daily News*, *Habari Leo*, *ZBC TV*, *ZBC Radio*, *Zanzibar Leo*, *na Zanzibar Mail*, mgombea urais kupitia CCM alipata mitajo 99. Hii ilikuwa ni mitajo mingi zaidi ikilinganishwa na wagombea wengine kwenye ngazi hiyo: Bwana Doyo alitajwa mara 16, Bwana Salum Mwalimu mara 13, Bwana Gombo mara 9, na Bwana Kunje alitajwa mara 5. Kwa ujumla wao, wagombea wengine 12 waliobakia walitajwa mara 49 kwenye vyombo vyote vya habari. Matokeo haya ya utafiti hayatofautiani na yale ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020, ambapo mgombea urais kwa tiketi ya CCM, John Pombe Magufuli, aliripotiwa mara nyingi zaidi na vyombo vya habari vya serikali kwa asilimia 81, ikilinganishwa na Lissu, ambaye alipeperusha bendera ya CHADEMA na kupata asilimia 26 ya uripoti wa vyombo vya habari vya serikali. Kwa kuzingatia kwamba, vyombo hivi vinagharamiwa na serikali, aina hii ya uripoti inazalisha maswali muhimu kama aina hii ya uripoti ilifanywa kwa makusudi ili kukipendelea chama tawala, CCM na mgombea wake ama vinginevyo.

Sehemu ya 4 ya Kanuni za Urushaji wa Matangazo ya Uchaguzi wa Vyama vya Siasa za mwaka 2020 (The Political Party Elections Broadcasts Code of 2020) inaeleza kuwa, "kila mtoa huduma za maudhui atahakikisha kwamba (a) matangazo yote ya habari wakati wa uchaguzi mkuu yanaripotiwa na kuwasilishwa kwa namna ya kitaalamu, isiyoegemea upande wowote, kwa usawa na kwa uwiano katika uripoti wa vyama vyote vya siasa." Zaidi ya hayo, kabla ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025, Idara ya Habari-Maelezo ilichapisha muongozo kwa vyombo vya habari na waandishi wa habari kuhusu namna ya kuripoti uchaguzi wa rais, wabunge, na madiwani ulioitwa "Mwongozo kwa Vyombo vya Habari na Waandishi wa Habari katika Kuripoti Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani wa Mwaka 2025." Mwongozo ulivitaka vyombo vya habari kuwa na uripoti wenye usawa kwa vyama vyote vya siasa na wagombea wakati wa kipindi cha kampeni. Wajibu huu wa kitaaluma ni mkubwa zaidi kwa vyombo vya habari vya serikali ambavyo vinaendeshwa kwa kodi za wananchi. Kuwepo kwa ukweli kwamba vyombo vya habari vinavyomilikiwa na serikali havikujali wala kuzingatia miongozo inayoandaliwa na taasisi nyingine za kiserikali, kunaacha maswali mengi.

Wagombea urais wanawake

Ili kuuelewa uripoti wa vyombo vya habari kwa wagombea urais wanawake, utafiti huu ulichambua jinsi walivyoripotiwa kwenye vyombo vya habari. Mgombea urais wa CCM, Samia Suluhu Hassan alipata uripoti wa kiwango cha juu kilichomnufaisha kutokana na kwamba yeye alikuwa akipeperusha bendera ya chama tawala na ni rais aliyeko madarakani. Kinyume chake, wagombea wengine wanawake, Saum Hussein Rashid (UDP) na Mwajuma Noty Mirambo (UMD), walipata uripoti wa chini wa takribani asilimia 4 ya uripoti wote uliohusu uchaguzi. Yaani, ni kama hawakuwemo kabisa kwenye uripoti wa vyombo vya habari. Matokeo haya ya utafiti wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025, hayatofautiani na hali ilivyokuwa kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020, ambapo wanawake wawili waliogombea nafasi ya urais wa muungano, Queen Cuthbert Sendiga (ADC) na Cecilia Augustino Mmanga (Demokrasia Makini), walipata uripoti wa chini kwa asilimia 5 na asilimia 3 mtawalia.



Tathmini ya picha na habari zilizopewa kipaumbele

Utafiti huu ulichunguza uwakilishi wa vyama vya siasa kupitia picha zilizowekwa kwenye kurasa za mbele za magazeti. Kwenye kipindi chote cha uchaguzi, magazeti 62 yaliweka picha kuu zinazohusiana na kampeni za vyama vya siasa kwenye kurasa zao za mbele. Kati ya picha 62 zilizofanyiwa uchunguzi, chama tawala, CCM kilikuwa na kazi 54 (asilimia 87.1). Kwa ulinganisho, vyama vya upinzani kwa pamoja vilikuwa na picha 8 tu ambazo ni sawa na asilimia 12.9 ya picha zote zilizokuwa kwewnye kurasa za mbele za magazeti. Kwa mtazamo wa nani aliripotiwa zaidi kwenye habari kuu za kurasa za mbele za magazeti, Samia aliripotiwa na habari 26, akifuatiwa na Salum Mwalimu, na Gombo (habari tatu kila mmoja), wakati Kunje na Doyo kila mmoja alionekana kwenye habari 2 tu.

Uchambuzi wa taarifa za habari kwenye vyombo vya habari vya utangazaji ulionyesha mwelekeo wa kuvutia: kama kawaida, CCM waliendelea kutawala uripoti wa habari za kwanza. Hili liko wazi zaidi unapochunguza idadi ya mitajo kwenye redio na televisheni. Kwa muktadha huu, matukio na kampeni za Samia yalikuwa kinara kwenye uripoti, akijitokeza mara 47 kwenye habari za mwanzo kwenye taarifa za habari.

Kinyume chake, japo si haba, Doyo, alikuwa na mitajo michache akiwa ametajwa mara 6. Kunje alifuatia kwa karibu akijitokeza mara 5, wakati Salum Mwalimu na Gombo walikuwa na mwisho kwa kupata mitajo 3 na 0 mtawalia. Utofauti huo katika mitajo unaibua maswali ya msingi kuhusu mienendo ya uripoti wa uchaguzi na ushawishi wa mikakati ya vyama vya siasa kwenye mtazamo wa wapiga kura. Hali hii pia inahamasisha uchunguzi zaidi wa sababu zinazochangia tofauti hii kubwa ya uangalizi wa vyombo vya habari, jambo ambalo linaelezwa kwa kina katika sehemu ya 5.0.



Uripoti wa maudhui yanayohusu sera

Kuripoti kuhusu sera za wagombea urais ni jambo la msingi katika uripoti wa habari za uchaguzi zikiwahabarisha na kuwaongoza wananchi katika kujifanyia uamuzi wao. Utafiti ulichunguza ikiwa maudhui ya sera na ahadi za wagombea ziliweza kuripotiwa vizuri angalau kwenye aya mbili za uripoti wa habari. Kwa sehemu kubwa, sera za mgombea urais kwa tiketi ya CCM ziliripotiwa kwenye kazi 285 zilizofanyiwa uchambuzi ikilinganishwa na za mgombea urais wa CHAUMMA, Salum Mwalimu (kazi 58), NLD, Ndugu Doyo Hassan Doyo (50), AAFP, Ndugu Kunje Ngombale Mwiru (24) na CUF, Bwana Gombo Simandito Gombo (23).

Uripoti wa sera kwa wagombea uchaguzi wa Urais wa Muungano



Uripoti wa sera za Samia kwenye vyombo vya habari ulijibainisha zaidi kwenye vyombo vya habari vyenye ufuasi mkubwa. *TBC Taifa* ilikuwa na uripoti wa juu kabisa (asilimia 6.7), ikifuatiwa na *Habari Leo* (asilimia 6.3) na *Fullshangwe Blog* (asilimia 6.3). Kwa upande mwingine, vyombo mbalimbali vya habari vilionesha uripoti wa chini: *Sengerema FM* (asilimia 0.7), *Jambo TV* (asilimia 0.7), *Tumbatu FM* (asilimia 0.4), *Mjini FM* (asilimia 0.4), na *Asam Online TV* (asilimia 0.4).

Kwa upande wa mgombea wa CHAUMMA, Ndugu Salum Mwalimu, uripoti wake ulijibainisha kwa kiasi kidogo kwenye vyombo vya habari ambapo *Clouds FM* ndio waliomripoti zaidi kwa asilimia 13.8 kwenye mitajo iliyohusu sera za wagombea, wakifuatiwa na *Dodoma FM* (asilimia12.1). Kinyume chake, vyombo mbalimbali vya habari vilikuwa na uripoti wa chini, kila kimoja kikichangia chini ya asilimia 2 ya mitajo yote iliyohusu sera. Hivi vinajumuisha *Radio One*, *Highlands FM*, *Jamii FM Radio*, *UFM*, *ITV*, na *Pambazuko* (kila kimoja kikiwa na asilimia 1.7).

Uripoti wa vyombo vya habari kuhusu Gombo, Kunje, na Doyo kwenye eneo la maudhui yanayohusu sera za wagombea, maudhui hayakugawanywa kwa usawa kwa vyombo vyote vya habari. *TBC Taifa* ndiyo iliyokuwa na uripoti wa hali ya juu zaidi ikiwa na asilimia 12.8 ya habari zote zilizohusu sera za wagombea. Kulikuwa na kundi la vyombo vya habari ambavyo vilionesha uripoti wa wastani, vikiwemo *UTV (Azam)* (asilimia 9.6), *Daily News* (asilimia 8.5), *Jamhuri na Clouds FM* (kila kimoja kikiwa na asilimia 6.4), na *Dodoma FM* (asilimia5.3). Kinyume chake, vyombo mbalimbali vya habari vilikuwa na uripoti wa chini, kila kimoja kikiwa na asilimia 1.1 ya maudhui yaliyohusu sera: *The Citizen*, *The Guardian*, *Highlands FM*, *TBC1*, *ZBC TV*, *Mwanahalisi Online*, *Ayo TV*, *Global TV Online*, *Michuzi Blog*, *na Pemba Today*. Uripoti usio wa usawa pia ulikuwa wazi kwenye vyombo vya habari vinavyomilikiwa na serikali. Maudhui ya sera za Samia yaliripotiwa kwenye kazi 84 zilizofanyiwa uchunguzi, ikilinganishwa na Doyo (13), Salum Mwalimu (9), Gombo (8), na Kunje (5). Hali kama hiyo pia inaonekana kwenye vyombo vya habari vya uchapishaji (Samia akiwa na kazi 87), Salum Mwalimu (23), Doyo (14), Gombo (10), na Kunje (6). Kwenye vyombo vya habari vya utangazaji, Samia (128), Salum Mwalimu (29), Doyo (27), Kunje (15), na Gombo (9). Kwenye vyombo vya habari vya mtandaoni, Samia aliongoza kwa kuwa na kazi 70, akifuatiwa na Doyo (9), Salum Mwalimu (6), Gombo (4), na Kunje (3).

Utekelezekaji wa programu na ahadi za wagombea

Wakati wa uchaguzi, vyombo vya habari vinatarajiwa kutekeleza jukumu la uangalizi (watchdog) ili kuhakikisha mchakato wa uchaguzi ni huru na wa haki. Njia mojawapo ya kutimiza jukumu hili la kidemokrasia ni kuchunguza kwa uhuru uwezekano wa utekelezaji wa programu na ahadi za wagombea, ikiwemo kama kuna rasilimali fedha za kutosha kutekeleza ahadi hizo na miradi wanayoipendekeza. Bila udhibiti huu, ahadi hewa na zisizo halisia zinaweza kuwapotosha wapiga kura wakati wa kampeni. Kama ilivyokuwa katika Uchaguzi Mkuu wa 2020, uripoti wa vyombo vya habari kuhusu uwezekano wa utekelezaji wa ahadi za wagombea uliendelea kubaki nyuma kwa kiasi kikubwa, ingawa kulikuwa na ongezeko dogo. Kwa ujumla, kazi 52 za habari (asilimia 14) viligusia kipengele hiki, vikiongezeka kutoka kazi 17 za habari mwaka 2025.

Uripoti wa kutekelezeka kwa ahadi za wagombea



Kwa Samia, sehemu kubwa ya maudhui hayakusema chochote kuhusu kutekelezeka kwa ahadi zake: Asilimia 90.3 ya kazi za kihabari zilizochambuliwa hazikugusa kabisa masuala ya kutekelezeka kwa kwa ahadi zake, huku asilimia 9.7 tu ndizo zilizochunguza jambo hilo. Kati ya kazi za kihabari zilizochunguza masuala ya kutekelezeka kwa ahadi za wagombea (n=37), kazi nyingi zilifanywa na vyombo binafsi vya habari (asilimia 78.4), wakati vile vya serikali vilifanya hivyo kwa asilimia 21.6 tu. Vyombo vya habari vya utangazaji ndivyo vilivyofanya vizuri kwenye eneo hili vikiripoti kwa asilimia 46, vikifuatiwa na vyombo vya habari vya mtandaoni (37.8%), na kwa kiwango cha chini, vyombo vya habari vya uchapishaji kwa asilimia 16.2.

Blogu ya Fullshangwe ndiyo iliyofanya vizuri zaidi kwenye eneo hili ikiwa na mitajo 11 (asilimia 29.7) iliyoripoti utekelezekaji wa sera za Samia. Nipashe na Arusha 1 FM (mitajo 3 kila kimoja, asilimia 8.1). Vyombo hivi viwili, pia vilikuwa na uripoti wa ujumla wa kipengele cha utekelezekaji wa ahadi na sera za wagombea ikilinganishwa na vyombo vingine vingi. *TBC Taifa*, *Radio Free Africa*, *ZBC Radio*, *TBC1*, *TM Timesmajira* (mitajo 2 kila kimoja, asilimia 5.4), wakati *Habari Leo*, *Raia Mwema*, *Jamhuri*, *Dodoma FM*, *Jamii FM Radio*, *UFM*, *ITV*, *UTV (Azam)*, *ZBC TV* na *Pemba Today* kila kimoja kikiwa na mtajo mmoja (1) sawa na asilmia 2.7.

Uripoti wa Salum Mwalimu ulitoa nafasi ndogo kwenye kipengele hiki ikishuhudiwa kwa asilimia 96.8 ya maudhui yaliyofanyiwa uchambuzi yakishindwa kugusia suala hilo. Ni asilimia 4 tu ya maudhui hayo yaligusia jambo hilo kwa sera na ahadi za Salum Mwalimu. Uripoti wote wa masuala yanayohusiana na utekelezekaji wa sera na ahadi za wagombea ulifanywa na vyombo binafsi vya habari (asilimia 100), huku kukiwa hakuna mchango wowote kutoka kwenye vyombo vya habari vinavyomilikiwa na serikali. Kwa msingi wa aina ya chombo cha habari, kipengele hiki kilijadiliwa zaidi kwenye vyombo vya habari vya uchapishaji kwa (asilimia 66.7), vikifuatiwa na vile vya utangazaji kwa asilimia 33.3, wakati vyombo vya habari vya mtandaoni havikugusa kabisa eneo hili.

Wakati Gombo akiwa hana habari iliyomgusa kwenye kipengele hiki, (Hapana kwa asilimia 100), Kunje alikuwa na asilimia 10.3 ya ahadi zake za kampeni kuripotiwa, ikiwa ni kiwango kikubwa kidogo ikilinganishwa na Samia na Salum Mwalimu, lakini ni cha chini ikilinganishwa na Doyo. Ahadi za kampeni za Doyo ziliripotiwa kuhusu kutekelezeka kwake kwa asilimia15.8, ikiwa ni kiwango cha juu zaidi kuliko wagombea wote. Kama ilivyokuwa kwa wagombea wengine wa upinzani, masuala yaliyohusu kutekelezeka kwa ahadi zao yaliripotiwa zaidi na vyombo binafsi vya habari (asilimia 88.9), wakati vyombo vya habari vya serikali vilichangia uripoti wa chini kwa asilimia 11.1.

UTV (Azam) ilijitokeza mwanzo kwa kuwa na mitajo 4 (asilimia 26.7), ikiashiria kwamba ndicho chombo kilichoripoti zaidi kuhusu utekelezekaji wa ahadi na sera za wagombea wa upinzani. *Raia Mwema na blogu ya Fullshangwe* kila kimoja kilikuwa na mitajo 2 (asilimia13.3), ikiashiria uripoti wa wastani. Vyombo vingine vyote vilivyobaki—*Mwananchi*, *Habari Leo*, *Nipashe*, *Clouds FM*, *Highlands FM*, *ITV*, *na Star TV*—kila kimoja kilikuwa na mtajo 1 (asilimia6.7).

Urejeleaji wa ilani za uchaguzi za vyama vya siasa

Urejeleaji wa ilani za uchaguzi za vyama vya siasa ulijitokeza katika idadi kubwa ya habari zilizowahusu wagombea. Kwa wagombea watano wa urais, kwa kiasi kikubwa uripoti wa vyombo vya habari ulirejelea ilani za vyama walivyokuwa wakiviwakilisha. Uripoti wa Samia ulijumuisha marejeo ya ilani ya chama chake katika habari 258 (asilimia 67.9), ilhali Salum Mwalimu, Gombo, Kunje na Doyo walipata viwango vya juu kidogo, wakipata uripoti wa kati ya asilimia 71.0 hadi 79.3, huku Kunje akiongoza kwa asilimia 79.3. Vyombo vya habari binafsi vilitawala uripoti kwa wagombea wote, vikichangia kati ya asilimia 71.7 (Samia) hadi 83 (Salum), wakati vyombo vya habari vya serikali vilichangia kwa kiwango kidogo, hususan kwa Salum (asilimia 17) na Doyo (asilimia18.6).

Urejeleaji wa ilani za uchaguzi

Wagombea urais wa muungano	Samia Suluhu Hassan	Salum Mwalimu	Gombo Samandito Gombo	Kunje Ngombale Mwiru	Doyo Hassan Doyo
					
Hapana	122 (32%)	19 (26%)	9 (29%)	6 (21%)	14 (25%)
Ndiyo	258 (68%)	53 (74%)	22 (71%)	23 (79%)	43 (75%)
Jumla*	380 (100%)	72 (100%)	31 (100%)	29 (100%)	57 (100%)
Umiliki wa vyombo vya habari					
Vya binafsi	185 (72%)	44 (83%)	16 (73%)	18 (78%)	35 (81%)
Vya Serikali	73 (28%)	9 (17%)	6 (27%)	5 (22%)	8 (19%)
Jumla	158 (100%)	53 (100%)	22 (100%)	23 (100%)	43 (100%)
Aina ya Chombo cha habari					
Vya uchapishaji	80 (31%)	22 (42%)	10 (45%)	4 (17%)	14 (33%)
Vya utangazaji	112 (43%)	25 (47%)	9 (41%)	16 (70%)	21 (49%)
Vya mtandaoni	66 (26%)	6 (11%)	3 (14%)	3 (13%)	8 (19%)
Jumla	258 (100)	53 (100%)	22 (100%)	23 (100%)	43 (100%)

*: Jumla ya habari zilizoripoti uchaguzi wa urais muungano.

Kwa Samia, vyombo vitatu vya habari vilichangia kwa wastani wa asilimia 19.4 ya uripoti uliorejelea ilani yake ya uchaguzi. *Habari Leo* (asilimia) walikuwa na mitajo 18, *TBC Taifa* (asilimia) sawa na mitajo 16 na blogu ya *Fullshangwe* () sawa na *TBC Taifa* kwa mitajo 16. Kinyume chake, vyombo 7 vya habari vilikuwa na uripoti wa chini kwenye eneo hili vikichangia chini ya asilimia 0.8 ya mitajo: *Sengerema FM*, *Pambazuko*, *Asam Online (asilimia)*, *na Zanzibar Mail*, *Mjini FM*, *Jambo TV*, *na Pemba Today* (asilimia 0.4).

Uripoti wa wagombea wa vyama vya upinzani

Kwa wagombea wa vyama vya upinzani, vyombo 9 vya habari vilijipambanua kwenye eneo hili vikichangia karibu asilimia 70 (69.2) ya uripoti wote uliorejelea ilani za uchaguzi za vyama vya hivyo. *Clouds FM* iliongoza kwa asilimia 10.8, ikifuatiwa na *TBC Taifa na UTV (Azam)* kwa asilimia 10 kila kimoja. Ikumbukwe kwamba kituo cha utangazaji cha serikali *(TBC Taifa)* kilikuwa na uripoti wa asilimia 10 kwa vyama vya upinzani, kikifanana na kituo kikubwa cha utangazaji cha binafsi, *UTV*. *Mwananchi Digital*, *Daily News*, *Nipashe*, *Raia Mwema*, *na Jamhuri* vyote vilichangia kwa asilimia 5. Vyombo vya habari vilivyokuwa na uripoti wa chini uliorejelea ilani za uchaguzi za vyama vya upinzani ni pamoja na *The Guardian*, *Highlands FM*, *TBC1*, *Mwanahalisi Online*, *Ayo TV*, *Pambazuko*, *Michuzi Blog*, *Pemba Today*, kila kimoja kikichangia kwa asilimia 0.8 ya kazi zote.

Mitazamo katika habari

Mitazamo mbali mbali ina dhima muhimu sana kwenye uripoti wa vyombo vya habari kwani hudokeza maoni yenye sura mbalimbali yanayomuunga mkono au kukinzana na mgombea, na hivyo kuchangia mtazamo mzuri kwa umma. Jinsi maoni chanya na hasi yanavyowasilishwa huweza hutambulisha kama chombo cha habari kimeripoti kwa usawa au kwa upendeleo. Uchambuzi wa uripoti wa vyombo vya habari unaonesha kutokuwepo kwa usawa kwa kiasi kikubwa, huku kukiwa na uripoti unaoegemea zaidi kwa mgombea urais wa chama tawala.

Mgombea urais wa CCM alipata uripoti chanya zaidi, akiwa na kazi 139 (asilimia 36.6) kati ya uripoti wote kwenye kipengele hiki. Takwimu hizi zinawakilisha ongezeko bayana kutoka asilimia 29 za uripoti chanya kwa mgombea wa CCM kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 (John Pombe Magufuli). Kwa sehemu kubwa, uripoti wa vyombo vya habari kwa Samia ulikuwa chanya. Kati ya kazi 380, kazi 139 (asilimia 36.6) zilikuwa na mtazamo uliomuunga mkono, huku kazi 9 (asilimia 1.6) tu ndizo zilizokuwa na maoni hasi dhidi yake. Hali hii inaonesha kwamba, Samia alipata upendeleo mkubwa kwenye uripoti wa vyombo vya habari achilia mbali maoni hasi machache yaliyotolewa dhidi yake. Mabadiliko kama haya katika tasnia ya Habari, siyo tu kwamba yanaakisi mabadiliko katika mwenendo wa mijadala ya kisiasa, bali pia huonesha kwamba, vyombo vya habari vinaweza kuunda simulizi kuhusu ugombea wa mgombea fulani, jambo ambalo linaweza likabadilisha mawazo ya wapiga kura na hatimaye kuamua kumpigia kura mgombea wa chama hicho.

Mtazamo kuhusu wagombea



Vyombo vitatu vya habari vimetawala uripoti unaomuunga mkono mgombea urais wa CCM vikichangia kwa asilimia 17.1 ya uripoti chanya wote. Vyombo hivyo ni Habari Leo (asilimia 5.8), TBC Taifa (asilimia5.8), na blogu ya Fullshangwe (asilimia 5.6). Vyombo sita vya habari vilikuwa na maudhui machache yaliyomuunga mkono Samia: *Sengerema FM* (asilimia 0.53), *Tumbatu FM* (asilimia 0.5), *Pemba Today* (asilimia 0.5), *Asam Online* (asilimia 0.5), *Zanzibar Mail* (asilimia 0.3), na *Mjini FM* (asilimia 0.3). Kwa upande mwingine, *TBC Taifa* (asilimia10.1) iliibuka kinara katika kuripoti maoni yaliyounga mkono mitazamo ya wagombea wa vyama vya upinzani, ikifuatiwa na *Dodoma FM* (asilimia 8.9), *Clouds FM* (asilimia 8.28), *Daily News* (asilimia 7.7), *UTV (Azam)* (asilimia7.7), *Jamhuri* (asilimia 6.5) na *Mwananchi Digital* (asilimia 5.9)

Haiba dhidi ya sera za wagombea (maudhui)

Utafiti huu pia ulichunguza uripoti wa vyombo vya habari kuhusu programu (sera) za wagombea na haiba zao wakati wa uchaguzi. Kimataifa, kuna mjadala unaoendelea kuhusu iwapo haiba ya mgombea inazidi uzito wa sera na maudhui ya msingi katika uripoti wa uchaguzi. Sawa na matokeo ya ripoti ya Uchaguzi Mkuu wa 2020, matokeo yanaonesha kuwa haiba za wagombea zilikuwa na mchango mdogo katika uripoti wa Uchaguzi Mkuu wa 2025.

Katika habari zilizowahusu wagombea urais wa Muungano, haiba za wagombea zilijitokeza katika matukio machache tu. Habari zilizomhusu Gombo zilikuwa na asilimia 3.2 ya maudhui yaliyohusu haiba yake, ikilinganishwa na asilimia 71 iliyojikita katika sera zake. Kwa Salum Mwalimu, uripoti wa haiba yake ulikuwa asilimia 2.8, wakati asilimia 80.6 ulihusu sera zake. Haiba ya Samia ilionekana katika asilimia 2.4 ya habari zote zilizomhusu, huku asilimia 81.3 ya habari hizo zikielezea sera zake. Kwa wagombea wengine, Kunje na Doyo, hakukuwa na habari zilizoripoti kuhusu haiba zao..

Uripoti wa masuala binafsi vs sera kwa wagombea Urais Muungano



UTV (Azam) ilisimama kama kinara katika kuripoti maudhui yanayohusu sera za viongozi wa upinzani ikiwa na asilimia 26.7, ikifuatiwa na *Raia Mwema* na *blogu ya Fullshangwe*, kila kimoja kikiwa na asilimia 13.3. kinyume chake, vyombo vingine vingi vilikuwa na uripoti wa chini kwenye kipengele hiki. Vyombo hivyo ambavyo kila kimoja kilichangia kwa asilimia 6.7 tu ni pamoja na *Mwananchi, Habari Leo, Nipashe, Clouds FM, Highlands FM, ITV, na Star TV*.

Ikilinganishwa na Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020, ambapo miito mingi kutoka makundi mbalimbali iliwataka wagombea kuzingatia sera zao – mfano ni kama vile matamko ya Jeshi la Polisi Tanzania, viongozi wa dini, na mashirika ya kitaifa yanayojihusisha na usimamizi wa uchaguzi, kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025, hali hiyo haikuwa na nafasi kubwa. Kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025, vyombo hivi vilisisitiza zaidi umuhimu wa kuheshimiana wakati wa kampeni. Ni sawa kabisa kusema kwamba, wagombea na vyombo vya habari vilijielekeza zaidi kwenye sera kuliko kwenye haiba za wagombea, jambo ambalo linafaa kuenziwa katika uripoti wa uchaguzi.

4.5.2 Uchaguzi wa rais wa Zanzibar: Uripoti wa wagombea wawili wenye ushawishi mkubwa

Uchaguzi mkuu wa rais wa Zanzibar ulikuwa ni mbio za farasi wawili. Kihistoria, ushindani ulikuwa baina ya CCM na CUF. Hata hivyo, tangu mwaka 2020, ushindani umegeuka na kuwa kati ya CCM dhidi ya ACT-Wazalendo. Mabadiliko haya ni matokeo ya kukimbia kwa viongozi wakuu na maelfu ya wanachama kutoka CUF akiwamo Katibu Mkuu wao na mgombea wa muda mrefu wa urais Maalim Seif Sharif Hamad, na kujiunga na ACT-Wazalendo. Utawala wa vyama viwili shindani huathiri namna vyombo vya habari vinayoripoti uchaguzi wa Zanzibar.

Kama ilivyobainishwa hapo juu, uchaguzi wa rais wa Zanzibar, ulikuwa ni uchaguzi wa pili kupata uripoti mkubwa wa vyombo vya habari, baada ya uchaguzi wa rais wa muungano. Jumla ya kazi 273 za kihabari ziliripoti kuhusu uchaguzi wa Zanzibar. Kwa ujumla, mgombea wa ACT-Wazalendo Othman Masoud Othman, aliripotiwa kwenye kazi 107 (asilimia 39.2), ikilinganishwa na mgombea urais wa CCM, Hussein Ali Mwinyi, aliyeonekana kwenye kazi 106 za kihabari sawa na asilimia 38.8. Wagombea wengine walipata asilimia 23.5 ya uripoti wa vyombo vya habari.

Ikichunguzwa kwa makini miongoni mwa aina za vyombo vya habari (vya uchapishaji, vya utangazaji, na vya mtandaoni), Mwinyi aliripotiwa zaidi na magazeti (asilimia 40.6) dhidi ya Othman Masoud Othman (asilimia 28.1), wakati Othman Masoud Othman akiripotiwa zaidi na vyombo vya habari vya mtandaoni (asilimia 32.7), ikilinganishwa na asilimia 22.64. Uripoti wa vyombo vya habari kwa pande zote mbili, Tanzania Bara na Zanzibar kwa wagombea hao wawili ni kama ulikuwa sawa. Vyombo vya habari vya Tanzania bara vilimripoti Mwinyi kwa asilimia 54.7 dhidi ya asilimia 57 za Othman Masoud Othman, vyombo vya habari vya Zanzibar vilimripoti Mwinyi kwa asilimia 45.3, ikilinganishwa na Othman Masoud Othman aliyepata asilimia 43.

Uripoti wagombea urais Zanzibar kulingana na makundi ya vyombo vya habari



Kama ilivyokuwa kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020, vyombo vya habari vya serikali vilitoa upendeleo wa moja kwa moja kwa mgombea urais wa CCM. Kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 mgombea kupitia CCM (Mwinyi) alipata wastani mzuri wa uripoti kwa asilimia 41.51 ya uripoti wote uliofanywa na vyombo vya habari vyenye mwelekeo wa kiserikali, ikilinganishwa na mshidani wake wa karibu kutoka chama cha ACT Wazalendo aliyepata asilimia 21.5 ya uripoti wa vyombo vya habari. Zanzibar Leo na redio ya *ZBC* viliongoza kwa kuwa na uripoti wa juu zaidi kwenye kampeni za Mwinyi ikiwa ni asilimia 9.4 na 7.6 mtawalia. Kama ilivyoelezwa hapo juu, uchaguzi wa Zanzibar ulikuwa ni suala la watu wa visiwani. Vyombo vyote vya habari vilivyokuwa na uripoti wa chini ya asilimia 1 kwa Mwinyi vilikuwa ni vyombo vya Tanzania bara: *Raia Mwema*, *Radio Free Africa*, *Radio One*, *Highlands FM*, *UFM*, *ITV*, *Star TV*, *The Chanzo*, *Global TV Online*, *blogu ya Fullshangwe*, *Jambo TV na TM Timesmajira*.

Utofauti huu katika uripoti unaleta maswali mengi na ya muhimu kuhusu upendeleo wa vyombo vya habari vya serikali na athari zake kwa mtazamo wa umma wakati wa mchakato wa uchaguzi. Tofauti kubwa katika uchambuzi na uwasilishaji wa kihabari unaonesha kwamba, mara nyingi, wapiga kura walikuwa wakipewa simulizi zenye mwelekeo wa kumuunga mkono Mwinyi (CCM) na kampeni zake, wakati kwa upande wa mgombea wa ACT-Wazalendo (Othman Masoud Othman), hali ilikuwa tofauti ambapo habari zake hazikuonekana sana.

Mambo kama haya yanaweza kuathiri siyo tu nafasi ya wapiga kura kuchagua, bali pia usawa na ushindani kwa ujumla wakati wa mchakato wa uchaguzi. Muundo huu unaakisi hali ilivyokuwa kwenye chaguzi zilizopita zikizua hoja kuhusu usawa katika uripoti unaofanywa na vyombo vya habari vya serikali, wakati wa mchakato wa uchaguzi na athari zake kwa hali ya kidemokrasia nchini.

Tathmini ya picha na habari zilizopewa kipaumbele

Mwinyi alipewa nafasi kubwa kwenye ukurasa wa mbele kama habari kuu mara 16. Kiwango hiki cha uangalizi kinazidi kwa kiasi kikubwa kile cha Othman Masoud Othman, ambaye alionekana kwenye ukurasa wa mbele kama habari kuu mara tatu tu. Tofauti hii ya uandishi inaashiria kuwepo kwa pengo kubwa katika mvuto wa umma au mwelekeo wa vyombo vya habari kati ya wawili hao. Mwelekeo huo pia unaonekana katika vyombo vya habari vya utangazaji, ambapo idadi ya mara wanavyojitokeza hutumika kama kiashiria kingine cha uangalizi wa vyombo vya habari. Matukio au kampeni za Mwinyi zilioneshwa mara 14 kama habari ya kwanza au kuu katika vipindi vya habari, ilhali Othman alionekana mara 8 katika nafasi hiyo. Kwa mantiki hiyo, Mwinyi si tu aliongoza katika vyombo vya habari vya kuchapisha bali pia aliendelea kuwa na uwepo mkubwa katika habari za utangazaji, jambo lililoimarisha nafasi yake mbele ya umma. Kwa kuwa Mwinyi alikuwa rais aliyeko madarakani wakati wa kampeni za uchaguzi, umaarufu huu unaweza pia kueleweka kutokana na mpangilio wa kiuongozi katika utoaji wa habari na vyombo vya habari.

Uripoti wa maudhui yaliyohusu sera

Uchambuzi wa uripoti wa vyombo vya habari na jinsi vilivyoripoti maudhui ya sera za wagombea urais kwenye uchaguzi wa Zanzibar, unaonesha uwepo wa usawa kati ya wagombea wakuu wawili, Othman na Mwinyi. Uripoti wa sera za Othman ulipata asilimia 76.7 ya uripoti wake wote kwenye vyombo vya habari, ilhali Mwinyi alipata asilimia 75.5 ya uripoti uliohusu sera zake. Hali inakuwa tofauti mno wakati inapochunguzwa namna vyombo vya habari vya serikali (vya uchapishaji, vya utangazaji na vya mtandaoni) vinavyoripoti.

Uripoti wa vyombo vya habari vya serikali unaonesha kwamba maudhui ya sera za Mwinyi yalipata uripoti wa asilimia 45, ambayo inatofautiana na ya Othman aliyepata asilimia 25.3. Pengo hili linaonesha upendeleo unaoweza kubainika wazi kwenye vyombo vya habari vya serikali na namna vinavyoegemea upande unaompendelea Mwinyi. Kwenye vyombo vya habari vya uchapishaji, utofauti huo uliendelea vile vile: Mwinyi alipata asilimia 38.8 ya uripoti wa sera zake, ikilinganishwa na Othman, aliyepata asilimia 25.3. Hali hii inaashiria kwamba vyombo vya habari vya uchapishaji viliegemea zaidi kwenye uripoti wa sera zilizokuwa zikinadiwa na Mwinyi, na hivyo, kuonesha wazi kwamba mtazamo wa vyombo vya habari haukuwa sawa katika uripoti wake kwani ulimpendelea zaidi Mwinyi (CCM).

Kinyume chake, hali ya uripoti wa vyombo vya habari vya mtandaoni vilitoa picha tofauti kabisa. Kwa upande huu, maudhui yaliyohusu sera za Othman yalipewa uzito zaidi vikiripoti kwa asilimia 36.7, yakiyazidi maudhui yaliyoripoti sera za Mwinyi aliyepata asilimia 23.8. Hali hii inadhihirisha kwamba, wakati vyombo asilia vya habari vinaegemea upande wa Mwinyi, majukwaa ya mtandaoni yanatoa fursa kwa mitazamo mbalimbali, vikimpatia Othman nafasi ya kusikika zaidi kwenye ulimwengu wa kidijitali.

Uripoti wa sera kwa wagombea



Ikilinganishwa na Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 ambapo vyombo vya habari vilimpendelea zaidi mgombea wa CCM Mwinyi (kwa asilimia 46 ya habari zote zilizoripoti maudhui ya sera za wagombea), ikilinganishwa na mgombea wa ACT-Wazalendo Hamad (asilimia 28), kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025, uripoti wa vyombo vya habari katika eneo hili kwa namna fulani uliimarika zaidi. Maendeleo haya kwa namna fulani yanaweza yakahusishwa na uamuzi wa kuvihusisha vyombo vya habari vya mtandaoni kwenye utafiti wa mwaka 2025, jambo ambalo halikufanyika kwenye utafiti wa mwaka 2020.

Haiba dhidi ya sera

Sawa na ilivyokuwa kwa wagombea wa urais wa muungano kama ilivyojadiliwa hapo juu, uripoti wa vyombo vya habari vya Zanzibar kuhusu wagombea urais wa Zanzibar, ulijielekeza kwenye sera za wagombea. Uchambuzi umebaini kwamba Othman alipata asilimia 82.2 ya uripoti kuhusu sera zake, ilhali Mwinyi alipata asilimia 80.2. Haiba ya wagombea haikupewa nafasi sana na ilikuwa na asilimia chini ya 3 kwa uripoti wa kila mgombea. Mwaka 2020, kulikuwa na habari 12 (asilimia 5) ambazo zilijikita katika haiba ya Mwinyi wakati kwa Sharif Hamad kulikuwa na habari 5 (asilimia 3).

Uripoti wa masuala binafsi vs sera kwa wagombea Urais Zanzibar



Mitazamo mbalimbali kuhusu wagombea

Uripoti wa Mwinyi ulikuwa na maoni mengi ambayo ni chanya kwa asilimia 39.6 ya habari zote kuhusu yeye kama mgombea. Kinyume chake, Othman alipata asilimia 22.4 tu ya mitazamo chanya kuhusu yeye. Maoni hasi yalionekana kwa nadra sana yakimuelezea mgombea ambapo Mwinyi alikuwa na asilimia 0 na Othman akiwa na asilimia 0.9. Takwimu hizi zinaashiria kushuka kutoka asilimia 3 za Mwinyi mwaka 2020 na asilimia 4 za mgombea urais wa ACT-Wazalendo Seif Sharif Hamad kwenye kipindi hicho hicho cha uchaguzi.

Mitazamo kuhusu wagombea urais Zanzibar

Mitazamo inayounga mkono na isiyounga mkono kutokana na vyombo vya habari vya Serikali, binasfi, vya uchapishaji, vya utangazaji na mtandaoni





Dr Hussein Ali Mwinyi (n=106)

Othman Masoud Othman (n=107)

Mitazamo iliyomuunga mkono	42 (39.62)	24 (22.43)
Mitazamo isiyomuunga mkono	0 (0)	1 (0.93)

4.5.3 Tathmini ya wagombea ubunge na vyama vyao vya siasa

Uchaguzi wa wabunge uliripotiwa kwenye kazi 332 za kihabari. Kati ya kazi hizo, kazi 274 (asilimia 82.5) zilimlenga mgombea mmoja mmoja, wakati kazi 58 (asilimia 17.5) zilijumuisha wagombea wawili au zaidi. Mwenendo huu unatofautiana na jinsi ilivyokuwa kwenye chaguzi zilizopita ambapo ni asilimia 64 tu ya uripoti wa vyombo vya habari ulihusisha mgombea mmoja, wakati asilimia 24 ukihusisha wagombea wawili au zaidi. Kwa upande wa aina ya chombo cha habari, vyombo vya habari vya uchapishaji viliripoti wagombea wawili au zaidi kwa asilimia 20 ikilinganishwa na vyombo vya habari vya utangazaji (asilimia 18). Utofauti kati ya vyombo vya habari vya serikali na vile vya binafsi haukuwa mkubwa sana, ambapo vyombo vya habari vya serikali viliripoti kuhusu wagombea wawili au zaidi kwa asilimia18 ya uripoti wao, ikilinganishwa na vyombo binafsi vya habari vilivyokuwa na asilimia 17. Hali hii inamaanisha kwamba wananchi walikuwa na taarifa chache kuhusu wagombea, hali ambayo ingewawezesha kufanya uamuzi sahihi wakati wa uchaguzi. Uwasilishaji wa mitazamo kinzani kutoka kwa wagombea mbalimbali ni jambo muhimu katika kuwafanya wananchi wawe na ufahamu wa kutosha. Bahati mbaya zaidi, jambo hili halikufanyika vizuri.

Wakati idadi ya habari zilizohusu wagombea ubunge zilikuwa 332, idadi ya wagombea ubunge waliotajwa kwenye habari hizo ilikuwa 416. Hii inamaanisha kwamba kwenye habari moja iliyohusu uchaguzi wa wabunge, kuliripotiwa mgombea zaidi ya mmoja. Kwa kuzingatia takwimu hizi (416), CCM waliripotiwa kwa asilimia 56, wakifuatiwa na ACT-Wazalendo (asilimia 15.1), CHAUMMA (asilimia 9.6), CUF (asilimia 3.9), NLD (asilimia 2.9), na vyama vingine vilivyosalia (asilimia 12.5). Uripoti wa CCM ulishuka kidogo kwa asilimia 2 ikilinganishwa na uripoti wa wabunge kwa mwaka 2020, badiliko ambalo siyo kubwa sana.

Uripoti wa vyama uchaguzi wa Bunge



Kwa ujumla, uripoti uliofanywa na vyombo vya habari vinavyomilikiwa na serikali kwa wagombea wa CCM ulikuwa asilimia 66.2. Vile vile CCM ilijitokeza zaidi kwenye uripoti wa aina mbalimbali za vyombo vya Habari vya uchapishaji (asilimia 68.1), vya utangazaji (asilimia 42.1), na vya mtandaoni (asilimia 67.4). Kwa kuangalia uripoti wa chombo kimoja kimoja cha habari kwa wagombea wa CCM na wa vyama vya upinzani, CCM iliripotiwa zaidi na *Michuzi Blog* (asilimia 8.6), *Habari Leo* (asilimia 6.4), *Daily News* (asilimia 6.01), ilhali *Global TV Online na TM Timesmajira*, kila kimoja kikiwa na asilimia 5.6. Kwa upande mwingine, *UFM* (asilimia 8.7), *Jamii FM Radio* (asilimia 8.2), *Sengerema FM* (asilimia 6.6), *Highlands FM* (asilimia 5.5), ilhali *Habari Leo*, *Uvinza Community FM*, *na Mwananchi Digital*, kila kimoja kikiwa na asilimia 4.9, viliripoti zaidi kuhusu vyama vya upinzani. Habari Leo, ambalo ni gazeti la serikali, lilionekana kuripoti kuhusu wagombea wa CCM na wagombea wa vyama vya upinzani kwa usawa.

Haiba za Wagombea

IKatika uripoti wa uchaguzi wa wabunge, tulibaini kwamba, haiba ya wagombea ilikuwa na nafasi ndogo kwenye uripoti wa vyombo vya habari. Zilitajwa kwa asilimia chini ya moja (asilimia 0.9) ya uripoti wote wa wagombea ubunge. Kinyume chake, asilimia 83 ya uripoti huo ulijikita kwenye masuala ya sera za wagombea, ukiashiria kwamba vyombo vya Habari, na waandishi wa habari walijikita zaidi kwenye masuala ya msingi yaliyoletwa na wagombea, jambo ambalo ni la muhimu sana kwenye uripoti wa uchaguzi.

4.5.4 Uchaguzi wa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar

Uchaguzi wa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar haukupewa nafasi kubwa kwenye uripoti wa uchaguzi ukiwa na habari 73 tu kati ya habari zote zilizohuzu uchaguzi wa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, ikiwa ni uripoti wa chini ikilinganishwa na habari 75 mwaka 2020. Uchaguzi wa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar uliripotiwa zaidi na vyombo vya habari vya Zanzibar.

Uripoti wa vyama uchaguzi Baraza la Wawakilishi



Uhusiano wa vyama vya wagombea na uripoti wao

Kati ya wagombea 81 waliotajwa kwenye habari 73, CCM ilitajwa mara 57 ikiwa ni sawa na asilimia 70.4 ya kazi zote. Kwa ulinganisho, ACT-Wazalendo walipata mitajo 9 sawa na asilimia 11.1, huku vyama vingine vilivyosalia vikipata mitajo 15 ambayo ni sawa na asilimia 18.5. Tofauti na ilivyokuwa kwenye uchaguzi wa Bunge, ambako CCM ilipata asilimia 56 (angalia hapo juu sehemu inayohusu Wagombea Ubunge), uchaguzi wa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar ulikuwa na uripoti mkubwa zaidi. Uripoti huu mkubwa unahusishwa na uripoti wa kina wa vyombo vya habari vya serikali vikiwemo *Zanzibar Leo*, *ZBC TV*, *na Redio ZBC* ambavyo kwa pamoja, vilikuwa na uripoti wa asilimia 45.6 ya uripoti wote uliohusu uchaguzi wa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

Uripoti wa vyama vikuu viwili kule visiwani unaonyesha mwelekeo unaovutia sana. Wagombea kutoka Chama Cha Mpainduzi (CCM) waliripotiwa sana na vyombo mbalimbali vya habari: *Zanzibar Leo* walikuwa na asilimia 21.1 ya uripoti, *ZBC TV* walifanya hivyo kwa asilimia 15.8, *Pemba Today* kwa asilimia 12.3, *Asam Online* kwa asilimia 10.5, na *ZBC Radio* kwa asilimia 8.8. Kinyume chake, chama kikuu cha upinzani, ACT-Wazalendo, kiliripotiwa zaidi na *Pemba Today*, ambao walikuwa na asilimia 33.3 ya uripoti wake, na *Micheweni FM*, ambayo ilikuwa na asilimia 20.8. Kwa pamoja, vyombo hivi viwili vya habari vilichangia zaidi ya nusu ya uripoti wote uliohusu ACT-Wazalendo (asilimia 54.2). Vyombo hivi vya habari viko Pemba, eneo linalojulikana kama ngome ya ACT-Wazalendo. Zaidi ya hayo, chombo cha habari kinachomilikiwa na serikali, *Zanzibar Leo* kilitumia asilimia 12.5 ya uripoti wake kuripoti kuhusu ACT-Wazalendo.

Jinsi za wagombea

Kwenye uripoti wa uchaguzi wa wagombea wa ujumbe wa Baraza la Wawakilishi , asilimia 78.4 ya kazi zilizofanyiwa uchambuzi ziliwataja wagombea wanaume na asilimia 21.6 ziliwataja wagombea wanawake. Pemba Today liliripoti zaidi kuhusu wanawake (asilimia 52.6), wakati *Micheweni FM na Zanzibar Leo* wakifanya hivyo hivyo kwa asilimia 15.79 na 10.5, mtawalia.

Haiba dhidi ya sera za mgombea

Haiba za wagombea hayakuwa na nafasi kubwa kwenye uchaguzi wa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Sehemu kubwa ya uripoti (asilimia 81.8) ilikuwa kwenye eneo la “uripoti zaidi wa sera” za wagombea. Ni asilimia 2.3 tu ya habari ndizo zilizokuwa kwenye “uripoti wa haiba za wagombea”. Kama ilivyokuwa kwenye uchaguzi wa wabunge, vyombo vya habari na waandishi wa habari walijielekeza zaidi kwenye masuala ya sera za wagombea badala ya haiba zao

4.5.5 Tathmini ya wagombea udiwani

Masuala ya wagombea udiwani, wakiwamo wagombea wenyewe, yaliripotiwa kwenye habari 83 tu. CCM ilitajwa kwenye habari 59 sawa na asilimia 71.1, ACT-Wazalendo kwenye kazi 13 (asilimia 15.6), na vyama vilivyosalia vilitajwa kwenye kazi 11 (asilimia 13.3). Kama ilivyokuwa kwenye uchaguzi wa rais na wabunge kama ilivyojadiliwa hapo juu, hakukukuwa na uwiano katika uripoti wa chama tawala, (CCM) ikilinganishwa na vile vya upinzani.

Uripoti wa uchaguzi wa udiwani

Magazeti



Redio na TV



Vyombo vya Mtandaoni



4.6 Uripoti kwa mada

Utafiti huu ulichunguza mada kuu mbili: masuala yahusianayo na uchaguzi na maeneo muhimu ambayo kampeni zililenga. Mada za uchaguzi zilihusu vipindi kabla ya uchaguzi, siku ya uchaguzi na baada ya uchaguzi. Kinyume chake, ilikuwa ni masuala yaliyoibuliwa na wagombea wakati wa kampeni zao, kama ambavyo yalionekana muhimu kwa wapiga kura. Masuala kumi bora yaliyoibuka yalikuwa kama ifuatavyo: Amani na utulivu, kilimo na mifugo, misitu na uvuvi, mawasiliano ya simu na miundombinu, masuala ya afya, elimu, biashara, uchumi na fedha, jinsia na masuala ya familia, ulinzi na usalama wa taifa, utawala bora na uwajibikaji, na maji na usafi wa mazingira.

Kinyume chake, ni kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020, ambapo wagombea walijadili mada kama vile maji na usafi wa mazingira, afya, mazingira, mabadiliko ya tabia nchi, elimu, katiba mpya, sayansi, teknolojia, ubunifu, kazi, kukosa ajira, miundombinu, na mawasiliano ya simu, Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 uliweka msisitizo mkubwa kwenye amani na utulivu. Kwenye kipindi hiki cha uchaguzi, vyama vya siasa, wagombea, vyombo vinavyosimamia uchaguzi, vyombo vya ulinzi, na viongozi wa dini, wote walisisitiza umuhimu wa wa amani na utulivu.

4.6.1 Mada za uchaguzi

Kampeni za uchaguzi na uhamasishaji kujitokeza kupiga kura ndio mada zilokuwa muhimu zaidi zikiwa na asilimia 55.5 ya mitajo yote kwenye uripoti wa uchaguzi. Mada nyingine muhimu zilijumuisha ushirikishwaji wa wadau, elimu kwa mpiga kura, upigaji kura, na uhesabu wa kura na taratibu za ulinzi, ambazo zilipata mitajo kati ya asilimia 6 na 3 na 6 mtawalia. Hii ilisisitiza umuhimu wa masuala haya nyakati za uchaguzi.

5.0 MITAZAMO YA WADAU KUHUSU UCHAGUZI MKUU WA TANZANIA WA MWAKA 2025

Sehemu hii inawasilisha uchambuzi usio wa namba kwa kuzingatia mada kwa mahojiano yaliyofanyika kwa wadau muhimu waliokuwa kwenye mnyororo wa uchaguzi mkuu wa mwaka 2025, wakiwamo waandishi wa habari, wahariri, mameneja wa vyombo vya habari, wadhibiti, vyama vya kiraia, na wawakilishi wa vyama vya siasa. Madhumuni ya uchambuzi huu, ilikuwa ni kuchunguza namna vyombo vya habari vilivyotekeleza wajibu wao wa kidemokrasia wa kuhabarisha umma, kuwezesha mijadala, na kuchunguza michakato ya uchaguzi, huku vikibainisha sababu za kimuundo na kimuktadha, zilizosababisha aina ya uripoti wa vyombo vya habari kuwa kama ulivyokuwa wakati wa uchaguzi.

Kwa mtazamo wa wadau wote, vyombo vya habari vilichukuliwa kama nguzo muhimu ya utendaji wa kidemokrasia, vikitarajiwa kutoa taarifa sahihi, kuhakikisha uripoti wenye usawa miongoni mwa wadau wote wa kisiasa, na kuwawezesha wananchi kufanya maamuzi sahihi wakati wa kuchagua viongozi wao.

Wakati waandishi wa habari wakiendelea kuripoti kuhusu habari za maendeleo kwenye kampeni na michakato mingine ya uchaguzi, mahojiano yaliyofanyika yanabainisha kwamba, uripoti wa vyombo vya habari ulikuwa ukifanyika katika mazingira magumu yakijipambanua kwa kuwa na udhibiti wa hali ya juu, misukumo ya kiuchumi, masuala ya kiusalama, na misukosuko ya kiteknolojia. Masuala yote haya yaliathiri sio tu habari zilizoripotiwa bali pia hata jinsi habari hizo zilivyoripotiwa.

Matokeo ya utafiti yanaonesha ustahimilivu wa watendaji wa vyombo vya habari, wengi wao wakiwa ni wataalamu wenye weledi wa kiutendaji licha ya kufanya kazi kwenye mazingira magumu. matokeo ya utafiti yanabainisha vikwazo vya kimuundo, ambavyo viliathiri uamuzi wa kiuhariri na hivyo kuufinya wigo wa aina fulani za uripoti, hasa uandishi wa habari za kiuchunguzi na uwajibikaji.

Uchaguzi pia umeonesha kukua kwa hali ya kutegemeana kati ya uandishi wa habari na miundombinu ya kidijitali, kwani pale zilipojitokeza changamoto za kiteknolojia, ziliathiri mchakato wa uzalishaji wa maudhui na hata uwezo wa hadhira kupata taarifa. Utegemeano huu unaakisi mwelekeo mkubwa kwenye mageuzi ya vyombo vya habari duniani, huku ukidokeza udhaifu uliomo ndani yake. Mara zote hoja za wadau zimekuwa zikisisitiza kwamba, utendaji wa vyombo vya habari hauwezi kueleweka, ikiwa utatengwa na muktadha wa kisiasa na kitaasisi ambamo kwamo chombo hicho kinafanyia kazi zake. Mtazamo wa mamlaka ya udhibiti, uhalali wa kiuchaguzi, na imani ya

umma kwa pamoja huathiri namna uripoti wa vyombo vya habari unavyofanyika na unavyotafsiriwa.

Mada zinazofuata zinachanganua mitazamo hii ili kutoa taarifa kamili ya jinsi vyombo vya habari vilvyofanya uripoti wake wakati wa uchaguzi. Kila mada inachnguza kipengele mahsusi cha mazingira ya vyombo vya habari huku ikitambua mahusiano ya muundo, uchumi na sababu za kisiasa.

Vikichukuliwa kwa pamoja uchambuzi, unatoa picha siyo tu kwa changamoto zilizojitokeza wakati wa uchaguzi wa mwaka 2025, lakini pia kwenye fursa zitakazoimarisha mfumo wa vyombo vya habari kwenye chaguzi zijazo. Kwa kuyashughulikia masuala yote ya kimfumo yaliyobainishwa, wadau wanaweza kusaidia kutengeneza mazingira wezeshi kwa uandishi wa habari uliohuru na jumuishi.

5.1 Uhuru wa vyombo vya habari na uhuru wa kiuhariri

Uhuru wa vyombo vya habari kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 ulifafanuliwa kwa upana kuwa ulikuwepo lakini ulikuwa ukifanya kazi ndani ya mazingira yanayokidhi vigezo vya kitaasisi. Waandishi wa habari waliendelea kuripoti matukio ya kampeni, kuchapisha habari na kuandaa mijadala ya kisiasa. Hii ilionyesha kwamba vyombo vya habari bado viko hai kipindi chote cha mchakato wa uchaguzi. Hata hivyo, wadau wameendelea kusisitiza kwamba uamuzi wa kiuhariri uliathiriwa na matarajio ya kiudhibiti na mazingira ya tahadhari kwa ujumla wake.
Mifumo ya kisheria ilikuwa na jukumu kubwa la kubainisha mazingira ya kufanyia kazi kwa vyombo vya habari. Mchakato wa upatikanaji wa leseni, mahitaji ya kufuata sheria, na ufuatiliaji wa maudhui yanayoripotiwa yalionekana kama namna ya kuhimiza uzingatiaji wa viwango vya kitaaluma na kiweledi na kuhakikisha kunakuwepo usawa kwenye uripoti. Wakati baadhi ya wadau waliona hizi kama hatua muhimu, wengine wanaona kama ni udhibiti wa aina yake kwenye mazingira ya uripoti wa uchaguzi hasa linapokuja suala la uripoti wa maudhui nyeti yenye mtazamo wa kisiasa.

Uhuru wa vyombo vya habari wakati wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 ulikuwa kwenye mazingira ambayo yamedhibitiwa yanayobadilika badilika. Waandishi wa habari waliripoti wakiwa katika eneo walimopaswa kuzingatia mifumo ya kisheria na kiudhibiti kwa wakati mmoja iliyoambatana na vikwazo zaidi, ambavyo kwa namna moja au nyingine, viliathiri uamuzi wa kiuhariri. Uwepo wa majukwaa ya kidijitali yaliyafanya mazingira haya kuwa magumu zaidi, kwani yaliongeza idadi ya wadau wanaohusika kwenye mnyororo wa uzalishaji wa taarifa. Mmoja wa wahojiwa kutoka Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), alisema yafuatayo wakati wa mahojiano: “tofauti na utangazaji wa zamani, majukwaa ya mitandao ya kijamii yanaruhusu kila mwananchi kuwa mzalisha maudhui au ‘mwandishi wa habari’, na mara nyingi wakiwa hawajapata mafunzo ya kiutaalamu na kiweledi au kuwa na nyenzo za uwajibikaji”.

Taarifa kama hizi zinaonesha ugumu unaoongezeka kwenye mazingira ya vyombo vya habari ambamo uandishi wa habari wa kitaaluma unafanya kazi, sambamba na mtiririko wa taarifa usio na usimamizi. Kupanuka kwa ushiriki wa kidijitali kumeongeza kasi ya mzunguko wa taarifa, lakini pia, kumeongeza shinikizo kwa vyomba vya habari katika kuimarisha usahihi na kuaminika kwake kwenye mazingira yanayobadilika kwa kasi sana.

Mifumo ya umiliki wa vyombo vya habari pia kwa namna fulani ilichangia kuathiri uhuru wa uhariri. Mashirika ya vyombo vya habari yenye uhusiano na umma, yalifanya kazi ndani ya mamlaka ya kisiasa, inayoendana na mifumo rasmi ya mawasiliano, wakati vyombo binafsi vya habari vikiweka uzani sawa kati ya uhuru wa kitaaluma na kitaalamu dhidi ya masuala ya kibiashara.

Uimara wa kiuchumi ulikuwa ni kigezo muhimu cha kujiamini kwa wahariri. Mara nyingi vyombo vya habari vilivyotegemea mapato yaliyotokana na matangazo ya biashara, vilikuwa makini zaidi kwenye uripoti wake, hali inayoakisi mwingiliano uliopo kati ya uimara wa kifedha na kuzikabili hatari za kiuandishi wa habari. Uhusiano huu unaonesha umuhimu wa kuzingatia vigezo vya kiuchumi wakati wa kutathmini uhuru wa vyombo vya habari.

Ulinganisho wa kihistoria ulijibainisha katika hoja zilizokuwa zinatolewa na wadau. Waandishi wa habari wenye uzoefu wa kutosha wa kuripoti chaguzi kadhaa huko nyuma, waliyaelezea mazingira ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 kama ni mazingira yaliyokuwa na vikwazo vingi kuliko kipindi kilichopita, wakitafsiri kwamba yaliubana uhuru wa uhariri. Tafakari kama hizi zinaonesha nafasi ya kumbukumbu za kitaasisi katika kutengeneza matarajio ya vyombo vya habari.

Licha ya vikwazo hivi, wadau wanakiri kwamba waandishi wa habari waliendelea kutekeleza majukumu yao muhimu ya kuripoti matukio ya kisiasa na michakato ya kiuchaguzi. Hii inaonesha kwamba kuna ustahimilivu wa sekta ya vyombo vya habari na dhamira yake katika kutoa huduma kwa umma hata ikiwa kwenye mazingira magumu.

Vile vile, mada/dhamira inaonyesha kwamba mtazamo wa uhuru ni muhimu kama ilivyo muhimu kwa ulinzi rasmi wa kisheria. Waandishi wa habari wanapojiona wako kwenye vikwazo, hata kama si moja kwa moja, kwa namna fulani inaathiri jinsi wanavyoripoti hata mawanda ya uripoti wao, na hivyo kuleta taswira tofauti kwa umma kuhusu kuaminika kwa vyombo vya habari.

Kwa ujumla, uhuru wa vyombo vya habari wakati wa uchaguzi unaweza kuelezwa kama ni wa kimakubaliano na si uhuru kamili. Kuimarishwa kwa uhuru wa vyombo vya habari kwenye chaguzi zinaokuja kutahitaji kuzishughulikia kwa uwazi hoja za kiudhibiti, uchumi endelevu, na kuaminiana kitaasisi, ili kupanua nafasi kwa uandishi wa habari ulio thabiti.

5.2 Hofu, vitisho, na udhibiti binafsi

Hofu na hali ya kutokujihisi salama zilikuwa mkondo muhimu ulioathiri namna vyombo vya habari vilivyofanya kazi wakati wa kipindi cha uchaguzi. Waandishi wa habari waliokuwa wakiripoti mikutano ya kampeni, maandamano, na matukio ya baada ya uchaguzi walieleza kuwa walifanya kazi katika mazingira ambayo masuala ya usalama binafsi yaliathiri maamuzi yao ya kitaaluma. Uelewa huu wa hatari uliathiri si tu uandishi wa habari wa uwanjani bali pia mipango ya vyombo vya habari.

Ripoti za vurugu, unyanyasaji, na vitisho dhidi ya waandishi wa habari, ziliunda mazingira mapana ya tahadhari. Hata pale ambapo matukio yalikuwa ya eneo fulani tu, yalikuwa na athari ya kisaikolojia katika taaluma nzima, yakiongeza hisia ya kuwa katika hatari miongoni mwa wanahabari. Uzoefu huu unaonesha jinsi usalama na ulinzi wa waandishi wa habari na wafanyakazi wa vyombo vya habari, unavyoweza kuathiri uandishi wa habari hata nje ya muktadha wa matukio ya moja kwa moja.

Kujidhibiti katika uandishi wa habari (self-censorship) kuliibuka kama mwitikio wa kawaida wa kukabiliana na mazingira yaliyokuwepo. Badala ya kuwepo kwa vikwazo vya moja kwa moja, waandishi wa habari walieleza uwepo wa michakato ya ndani ya kutathmini madhara yanayoweza kujitokeza kutokana na kuchapisha taarifa nyeti. Tafakari hizi mara nyingi zilihusisha kusawazisha maslahi ya umma dhidi ya hofu ya usalama binafsi na uthabiti wa taasisi wanazofanyia kazi. Hivyo basi, tahadhari ya kiuhariri haikutokana tu na shinikizo la nje, bali pia na uamuzi wa kitaaluma ulioundwa na muktadha husika. Hali hii inaonesha jinsi mazingira ya kimuundo yanavyoweza kuathiri kwa njia isiyo ya moja kwa moja uandishi wa habari, kwa kubadilisha kile kinachoripotiwa na namna kinavyowasilishwa.

Madhara ya kisaikolojia ya kufanya kazi katika mazingira yenye msongo yalidhihirika pia. Waandishi wa habari waliripoti uchovu, msongo wa mawazo, na mzigo wa kihisia kutokana na kuripoti matukio yenye mvutano wa kisiasa. Uzoefu huu unaonesha umuhimu wa kutambua afya ya akili kama sehemu muhimu ya usalama wa waandishi wa habari. Vyombo vya habari vilijibu kwa njia tofauti, ambapo baadhi vilianzisha taratibu za usalama, huku vingine vikitegemea mitandao isiyo rasmi ya msaada. Tofauti hizi za mwitikio zinaakisi pengo la rasilimali za taasisi na kiwango cha maandalizi kilichopo.

Wadau kwa ujumla walikubaliana kwamba kuimarisha mifumo ya ulinzi ni muhimu ili kuhakikisha kuwa hofu haidhoofishi uhuru wa uandishi wa habari. Mifumo ya usalama, mafunzo, na uratibu na mamlaka husika vilitambuliwa kama maeneo yanayohitaji kupewa kipaumbele. Hivyo basi, mada hii inaonesha kuwa hofu na kujidhibiti katika uandishi wa habari havikuwa mambo ya pembeni, bali yalikuwa kiini cha kuelewa mwenendo wa vyombo vya habari wakati wa uchaguzi. Kushughulikia masuala haya kutakuwa muhimu katika kujenga mazingira ya vyombo vya habari yaliyo imara zaidi na yenye kujiamini katika siku zijazo.

5.3 Kutokuwepo usawa kisiasa na mwonekano wa vyama

Coverage patterns during the 2025 General Mifumo ya uripoti wakati wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 inaakisi tofauti muhimu katika mwonekano wa washiriki wakuu wa kisiasa kwenye majukwaa ya vyombo vya habari. Wadau waliona kwa upana kwamba vyama vyenye uwezo mkubwa wa kifedha na kitaasisi vilijihakikishia uwepo wake kwenye mazingira ya vyombo vya habari. Washiriki hawa walinufaika kutokana na kuwa na ratiba za kampeni zilizopangwa vizuri, uratibu mzuri wa kilojistiki na uwezo wa kushirikiana na vyombo vya habari mara kwa mara jambo ambalo linatafsiriwa kama viwango vya juu vya kutambulika.

Kwa ujumla, taasisi za kihabari zilielezea wajibu wao katika kuhakikisha kwamba vinatoa nafasi kwa usawa kwenye fursa za uripoti na muda wa hewani. Hata hivyo, hali halisi za kimuundo ziliathiri namna dhumuni hili lilivyoweza kutekelezwa katika hali halisi ya kiutendaji. Utofauti katika namna vyama vilivyokuwa vimejiandaa, mikakati ya kimawasiliano na mwitikio kwenye mialiko ya mahojiano viliathiri ukubwa wa uripoti pamoja na kina cha uripoti. Matokeo yake, mara kwa mara palikuwa na utofauti katika uripoti uliosababishwa zaidi na uwezo wa kuifikia fursa na ushirikishaji kuliko upendeleo wa chombo cha habari. Moja ya wahariri wakuu alisema: “kwenye mazingira mengine, wagombea wenyewe walikuwa hawafahamiki vizuri, hali iliyosababisha ugumu hata kwenye kufanya nao mahojiano. Baadhi ya vyama shiriki havikuwa vinafahamika kwa wandishi wa habari na kwa jamii”.

Matangazo pia yalichangia kuimarisha pengo la mwonekano. Wanasiasa wenye rasilimali kubwa za kifedha waliweza kununua nafasi za matangazo na kufadhili maudhui yanayohusiana na kampeni, hivyo kuongeza umaarufu na wasifu wao katika vyombo vya utangazaji na vya kuchapisha. Ingawa vyombo vya habari vilidumisha utenganisho rasmi kati ya maudhui ya uhariri na yale ya kibiashara, uwepo wa jumla wa vyama vyenye ufadhili mkubwa uliendelea kuongezeka kutokana na uwekezaji huu. Mhariri mmoja alisema wakati wa mahojiano: “Uwezo wa kifedha ulikuwa na mchango mkubwa. Chama tawala, CCM, kilikuwa kimejipanga vizuri kifedha na kilikuwa na rasilimali za kuwezesha usafiri na upatikanaji wa waandishi wa habari. Kinyume chake, vyama vingine vingi vilikosa uwezo huo... na vyombo vingi vya habari vyenyewe vilikuwa dhaifu kifedha, jambo ambalo liliathiri zaidi uwiano katika uandishi wa habari.”

Vyama vidogo vilikumbana na changamoto kubwa katika kupata uangalizi unaolingana. Ukosefu wa rasilimali za kifedha, miundo dhaifu ya kiutawala, na ugumu wa kuratibu mahusiano na vyombo vya habari

vilipunguza uwepo wao katika vyombo vya asili vya habari. Zanzibar, mmoja wa mameneja wakuu wa Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC), aliiambia Yearbook kwamba: “ZBC ilisimamia msimamo kwamba haikupendelea chama chochote cha siasa kwa makusudi na ilijitahidi kutoa nafasi kwa vyama vyote vilivyoshiriki. Hata hivyo, CCM iliweza kuonekana zaidi kutokana na jinsi walivyokuwa wamejipanga vizuri kitaasisi na uhamasishaji.” Baadhi ya wadau walisisitiza kwamba vikwazo hivi vinaakisi zaidi kutokuwepo kwa usawa wa kimuundo ndani ya mfumo wa kisiasa badala ya kuwa matokeo ya ubaguzi wa makusudi kutoka kwa vyombo vya habari.

Wadau pia walibainisha athari ya vigezo vya uhariri wa habari katika kuamua vipaumbele vya uandishi. Vyama vinavyogombea nafasi kubwa za kitaifa au vinavyozua mvuto mkubwa kwa umma kwa kawaida hupata uangalizi zaidi, jambo linaloakisi utaratibu wa kawaida wa uandishi wa habari. Msisitizo huu uliendelea kuchangia kutokuwepo kwa usawa wa mwonekano miongoni mwa wahusika wenye viwango tofauti vya umaarufu wa kisiasa.

Mitazamo kuhusu kutokuwepo kwa uwiano ilitofautiana miongoni mwa makundi ya wadau. Wakati baadhi ya wawakilishi wa kisiasa walitafsiri tofauti hizo kama ushahidi wa upendeleo, waandishi wa habari mara nyingi walielekeza kwenye sababu za kimfumo na kiutendaji kama vichocheo vikuu. Tofauti hii inaonesha umuhimu wa kutofautisha kati ya maamuzi ya makusudi ya kiuhariri na athari za mifumo katika namna vyombo vya habari vinavyowasilisha wahusika mbalimbali.

Hii inaonesha mwingiliano na changamano kati ya kanuni za uandishi wa habari, mienendo ya soko, na rasilimali za kisiasa katika uripoti wa uchaguzi. Kufikia usawa mkubwa zaidi katika chaguzi zijazo kunaweza kuhitaji hatua maalum, ikiwa ni pamoja na kuboresha upatikanaji wa majukwaa ya vyombo vya habari kwa vyama vyenye rasilimali chache na kuweka miongozo iliyo wazi kuhusu uripoti wa uchaguzi wenye uwiano.
Kwa ujumla, matokeo yanaonesha kuwa mwonekano wa kisiasa wakati wa uchaguzi uliathiriwa si tu na maamuzi ya uhariri bali pia na hali za kimuundo. Kuelewa mienendo hii ni muhimu katika kubuni mikakati ya kukuza uwakilishi wa vyombo vya habari ulio na uwiano na jumuishi zaidi katika michakato ya uchaguzi ijayo.

5.4 Kuzimwa kwa intaneti na kuvurugwa kwa taarifa

Kuzimwa kwa kwa intaneti kuliibuka kama mojawapo ya sababu zenye athari kubwa zaidi katika utendaji wa vyombo vya habari wakati wa kipindi cha uchaguzi. Kusitishwa kwa intaneti, kulivuruga mchakato mzima wa uzalishaji wa habari, kuanzia ukusanyaji wa taarifa na mawasiliano na waandishi wa maeneo mbalimbali hadi uthibitishaji wa vyanzo na uchapishaji wa habari. Waandishi wa habari walieleza tukio hili kama wakati ulioonesha wazi kiwango kikubwa cha utegemezi wa vyombo vya habari kwa miundombinu ya kidijitali.

Vyumba vya habari vilikumbana na changamoto kubwa za kiutendaji, ikiwa ni pamoja na ucheleweshaji wa kupokea taarifa kutoka kwa waandishi wa mikoa na ugumu wa kupata vyanzo vya data mtandaoni. Wahariri walilazimika kutegemea njia mbadala za mawasiliano, kama vile kupiga simu za kawaida, jambo lililopunguza ufanisi na kuchelewesha usambazaji wa habari. Usumbufu huu uliathiri vyombo vya habari vinavyotegemea mtandao pekee (kidijitali) pamoja na vile vya asili.

Vile vile, kuzimwa kwa intaneti kulileta athari mbaya kwa umma katika kupata habari. Wananchi waliotegemea vyombo vya habari vya mtandaoni kujipatia taarifa za yanayojiri, walijikuta wakiwa na vyanzo vichache vya kuwapatia taarifa za papo kwa hapo, hivyo kuminya uwezekano wa kupata mitazamo tofauti iliyopo kwenye kipindi muhimu cha mchakato wa kidemokrasia. Hali hii inasisitiza umuhimu wa kuunganishwa na intaneti ili kuwa na ushiriki wa jamii yenye taarifa sahihi.

Athari za kiuchumi zilikuwa za haraka na zilienea sehemu kubwa. Vyombo vya habari viliripoti kupoteza mapato ya matangazo na ushiriki wa hadhira, hasa vile vilivyokuwa na mifumo imara ya kidijitali. Mhariri mmoja wa vyombo vya habari mtandaoni alieleza kwamba, “kwa vyombo vya habari vya mtandaoni, kuzimwa kwa intaneti kulikuwa na athari kubwa kwa sababu miundombinu yao yote inategemea intaneti.” Aliongeza kuwa, “hofu na hatua za awali za udhibiti zilichochea zaidi kujidhibiti katika uandishi wa habari.” Usumbufu huu uliweka wazi udhaifu wa taasisi za vyombo vya habari zinazofanya kazi katika mazingira yenye rasilimali
finyu za kifedha pamoja na athari pana za kiuchumi zinazotokana na vizuizi vya kiteknolojia. “Kiuchumi, athari zilikuwa kubwa. Kama taasisi, tulipoteza mapato ya matangazo kutoka kwa wateja... kuzimwa kwa mtandao kuliathiri huduma za fedha kwa njia ya simu, benki mtandaoni, wananchi wa kawaida, pamoja na taasisi za binafsi na za umma,” alisema mmoja wa wahariri wakuu wa kituo cha redio.

Ripoti iliyotolewa na Tech & Media Convergency (TMC) mwaka 2026 inaeleza kuwa kuzimwa kwa huduma za intaneti wakati wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 (29 Oktoba–3 Novemba 2025) kulivuruga kwa kiasi kikubwa mfumo wa kidijitali na shughuli za kiuchumi nchini Tanzania, kusababisha hasara ya jumla ya Dola za Kimarekani zaidi ya Milioni 250. Matokeo haya yanaonesha kuwa vikwazo vya intaneti havipunguzi tu upatikanaji wa taarifa, bali pia husababisha athari kubwa za kiuchumi na kitaasisi, jambo linalosisitiza umuhimu wa kulinda miundombinu ya kidijitali wakati wa michakato ya uchaguzi.

Kuzimwa kwa intaneti kuliathiri mchakato wa kuthibitisha habari, kwani waandishi wa habari walikuwa na wakati mgumu katika kuthibitisha taarifa walizo nazo kupitia vyanzo mbali mbali vya

habari. Kikwazo hiki kilisababisha uwepo wa uripoti wenye tahadhari kubwa na wakati fulani, kuchelewa kuipeleka habari hewani mpaka uthibitisho ulipopatikana. Mazingira hayo yanathibitisha ni kwa namna gani changamoto za kiteknolojia zinaweza kuathiri uamuzi wa kiuhariri na usahihi wa taarifa.

Wadau walibainisha kwamba muda wa kuzimwa kwa intaneti bila kutarajia uligongana na kipindi cha mivutano mikubwa ya kisiasa, jambo ambalo liliongeza athari zake kwenye shughuli za vyombo vya habari na mtazamo wa umma. Kukatika kwa njia za mawasiliano kulichangia kuleta wasiwasi na dhana, ikionyesha umuhimu wa taarifa zinazopatikana kwa wakati katika kudumisha imani ya umma.

Uzoefu huu uliibua tafakari pana kuhusu ustahimilivu wa mifumo ya kidijitali na umuhimu wa kupanga mikakati ya dharura ndani ya vyombo vya habari. Kuimarisha mifumo mbadala ya kimawasiliano na kuanzisha protokali bayana za namna ya kufanya kazi nyakati za kukatika kwa intaneti vilionekana kuwa ni vitu vya kupewa kipaumbele wakati tukijiandaa kwa hali kama hizo hapo baadae.

Kwa ujumla, kuzimwa kwa intaneti sio kwamba kulifanya kazi kama tatizo la kiufundi tu bali pia kama tukio la kimfumo lililotengeneza upya mazingira ya upashanaji habari. Kujihakikishia upatikanaji wa kuaminika wa miundombinu ya kidijitali ni muhimu katika kulinda utendaji wa vyombo vya habari na upatikanaji wa taarifa kwa umma wakati wa uchaguzi zijazo.

5.5 Uwajibikaji mdogo na kuripoti utendaji

Wakati vyombo vya habari vikiripoti kwa kina matukio ya kampeni, ilani za uchaguzi, na mijadala ya kisiasa, tathmini ya kimfumo ya matukio yaliyopita ya wagombea haikuwa endelevu kwenye vyombo vyote vya habari. Wadau waliona kwamba uripoti uliotegemea matukio ndio ulitawala kwenye vyombo vya habari ikiakisi ukaribu wa shughuli za kampeni na changamoto halisi za kuripoti uchaguzi.

Changamoto za kirasilimali ndio ilikuwa sababu ya msingi iliyosababisha kutokuwepo kwa uripoti wa kina wa kiuwajibikaji. Kazi za kiuchunguzi zinahitaji muda, ujuzi mahsusi, na uwekezaji wa kifedha, vitu ambavyo havikugawanyika kwa usawa kwa taasisi zote za vyombo vya habari. Kipekee, vituo vidogo vidogo vya habari vilikumbana na ugumu katika kudumisha uchambuzi wa kina kwenye kipindi kilichokuwa na kasi ya aina yake wakati wa uchaguzi.

Upatikanaji wa habari pia uliathiri mawanda ya uripoti. Waandishi wa habari waliripoti changamoto zilizokuwepo kwenye kupata rekodi za kina za matokeo ya sera au utendaji wa serikali, hali iliyozuia fursa ya kuwa na uchunguzi wa kina. Mapengo haya ya taarifa yanaonyesha umuhimu wa uwazi na upatikanaji rahisi wa data za umma kwa ajili ya uripoti wa kiuwajibikaji wenye ufanisi.
Tahadhari ya kiuhariri iliendelea kuathiri uripoti. Katika mazingira yenye unyeti wa kisiasa, baadhi ya vyombo vya habari viliweka kipaumbele kuripoti matukio kwa kuzingatia ukweli zaidi kuliko kufanya uchambuzi wa kina, hali iliyoakisi hofu ya madhara yanayoweza kujitokeza au tafsiri potofu dhidi ya uchambuzi huo. Mtazamo huu uliwezesha mwendelezo wa utoaji wa habari, lakini ulipunguza uzito wa maudhui ya uchunguzi.
Licha ya vikwazo hivi, wadau walikiri kwamba baadhi ya vyombo vya habari vilifanya jitihada za kuendesha mahojiano ya wasifu na vipindi vya uchambuzi vilivyochunguza rekodi za wagombea. “TBC ilifanikiwa kuandaa wasifu wa wagombea wote, ikilenga maono na ahadi zao. Hata hivyo, kulikuwa na msisitizo mdogo katika kuchunguza mapungufu au kutathmini kwa kina utendaji wao wa awali,” alisema mmoja wa wafanyakazi waandamizi wa TBC wakati wa mahojiano. Mipango hii inaonesha kuwa uandishi wa habari wa uwajibikaji uliendelea kuwepo, japokuwa haukusambazwa kwa uwiano sawa katika sekta nzima.

Msisitizo juu ya ahadi za kampeni zinazolenga siku zijazo badala ya tathmini ya yaliyopita pia uliakisi mahitaji ya hadhira ya kupata taarifa za haraka kuhusu maendeleo ya kisiasa. Vigezo vya uandishi wa habari vinavyotanguliza wakati (uharakati wa habari) na umuhimu wake vilichochea maamuzi ya kiuhariri, vikionesha mwingiliano kati ya matarajio ya hadhira na utendaji wa uandishi wa habari.

Kuimarisha uandishi wa habari wa uwajibikaji kulitambuliwa kwa upana kama kipaumbele kwa chaguzi zijazo. Wadau walisisitiza umuhimu wa kuboresha upatikanaji wa taarifa za umma, kuwekeza katika uwezo wa uandishi wa uchunguzi, na kuanzisha mipango ya ushirikiano ili kusaidia uchambuzi wa kina.

Kwa ujumla, matokeo yanaonesha kwamba ingawa vyombo vya habari vilitimiza jukumu lake la kutoa taarifa, nafasi yake ya kuwa msimamizi (watchdog) ilizuiwa kwa kiasi fulani na sababu za kimuundo na kimazingira. Kushughulikia vikwazo hivi kunaweza kuboresha kina na ufanisi wa uandishi wa habari kuhusu uchaguzi uchaguzi kwa siku za usoni.

5.6 Usalama wa waandishi wa habari na upungufu wa kiulinzi

Uchaguzi mkuu wa mwaka 2025 ulionyesha uthabitiwa waandishi wa habari pamoja na udhaifu wa kimuundo katika mifumo iliyoandaliwa kuwalinda. Wadau walifafanua mazingira ambamo kwamo waandishi wa habari mara kwa mara wanafanyia kazi, yaliwafanya kuwa na wasiwasi mkubwa wa kiusalama, hasa wakati wa kampeni, maandamano, na yaliyotokea baada ya uchaguzi. Mazingira ya aina hii siyo tu yaliathiri uripoti kutoka uwandani bali pia hata mipango ya vyumba vya habari na tathmini kuhusu hatari zilizopo.

Matukio yanayohusisha vitisho, unyanyasaji, na vurugu dhidi ya waandishi wa habari yalitajwa mara kwa mara kama ushahidi wa hatari zinazohusiana na uandishi wa habari kuhusu uchaguzi. Hata pale ambapo matukio hayo yalikuwa ya maeneo maalum, yalikuwa na athari pana katika taaluma nzima, yakiongeza hisia ya pamoja ya kuwa katika hatari miongoni mwa wanahabari. Mtazamo huu wa hatari uliathiri maamuzi kuhusu ugawaji wa kazi, usafiri, na namna ya kuwasilisha habari nyeti.

Mashirika ya vyombo vya habari yalijiandaa kwa viwango tofauti vya maandalizi. Taasisi kubwa mara

nyingi zilianzisha mafunzo ya usalama, vifaa vya kujikinga, na mipango ya dharura, huku vyombo vidogo vikitegemea zaidi mitandao isiyo rasmi ya msaada. Akielezea maandalizi katika chombo chake cha habari, mhariri wa UTV alisema kwamba, “UTV iliweka mpango wa kina wa kuripoti uchaguzi… vifaa vya kujikinga, ambulensi za dharura, huduma za matibabu, na msaada wa kisaikolojia vilitolewa kwa waandishi wa habari.” Tofauti hizi zinaonesha athari ya rasilimali za taasisi katika uwezo wa kulinda wafanyakazi kwa ufanisi.

Ustawi wa kisaikolojia uliibuka kama kipengele muhimu cha usalama wa waandishi wa habari. Kuripoti matukio yenye mvutano wa kisiasa katika mazingira yasiyotabirika kulisababisha msongo wa mawazo na uchovu wa kihisia, hali iliyosisitiza umuhimu wa kuwepo kwa mifumo rasmi ya msaada wa kisaikolojia ndani ya vyombo vya habari. Wadau walisisitiza kwamba masuala ya afya ya akili ni sehemu muhimu katika kudumisha utendaji wa kitaaluma.

Ukosefu wa mfumo wa kitaifa ulioratibiwa wa usalama ulitambuliwa kwa upana kama pengo kubwa. Ingawa vyombo vya habari vya binafsi vilianzisha hatua za ndani, kukosekana kwa mkabala wa pamoja kulipunguza ufanisi wa mikakati ya ulinzi. Wadau walipendekeza kwamba kuwepo kwa taratibu zilizo wazi zaidi pamoja na ushirikiano imara na vyombo vya usalama kunaweza kuboresha kiwango cha maandalizi.

Mafunzo na programu za kujenga uwezo zilitambuliwa kuwa muhimu katika kuboresha matokeo ya usalama. Mafunzo ya uelewa wa hatari, ujuzi wa kuripoti wakati wa migogoro, na uwepo wa njia wazi za mawasiliano vilibainishwa kama hatua za vitendo zinazoweza kuimarisha uwezo wa waandishi wa habari kufanya kazi kwa usalama katika mazingira yenye hali tete.

Mada hii pia inaonesha uhusiano kati ya usalama na uhuru wa vyombo vya habari. Waandishi wa habari wanapojihisi salama, huwa na uwezekano mkubwa wa kufuatilia habari muhimu na kushiriki katika uandishi wa uchunguzi. Kinyume chake, hali ya kutokuwa salama inaweza kusababisha uripoti wenye tahadhari unaotanguliza ulinzi binafsi kuliko dhamira ya kiuhariri.

Kwa ujumla, matokeo yanaonesha kuwa kuimarisha usalama wa waandishi wa habari kutahitaji dhamira ya taasisi pamoja na mageuzi ya kimfumo. Kuanzisha mifumo ya kina ya ulinzi kutakuwa muhimu ili kuhakikisha kuwa wanahabari wanaweza kutekeleza majukumu yao bila hatari zisizo za lazima katika chaguzi zijazo.

5.7 Ujumuishaji, upatikanaji na mienendo ya kijinsia

Jitihada za kukuza uripoti wa wa vyombo vya habari wenye ujumuishi wakati wa uchaguzi wa mwaka 2025 ziliakisi maendeleo pamoja na changamoto zinazoendelea. Wadau walibainisha kwamba baadhi ya vyombo vya utangazaji vilijumuisha hatua za kurahisisha upatikanaji wa maudhui, kama vile matumizi ya wakalimani wa lugha ya alama, hasa katika vipindi muhimu vya kisiasa. Hatua hizi zinawakilisha maendeleo muhimu katika kuhakikisha kuwa taarifa za uchaguzi zinafikia hadhira pana zaidi.

Hata hivyo, utekelezaji haukuwa wa uwiano katika mazingira ya vyombo vya habari. Vikwazo vya rasilimali vilizuia baadhi ya vyombo kutoa huduma hizi za ufikivu kwa uthabiti, hasa katika vyombo vya habari vidogo vidogo na vyenye bajeti ndogo. Hali hii inaonesha umuhimu wa msaada wa kitaasisi katika kuendeleza mawasiliano jumuishi.

Mienendo ya kijinsia pia iliathiri ushiriki wa vyombo vya habari. Wagombea wanawake walishiriki kikamilifu katika mahojiano na mijadala, hata hivyo wadau waliripoti kuwa mara nyingi walikumbana na uchunguzi wa ziada pamoja na uhasama mtandaoni. “Kulikuwa na jitihada za makusudi za kuepuka ubaguzi katika uandishi wa habari wa kawaida, lakini kwenye mitandao ya kijamii kulijaa bughudha, lugha za matusi, na maoni ya kudhalilisha yaliyowalenga wanawake”, alisema Mkurugenzi Mtendaji wa moja ya mashirika ya vyombo vya habari nchini. Uzoefu huu unaonesha jinsi mitazamo ya kijamii inavyoingiliana na uwakilishi wa vyombo vya habari, na hivyo kuathiri ushiriki pamoja na mtazamo wa umma.

Mazingira mapana ya kidijitali yalikuwa na mchango mkubwa katika kuunda ujumuishi. Majukwaa ya mitandao ya kijamii yalitoa nafasi mbadala za ushiriki, lakini pia yaliwaweka wagombea katika hatari ya unyanyasaji na upotoshaji wa taarifa. Kuzimwa kwa intaneti pia kuliathiri ujumuishi kwa kuzuia upatikanaji wa majukwaa haya, hasa kwa makundi yanayotegemea kwa kiwango kikubwa mawasiliano ya kidijitali.

Upatikanaji pia ulihusishwa na mazingira ya kimwili ya matukio ya kisiasa. Wadau walibainisha kuwa maeneo ya kampeni hayakuwa kila mara na miundombinu inayoweza kuwahudumia watu wenye ulemavu, jambo lililopunguza ushiriki wao pamoja na mwonekano wao kwenye vyombo vya habari. Hata hivyo, baadhi ya vyombo vya habari vilifanya jitihada zinazostahili pongezi katika kuhakikisha taarifa za uchaguzi zinawafikia wananchi wote. Akizungumzia hili, kiongozi mwandamizi wa TBC alisema, “TBC iliimarisha ujumuishi kwa kuongeza idadi ya wakalimani wa lugha ya alama… kuhakikisha kwamba watu wenye ulemavu wa kusikia wanapata taarifa.” Kauli hii inaonesha kwa dhahiri jinsi vikwazo vya kimuundo vinavyohusiana kwa karibu katika kuathiri ujumuishi.

Taasisi za vyombo vya habari zilihimizwa kupitisha mikakati ya ujumuishi ya makusudi badala ya hatua za kuitikia baada ya matatizo kujitokeza. Wadau walisisitiza kwamba uandishi wa habari wenye usawa unahitaji upangaji wa makini, ikiwa ni pamoja na vipindi maalum, ushirikiano na makundi ya utetezi, na viwango thabiti vya upatikanaji wa maudhui.

Mawasiliano jumuishi ni nguzo muhimu ya ushiriki wa kidemokrasia. Pale ambapo makundi fulani yanakumbana na vikwazo vya kupata taarifa au uwakilishi, ubora wa ushiriki wa kidemokrasia kwa ujumla huathirika.

Kwa muhtasari, ingawa kulikuwa na maendeleo yanayoonekana, kufikia uandishi wa habari wa uchaguzi ulio jumuishi kikamilifu kutahitaji dhamira endelevu, ugawaji wa rasilimali, na ushirikiano kati ya taasisi mbalimbali. Kuimarisha mifumo ya upatikanaji wa maudhui kutakuwa muhimu katika kuhakikisha ushiriki wenye usawa katika chaguzi zijazo.

5.8 Udhaifu wa kiuchumi na shinikizo la kibiashara

Udhaifu wa kiuchumi ulijitokeza kama jambo linaloonekana kuwa sababu inayoathiri utendaji wa vyombo vya habari wakati wa uchaguzi. Vyombo vingi ya habari vilifanya kazi huku vikiwa kwenye bajeti finyu, hivyo kujikuta vikitegemea mapato yanayotokana na matangazo ya biashara, hasa kwenye kampeni za kisiasa. Hali hii ya utegemezi iliathiri vipaumbele vya kiuhariri na ufanyaji uamuzi kitaasisi.

Kipindi cha uchaguzi kilikuwa na sura mbili yaani kipindi cha fursa lakini pia ni kipindi cha hatari kwa taasisi za vyombo vya habari. Wakati ongezeko la matangazo ya biashara ya kisiasa likiongeza kipato kwa vyombo vya habari, hali hiyo pia iliongeza shinikizo kibiashara, hasa kwa vyombo vya habari vilivyohitaji kudumisha uhusiano na watoa matangazo wakubwa (major advertizers). Mienendo hii inaonyesha uhusiano tete kati ya nguvu ya soko na uhuru wa uhariri.

Kuzimwa kwa intaneti kuliongeza changamoto za kifedha, kulivuruga ratiba za matangazo ya biashara na kushusha kiwango cha ushirikishwaji wa hadhira. Taasisi za vyombo habari ziliripoti hasara kubwa na usumbufu kiutendaji, hali inayoonyesha udhaifu wa taasisi zinazotegemea majukwaa ya kidijitali. Shida hizi za kifedha zilionesha umuhimu zaidi wa kuwa na vyanzo tofauti vya mapato.

Vyombo vidogo vya habari vya kijamii viliathirika zaidi kwani havikuwa na msuli wa kifedha kukabiliana na usumbufu uliojitokeza. Kwa hiyo, utofauti wa kipato miongoni mwa vyombo vya habari ulitafsiriwa kwa namna tofauti katika ustahimilivu na katika uwezo wake kuendeleza uripoti kwenye nyakati za changamoto.

Masuala ya kibiashara pia yaliathiri uamuzi wa upangiliaji wa vipindi. Uandishi wa habari unaotegemea matukio, kama vile matangazo ya moja kwa moja ya mikutano ya kampeni na matamko ya kampeni, mara nyingi ulipewa kipaumbele kutokana na gharama zake ndogo za uzalishaji na mvuto mkubwa kwa hadhira. Uripoti uliotegemea matukio kama vile kuripoti mubashara kampeni za vyama vya siasa pamoja na matangazo ya kampeni mara nyingi vilipewa kipaumbele kwa sababu ya gharama ndogo za uzalishaji na mvuto wake kwa jamii. Kinyume chake, uandishi wa habari za uchunguzi ulihitaji uwekezaji mkubwa, na kwa hiyo haukupewa kipaumbele.

Wadau walisisitiza umuhimu wa kuwa na mfumo endelevu wa kibiashara ambao utapunguza utegemezi kwenye mapato yatokanayo na uchaguzi. Kuwa na vyanzo tofauti vya mapato ikiwa ni pamoja na kuwa na ubia na mikakati ya kibunifu ya kidijitali ilionekana inaweza kuimarisha ustahimilivu wa kifedha kwa vyombo vya habari.

Uhusiano kati ya uthabiti kiuchumi na uhakika wa kiuhariri ilikuwa ni mada inayojirudiarudia. Taasisi za vyombo vya habari zenye msuli wa kifedha zilikuwa na nafasi nzuri ya kufanya uripoti wa kina, na kujihakikishia uhuru wake, wakati vile vilivyokuwa na ufinyu wa bajeti, vilichukua mkondo wa kuwa na uripoti wenye tahadhari kubwa.

Kiujumla, matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba, uthabiti endelevu wa kiuchumi ni suala linaloendana moja kwa moja na mafanikio ya kiutendaji kwa vyombo vya habari. Kuimarisha hali ya ustahimilivu wa kifedha kwa vyombo vya habari kutaongeza uwezo wao katika kufanikisha majukumu yao ya kidemokrasia kwenye chaguzi zijazo.

5.9 Mageuzi ya udhibiti na uhalali wa taasisi

Mara nyingi wadau walitafsiri changamoto za vyombo vya habari wakati wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 katika muktadha mpana wa uaminifu wa taasisi na mifumo ya utawala. Wengi wa waliohojiwa walisisitiza kuwepo kwa uhusiano wa karibu kati ya ufanisi na uhuru wa taasisi za vyombo vya habari, kwa upande mmoja, na uhalali wa taasisi za uchaguzi na za udhibiti, kwa upande mwingine. Pale ambapo uaminifu wa taasisi unakuwa na mashaka, uandishi wa habari huwa chini ya uchunguzi mkali zaidi na tafsiri za kisiasa.

Mifumo ya udhibiti ilitambuliwa kwa upana kuwa muhimu katika kudumisha viwango vya kitaaluma na kuzuia upotoshaji wa taarifa. Hata hivyo, wadau pia walisisitiza umuhimu wa kuwa na uwiano na uwazi katika utekelezaji wake. Mitazamo kwamba mifumo ya usimamizi ilikuwa na vikwazo vingi kupita kiasi au ilitumika kwa namna isiyo thabiti ilichangia hali ya kutokuwa na uhakika ndani ya vyombo vya habari na kuathiri maamuzi ya kiuhariri.

Wito wa mageuzi ulilenga kuboresha uwazi na utabirikaji katika michakato ya udhibiti. Wadau walipendekeza kurahisishwa kwa taratibu za usajili (accreditation), utoaji wa miongozo iliyo wazi zaidi, na kuwepo kwa majadiliano ya kimfumo kati ya wadhibiti na taasisi za vyombo vya habari ili kupunguza mvutano na kuimarisha uelewano wa pande zote.

Upatikanaji wa taarifa uliibuka kama suala lingine muhimu. Waandishi wa habari walibainisha changamoto katika kupata data rasmi kwa wakati na kwa kina, jambo lililopunguza uwezo wao wa kufanya uandishi wa habari wa uchambuzi wa kina. Hivyo, kuimarisha mifumo ya uwazi na kuboresha upatikanaji wa taarifa za umma kulionekana kuwa hatua muhimu katika kuendeleza uandishi wa habari wa uwajibikaji.
Mjadala mpana kuhusu uhalali wa uchaguzi pia uliathiri mitazamo kuhusu utendaji wa vyombo vya habari. Pale ambapo baadhi ya makundi ya umma au wanasiasa walitilia shaka haki ya michakato ya uchaguzi, uandishi wa habari ulitafsiriwa kupitia mtazamo wa kuaminika au kutoaminika kisiasa. Mienendo hii inaonesha uhusiano wa karibu kati ya taasisi za kidemokrasia na mfumo wa vyombo vya habari.

Wadau walisisitiza kwamba mageuzi ya udhibiti hayapaswi tu kuimarisha usimamizi bali pia kuunda mazingira wezeshi kwa uandishi wa habari ulio huru. Kuweka uwiano kati ya udhibiti na kuunga mkono uhuru wa uhariri kulionekana kuwa jambo muhimu katika kujenga hali ya jamii kuziamini taasisi za kiusimamizi na vyombo vya habari.

Ulinganifu wa taasisi katika kuunga mkono mawasiliano ya kidemokrasia ni muhimu. Pale ambapo mifumo ya utawala inaonekana kuwa ya haki na yenye uwazi, taasisi za vyombo vya habari zinaweza kufanya kazi kwa kujiamini zaidi na kwa uaminifu mkubwa. Kwa ujumla, matokeo yanaonesha kwamba kuimarisha uhalali wa taasisi kupitia mifumo ya udhibiti iliyo wazi na yenye uwajibikaji, kutakuwa jambo la msingi katika kuboresha utendaji wa vyombo vya habari katika chaguzi zijazo.

6.0 URIPOTI WA VYOMBO HABARI VYA KIMATAIFA KWENYE MATUKIO YA BAADA YA UCHAGUZI

Siku ya kupiga kura ilikuwa tarehe 29 Oktoba, 2025. Siku hiyo, kutegemeana na unayemuuliza, maandamano, migomo, na vurugu ziliripuka, hali iliyotikisa usalama na mchakato wa upigaji kura. Siku hiyo hiyo, Inspekta Jenerali wa Polisi (IGP), Camilius Wambura, alitokea katika kituo cha taifa cha utangazaji, TBC1, na kutangaza amri ya kutotoka nje kuanzia saa 12 jioni hadi saa 12 asubuhi jijini Dar es Salaam, ambayo kwa vitendo, ilitekelezwa nchi nzima. Tangu wakati huo, Chama cha Mawakili Tanganyika (TLS) kilifungua kesi ya kikatiba kikihoji uhalali wa amri ya kutotoka nje Siku iliyofuata, tarehe 30 Oktoba 2025, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi (CDF), Jacob John Mkunda, alijitokea pia katika Chombo cha Taifa cha Utangazaji (TBC1) na kuamuru kusitishwa kwa kile alichokiita "vitendo vya kihalifu" vinavyofanywa na watu wasioitakia mema Tanzania

Kufuatia vurugu hizo za uchaguzi na kiusalama, haraka sana nchi iliwekwa kwenye hali ya udhibiti wa kidijitali ili kudhibiti mitandao ya kijamii na mawasiliano ya mtandaoni. Uamuzi huo ulilaumiwa sana na taasisi mbalimbali ikiwamo Tume ya Haki za Binadamu Afrika (The African Commission on Human and Peoples' Rights - ACHPR), ambayo, sehemu ya tamko lake lililotolewa tarehe 1 Novemba, 2025 inasomeka, "Tume imeguswa na ripoti kwamba, siku ya Jumatano, tarehe 29 Oktoba 2025, Tanzania, ilikumbwa na kukatika kwa huduma ya intaneti nchi nzima, wakati uchaguzi ulipoanza huku kukiwa na mawasiliano machache sana au kutokuwepo kabisa... Kusitishwa kwa huduma za intaneti bila shaka kunajumuisha ukiukwaji wa Ibara ya 9 ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu, ambayo inahakikisha haki ya kila mtu kupata taarifa, pamoja na haki ya kujieleza na kusambaza taarifa... Tume inaitaka Serikali ya Tanzania kutekeleza wajibu wake wa kulinda haki za binadamu nchini, kwa kuhakikisha kuwa haki za wananchi za uhuru wa kujieleza na upatikanaji wa taarifa zinaheshimiwa na kulindwa."

Kuwepo kwa amri ya kutokutoka nje, kuzorota kwa hali ya usalama, na kuzimwa kwa intaneti, kulivikuta vyombo vya habari na waandishi wa habari nchini wakiwa hawajajiandaa. Mazingira haya yaliifanya kazi yao kuwa ngumu mno, na vyombo vingi vya habari vya utangazaji viliamua kurusha maudhui ya muziki, makala za siku nyingi, na tamthiliya. Kuwepo kwa amri ya kutokutoka nje, moja kwa moja magazeti yalijikuta hayapo sokoni. Ombwe lililotokana na kuzimwa kwa mawasiliano, kwa haraka lilijazwa na vyombo vya habari vya kimataifa kutoka barani Afrika na nje ya Afrika. Utafiti huu ulifanya mapitio ya nasibu ya uripoti wa baadhi ya vyombo vya habari vya kimataifa kwa kutumia sampuli ndogo, kwa kuwa kipengele hiki hakikuwa sehemu ya msingi ya upeo wa utafiti wa awali.

Uripoti wa vyombo vya habari vya kimataifa kuhusu matukio ya baada ya uchaguzi nchini ulijikita katika maeneo makuu manne: ukiukwaji wa haki za binadamu na matumizi ya nguvu kupita kiasi ya vyombo vya dola—ikiwemo mauaji, utekaji na utesaji; wito wa kuundwa kwa serikali ya mpito; wito wa kufanyika kwa uchunguzi wa kimahakama; na suala la uhalali wa uchaguzi. Vyama vya upinzani, mashirika ya kimataifa pamoja na mashirika ya haki za binadamu vilitawala mijadala katika vyombo vya habari na maeneo ya umma, huku sauti za serikali zikionekana kwa kiwango kidogo. Hata hivyo, hakuna kati ya masuala hayo manne yaliyodumu kama ajenda endelevu ya vyombo vya habari vya ndani baada ya uchaguzi, mara tu amri ya kutotoka nje ilipoondolewa na huduma za intaneti kurejeshwa.

Uripoti wa vyombo vya habari vya kimataifa ulikuwa na nafasi yake muhimu katika kujenga mtazamo wa hadhira ya ndani ya nchi na ile ya kimataifa. Ndani ya nchi, palitengenezwa mijadala ya kijamii, hasa mitandaoni. Makala ya CNN iliyoitwa: "'Oh Mungu wangu, hii ndiyo Tanzania yetu': Uchunguzi wa CNN unaonyesha polisi wakiwapiga risasi waandamanaji, ishara ya makaburi ya halaiki", ni mfano wa taarifa iliyoibua mijadala. Makala iliripoti kwamba polisi na watu wenye silaha waliwapiga risasi waandamanaji ambao hawakuwa na silaha, wengi wao walionekana wamebeba mawe na fimbo tu, na ilitoa ushahidi wa maiti nyingi kupita kiasi na picha za setelaiti kuthibitisha uwepo wa makaburi ya halaiki huko Dar es Salaam. Serikali ya Tanzania iliukosoa uandishi wa habari wa aina hiyo, ikidai ulikuwa wa kuchochea jamii na uliokosa maadili kwa kutokutoa nafasi kwa serikali kujibu madai hayo, jambo ambalo CNN walilipinga wakisema walikwenda kwa serikali lakini hawakupata jibu lolote.

Makala ya CNN ilikosolewa na gazeti linalomilikiwa na serikali, Daily News, kwenye Makala yake iliyoitwa, "Wakati uripoti wa habari unapogeuka uchochezi: Kwa nini uripoti wa CNN kuhusu Tanzania unahitaji kuchunguzwa". Sehemu ya Makala hiyo inasomeka: "Kwa nchi kama Tanzania, inayotoka kwenye uchaguzi uliokumbwa na ghasia, hasara na msongo wa kijamii, nguvu hii inabeba jukumu kubwa la kimaadili. Vyombo vya habari vya kimataifa vinavyoripoti kuhusu matukio haya vina wajibu wa kimaadili kuhabarisha watu kuhusu ukweli, kwa hekima, na katika muktadha sahihi". Hata hivyo, uripoti wa CNN unaoendelea kuhusu matukio ya baada ya uchaguzi nchini, unaleta wasiwasi mkubwa wa kimaadili. Badala ya kutoa habari zenye uwiano, kutoka katika muktadha sahihi wa uripoti, mtandao huo unaonekana kutumia picha zinazorudiwarudiwa, zenye hisia kali, na zenye kutoa mtazamo wa upande mmoja, hali ambayo inahatarisha siyo tu uadilifu wa kiuandishi wa habari bali pia hali tete ya jamii iliyo kwenye taifa lenye majonzi".

Uripoti wa vyombo vya habari vya kimataifa uliweka mkazo mkubwa kwenye vifo, huku vyombo mbalimbali vikitoa takwimu tofauti za idadi ya waliokufa. Vikiwanukuu viongozi wa vyama vya upinzani, makundi ya kutetea haki za binadamu pamoja na vyanzo vya kidiplomasia, uripoti huo uliweka idadi ya vifo kati ya mamia na maelfu. Habari ya BBC iliyochapishwa tarehe 1 Novemba 2025 iliripoti: "Wakati msemaji wa chama cha upinzani CHADEMA akiliambia shirika la habari la AFP kwamba 'takribani watu 700' walikuwa wameuawa katika makabiliano na vikosi vya usalama, chanzo cha kidiplomasia nchini Tanzania kiliiambia BBC kuwa kulikuwa na ushahidi wa kuaminika kwamba angalau watu 500 walikuwa wameuawa". Hakuna taarifa yoyote kati ya zilizoripotiwa kuhusu idadi ya vifo iliwahi kuthibitishwa na chanzo chochote cha kiserikali.

7.0 TATHMINI YA USHIRIKI WA WANANCHI MTANDAONI

Utafiti huu ulichunguza vipengele viwili vya ushiriki wa wananchi katika mchakato wa uchaguzi. Kipengele cha kwanza, kilichojadiliwa awali, kinahusu namna vyombo vya habari vinavyojumuisha sauti za wananchi katika uripoti wao. Kipengele cha pili kinachunguza ushiriki wa wananchi mtandaoni, hususan namna wanavyojihusisha na machapisho yanayohusiana na uchaguzi kwenye mitandao ya kijamii. Juhudi hii ni ya kwanza kuchunguza jinsi wananchi wanavyoitikia machapisho kama haya kutoka kwenye vyombo vya habari nchini.

Ili kutathmini ushiriki wa wananchi mtandaoni, utafiti ulichambua habari za uchaguzi kutoka majukwaa mbalimbali ya vyombo vya habari mtandaoni, hususan majukwaa ya televisheni mtandaoni na akaunti za mitandao ya kijamii za vyombo vya habari vilivyochaguliwa, yaani Facebook na Instagram. Awali, vyombo 14 vya habari mtandaoni vilichaguliwa kama sampuli, lakini uchambuzi wa mwisho ulihusisha saba tu: *TBC Online*, *Ayo TV*, *Global TV*, *Mwananchi Digital*, *Jambo TV*, *Mwanahalisi Online*, *na The Chanzo*. *Vyombo vingine saba—Fullshangwe Blog*, *Michuzi Blog*, *Green Waves Media*, *Pemba Today*, *ASAM Online TV*, *Dar24 na TM Times Majira*—viliondolewa kwenye sampuli kwa sababu havikutimiza kigezo cha kuwa na machapisho yenye angalau maoni (comments) 100. Aidha, Dar24 haikuwa ikifanya kazi katika kipindi cha uchaguzi.

Utafiti ulichunguza maoni 17,202 kutoka kwenye machapisho 200. Kwa kila chapisho, yalichunguzwa maoni 100 ya kwanza, lakini pia tulijumuisha baadhi ya machapisho yaliyokuwa na maoni machache ili kupata uwakilishi wenye usawa kwa vyombo vyote saba, ikizingatiwa kwamba hata idadi ya ushirikishwaji wa hadhira uko tofauti miongoni mwa vyombo hivyo.

Uchunguzi ulihusisha kuchambua kila chapisho na maoni 100 ya mwanzo, kisha kuyaainisha katika makundi yafuatayo: yale yanayoikosoa CCM; yanayoikosoa serikali/mamlaka za dola; yanayokosoa vyama vya upinzani; yanayokosoa vyombo vya usalama/utekelezaji wa sheria; yanayokosoa maudhui ya habari; yanayokosoa taasisi za uchaguzi; yanayoikosoa mhusika au chanzo cha habari; yanayokosoa chombo cha habari na mwandishi; yanayokosoa viongozi au taasisi za dini; yanayokosoa uchaguzi kwa ujumla; yanayokosoa mashirika ya kiraia/wanaharakati/washawishi; yanayounga mkono vyama vya upinzani; yanayounga mkono maudhui ya habari; yanayounga mkono CCM; maoni ya kuunga mkono chapisho; pamoja na mengineyo. Kundi la “mengineyo” liliwekwa ili kuruhusu uainishaji wa maoni ya kipekee ambayo hayakuweza kuingia katika makundi yaliyotajwa hapo juu.

Matokeo yanaonesha kuwa maoni mengi ya wananchi yalikuwa ya ukosoaji dhidi ya wahusika mbalimbali. CCM ilipokea kiwango kikubwa zaidi cha ukosoaji (asilimia 30), ikifuatiwa kwa mbali na maoni yaliyokosoa serikali/mamlaka za dola (asilimia14), vyama vya upinzani (asilimia 12.5), na vyombo vya usalama/utekelezaji wa sheria (asilimia 8.5). Maoni ya kuunga mkono yalikuwa machache. Maoni yaliyounga mkono vyama vya upinzani yalikuwa asilimia 4.5, maudhui ya habari (asilimia 3), CCM (asilimia 3), na yale ambapo watoa maoni waliungana mkono wao kwa wao yalikuwa ni asilimia 2.5.

Maoni ya wananchi mtandaoni

Maoni ya hadhira mtandaoni	Idadi	Asilimia
Kuikosoa CCM	60	30.0
Kuikosoa serikali/mamlaka za nchi	28	14.0
Kukosoa vyama vya upinzani	25	12.5
Kuvikosoa vyombo vya usalama/wasimamizi wa sheria	17	8.5
Kuunga mkono vyama vya upinzani	9	4.5
Kukosoa maudhui ya habari husika	8	4.0
Kukosoa vyombo vinavyosimamia uchaguzi	8	4.0
Kukikosoa chanzo cha habari	7	3.5
Kuunga mkono maudhui ya habari husika	6	3.0
Kukikosoa chombo husika cha habari na mwandishi	6	3.0
Kuiunga mkono CCM	6	3.0
Kuwakosoa viongozi/taasisi za kidini	6	3.0
Kuukosoa uchaguzi kwa ujumla wake	6	3.0
Kuungana mkono wao kwa wao	5	2.5
Kuwakosoa wanaharakati/watu wenye ushawishi	2	1.0
Other	1	0.5
Jumla	**200**	**100**

Kwa ujumla, asilimia 82.5 ya maoni ya wananchi yalikuwa ya ukosoaji dhidi ya taasisi na masuala mbalimbali. Ingawa ni muhimu kutambua uwezekano wa upendeleo katika sampuli hii ya mtandaoni—na kwa ujumla katika sampuli za mtandaoni—kutokana na tofauti za upatikanaji wa teknolojia za kidijitali, takwimu zilizopo zinaonesha kuwa wale waliokuwa hawajaridhika waliweza kueleza maoni yao, huku wengi wao wakitoa maoni hasi. Kwa jumla, zaidi ya nusu ya maoni yote (asilimia 56.5) yalikuwa yakikosoa CCM na serikali.

Kwa ujumla, nafasi ya kidijitali iligawanyika katika makundi mawili: wale waliokuwa wakishinikiza mageuzi kabla ya uchaguzi (No Reform, No Election) chini ya mwavuli wa upinzani, hususan CHADEMA, na wale waliokuwa wakihamasisha uchaguzi uendelee kama ulivyopangwa (Oktoba Tunatiki) kwa upande wa chama tawala. Wananchi walieleza kutoridhishwa kwao kuhusu masuala mbalimbali, wakionyesha kutofurahishwa na CCM, serikali/mamlaka za dola, pamoja na vyama vya upinzani. Mitazamo iliyotolewa ilikuwa pana na ilijumuisha maneno makali na ukosoaji mwingi, ambao baadhi yake yameweza kujumuishwa katika ripoti hii.

8.0 HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

Utafiti huu ulichunguza ubora wa uripoti wa vyombo vya habari kuhusu Uchaguzi Mkuu wa 2025 nchini Tanzania. Kwa kutumia uchambuzi wa maudhui na viashiria maalum vya ubora vinavyotokana na nadharia, taaluma na tafiti za uandishi wa habari, utafiti ulibaini kuwepo kwa ukosefu wa uwiano katika uripoti wa CCM na vyama vya upinzani katika vyombo vya habari vinavyomilikiwa na serikali. CCM na wagombea wake walipata uripoti mkubwa zaidi ikilinganishwa na vyama vya upinzani na wagombea wao.

Matokeo yanaonesha kuwa uripoti wa vyombo vya habari kuhusu uwezekano wa utekelezaji wa ahadi za wagombea wakati wa uchaguzi ulikuwa mdogo, ambapo ni asilimia 14 tu ya maudhui ya vyombo vya habari yaliyogusia kipengele hiki. Kwa kuzingatia jukumu muhimu la vyombo vya habari wakati wa uchaguzi, upungufu huu mkubwa wa kitaaluma unatoa tahadhari, kwani vyombo vya habari vina wajibu wa kuhoji misingi ya ahadi zinazotolewa na wagombea na hivyo kuwawezesha wapiga kura kufanya maamuzi sahihi. Wajibu huu wa vyombo vya habari ndio unaochochea na kuimarisha demokrasia.

Matokeo yanaonesha kuwa uripoti wa vyombo vya habari kuhusu uwezekano wa utekelezaji wa ahadi za wagombea wakati wa uchaguzi wa mwaka 2025 ni kama haukuwepo kabisa, ambapo ni asilimia 1 tu ya maudhui ya vyombo vya habari yaliyogusia kipengele hiki. Kwa kuzingatia jukumu muhimu la vyombo vya habari wakati wa uchaguzi, upungufu huu mkubwa wa kitaaluma unatoa tahadhari kubwa, kwani vyombo vya habari vina wajibu wa kuhoji misingi na ahadi zinazotolewa na wagombea na hivyo kuwawezesha wapiga kura kufanya maamuzi sahihi. Wajibu huu wa vyombo vya habari ndio unaochochea na kuimarisha demokrasia.

Utafiti huu unaonesha kuwa ubora wa utendaji wa uandishi wa habari haujaimarika kwa kiwango kikubwa, isipokuwa kwa ongezeko dogo katika baadhi ya viashiria vya ubora. Kwa mfano, idadi ya vyanzo vya wanawake imeongezeka kutoka asilimia 20 hadi asilimia 38, na vyombo vya habari vimeendelea kujikita zaidi katika sera za wagombea badala ya haiba zao.

Mapendekezo:

Kutokana na matokeo haya, utafiti unapendekeza yafuatayo kwa wadau husika:

Vyombo vya habari

- **Utekelezekaji wa ahadi za wagombea–** Kuandaa programu za kujenga uwezo kwa waandishi wa habari ili kuyashughulikia mapungufu ya uripoti yaliyobainishwa na utafiti huu, hususan hitaji la kutathmini uwezekano wa utekelezaji wa ahadi za wagombea. Vyombo vya habari na wadau wengine wanapaswa kushirikiana na wataalamu wa uhakiki wa taarifa (fact-checkers) ili kuhakiki kwa uhuru madai na ahadi za wagombea. Ushirikiano huu unaweza kuimarisha uripoti wenye kina na ubora zaidi.

- **Kuboresha uwakilishi wa sauti za wananchi –** Vyombo vya habari, hususan redio za kitaifa na kijamii, kwa kushirikiana na mashirika yenye mtazamo unaofanana, vinapaswa kuzingatia kuanzisha mipango ya uripoti wa kijamii pamoja na vipindi maalum vinavyohamasisha uandishi wa habari wa wananchi (citizen journalism), ili kuwawezesha wanajamii kuripoti masuala ya eneo lao na kushiriki katika mchakato wa uchaguzi. Hii inaweza kusaidia kuongeza utofauti wa sauti katika uripoti wa vyombo vya habari. Aidha, vinapaswa kuandaa majukwaa ambapo wananchi wanaweza kuwasiliana moja kwa moja na wagombea na kueleza hoja zao, huku mijadala hiyo ikiripotiwa na vyombo vya habari.

- **Kuongeza uwakilishi wa wagombea wasiopewa nafasi ya kutosha –** Vyombo vya habari vinaweza kuanzisha vipindi au sehemu maalum vinavyoangazia wagombea wasiojulikana sana, ambao wengi wao ni vijana na wanawake, ili kuwapa fursa ya kuwasilisha ajenda zao na kushirikiana na wapiga kura. Vilevile, vinapaswa kuhakikisha kunakuwa na uwakilishi wa haki na usawa, hususan kwa vijana, wanawake, na wagombea kutoka makundi maalumu

- **Kutafuta vyanzo endelevu vya kifedha –** Kutokana na changamoto zinazovikabili vyombo vya habari katika uendeshaji wake, vinapaswa kuendelea kutafuta vyanzo mbadala vya mapato ili kuongeza utofauti wa mapato yao. Katika juhudi hizi, ushirikiano kati ya vyombo vya habari vyenyewe pamoja na kati ya vyombo vya habari na mashirika yenye malengo yanayofanana ni muhimu. Aidha, serikali na washirika wa maendeleo wanapaswa kuzingatia kutoa ruzuku za kifedha kwa vituo vya redio za kijamii ili kukuza uandishi wa habari huru nyakati za uchaguzi.

- **Kuimarisha uhuru wa vyombo vya habari–** Vyombo vya habari, wataalamu wa habari na watetezi wa haki, wanapaswa kushirikiana na mashirika ya kiraia kushawishi sera na mifumo ya udhibiti inayolinda uhuru wa vyombo vya habari. Hii inaweza kujumuisha kushinikiza sheria zinazozuia udhibiti (censorship) na kukuza uwazi katika uendeshaji wa vyombo vya habari. Aidha, taasisi za kitaaluma za vyombo vya habari zinaweza kushirikiana na wataalamu wa sheria kupinga matukio ya matumizi mabaya ya mamlaka ya dola na kulinda utekelezaji wa Katiba.

Serikali

Ili kuboresha utendaji wa vyombo vya habari vinavyomilikiwa na serikali, mamlaka za udhibiti wa vyombo vya habari zinapaswa kuvifuatilia vyombo hivyo kwa namna ile ile wanavyovifuatilia vingine. Uangalizi huu unaweza kuhakikisha kuwa vyombo vya habari vya serikali vinatimiza wajibu wao wa kisheria na kitaaluma wakati wa uchaguzi kwa kutoa uripoti wa haki na usawa kwa wagombea na vyama vyote vinavyoshiriki uchaguzi.

Wadau wa maendeleo

Washirika wa maendeleo wanapaswa kuzingatia kutoa msaada wa kimkakati kwa vyombo vya habari katika maeneo yafuatayo: mafunzo ya usimamizi wa vyombo vya habari na uendelevu wa kifedha, mafunzo ya vyombo vya habari mtandaoni, pamoja na msaada kwa vituo vya redio vya kijamii. Kwa kuzingatia changamoto za kifedha zinazoongezeka zinazovikabili vyombo vya habari nchini, ni muhimu kuweka kipaumbele katika mafunzo ya usimamizi na uendelevu wa kifedha wa vyombo vya habari. Programu nyingi za mafunzo zilizopo zimejikita zaidi katika uandishi wa habari, huku zikipuuza kipengele hiki muhimu cha uendeshaji wa vyombo vya habari. Kadiri idadi ya vyombo vya habari mtandaoni inavyoendelea kuongezeka na usajili wa huduma za intaneti kuimarika kwa kiasi kikubwa, ni muhimu kujumuisha mafunzo ya vyombo vya habari mtandaoni kama sehemu ya juhudi za kuimarisha sekta ya habari. Mtazamo huu pia unapaswa kutumika kwa vituo vya redio za kijamii katika mikoa yote, nchini Tanzania.

Kiambatisho

Vyombo vya kimataifa vilivyoangaziwa		
Chombo cha habari	**Vyombo vya habari vya kimataifa**	**Habari zilizoangaziwa**
CITIZEN TELEVISION	The Citizen TV (Kenya)	• Tanzania, Oh Tanzania! • Machafuko nchini Tanzania: waandamanaji wakabiliana na polisi mitaani • CHADEMA yapinga ushindi wa Samia • Genge la Habari: Tanzania, mwisho wa upole
ALJAZEERA	Al Jazeera	• Uchaguzi Tanzania: Upinzani wasema kwa uchache watu 700 wameuliwa kwenye vurugu za ukandamizaji • Kipindi cha The Al Jazeera Inside Story: *Nini kinachosababisha ghasia Tanzania baada ya rais kuchaguliwa tena?* • Kipindi cha The Al Jazeera Inside Story "*Je Tanzania inaelekea kwenye machafuko zaidi?*" • Rais Samia aapa baada ya uchaguzi wa kikatili nchini Tanzania
The Sun UK Edition	The Sun (UK edition)	• Kutana na dhalimu wa Afrika 'Mchinjaji wa Tanzania' ambaye 'aliwaua watu wake 10,000 na kutupa miili kwenye makaburi ya halaiki'
THE SUNDAY TIMES	The Sunday Times	• Jinsi Tanzania ilivyojikuta chini ya utawala wa mkono wa chuma wa 'Idi Amin mama'
AP	AP	• Upinzani Tanzania watoa wito kuwepo kwa serikali ya mpito baada ya uchaguzi uliopingwa
Reuters	Reuters	• Hassan wa Tanzania atangazwa mshindi kwa wingi wa kura katika uchaguzi uliopojaa vurugu • Serikali ya Tanzania yawataka wananchi kubaki nyumbani kabla ya maandamano yanayotarajiwa
The Telegraph	The Telegraph	• Moja ya mataifa thabiti zaidi Afrika sasa iko katika shida. Hii ndiyo sababu kwa nini tunaliangalia suala hili
DAILY NATION	Daily Nation	• Giza kisha risasi na mabomu ya kutoa machozi: Kukutana kwangu na kifo nchini Tanzania
rfi	RFI	• Umoja wa Mataifa wahuzunishwa na ripoti za vurugu za kikatili za uchaguzi nchini Tanzania • Tanzania yakanusha kutumia nguvu dhidi ya waandamanaji, yakanusha watu 700 kuuawa
THE CONVERSATION	The Conversation	• Tanzania: madaraka ya Rais Samia Hassan yaathiriwa na maandamano yasiyo na kifani
FRANCE 24	France 24	• Jinsi Rais wa Tanzania Samia Suluhu Hassan alivyotoka katika mageuzi hadi ukandamizaji
The Standard	The Standard (Kenya)	• Kwa nini wataalamu wanasema Tanzania haikuwa na uchaguzi halisi • Giza Dar es Salaam • Africa's sham polls • Uchaguzi wa udanganyifu barani Afrika Muaji ya kimbari Tanzania • Taji lililojaa damu
DAILY MAVERICK	Daily Maverick	• Katika ukimya na giza la kidijitali, waliwaua Watanzania.

Vyombo vya kimataifa vilivyoangaziwa

Chombo cha habari	Vyombo vya habari vya kimataifa	Habari zilizoangaziwa
CNN	CNN	• Upinzani Tanzania wadai polisi walitupa miili baada ya vurugu za uchaguzi • Rais wa Tanzania awakingia kifua polisi baada ya mauaji ya mamia kwenye maandamano ya uchaguzi wa Oktoba • "Oh Mungu wangu, hii ndiyo Tanzania yetu': Uchunguzi wa CNN unaonyesha polisi wakiwapiga risasi waandamanaji, ishara ya makaburi ya halaiki
The Economist	The Economist	• Msimkubali dikteta mpya wa Afrika
The Washington Post	The Washington Post	• Rais wa Tanzania ashinda uchaguzi uliopingwa ukihusishwa na maandamano na vifo • Familia zinatafuta miili nchini Tanzania baada ya mauaji ya halaiki ya kisiasa
DW	DW	• Ukatili uliofanyika Tanzania 'gizani' waanza kudhihirika
BBC	BBC	• Waandamanaji wanaopinga uchaguzi Tanzania wapingana na mkuu wa majeshi huku hofu ikitanda kuhusu idadi ya vifo

Imetolewa na:
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano kwa Umma
S.L.P 4067 Mikocheni B, Mtaa wa Makaburi Street,
Plot Block D, No.34 Simu: +255 (22) 2700756 Dar es Salaam, Tanzania
Barua pepe: sjmc@udsm.ac.tz yearbookmediatz@gmail.com
Tovuti: www.udsm.ac.tz

Schweizerische Eidgenossenschaft
Confédération suisse
Confederazione Svizzera
Confederaziun svizra
Embassy of Switzerland in Tanzania

UK International Development
Partnership | Progress | Prosperity

UBORA WA MAUDHUI YA
VYOMBO VYA HABARI TANZANIA

Upembuzi wa Mhimili wa Nne:
Uripoti wa Vyombo Vya Habari Katika Uchaguzi wa Mwaka 2025 Tanzania



1. Leila Rajab Khamis (NCCR-Mageuzi)
2. Ameir Hassan Ameir (Chama cha Makini)
3. Hamad Rashid Mohammed (ADC)
4. Mfaume Khamis Hassan (NLD)
5. Juma Ali Khatib (ADA Tadea)
6. Othman Masoud Othman (ACT)
7. Hamad Ibrahim Mohamed (UPDP)
8. Hussein Juma Salum (TLP)
9. Mgau Kombo Mgau kutoka (NRA)
10. Said Soud (AAFP)